# RIPOTI YA TUME YA BLAIR KUHUSU AFRIKA

## (RASIMU YA TAFSIRI)

## 2005

Tume ya A

# Utangulizi

## Kuhusu Ripoti Hii

Mwaka huu ni muhimu sana kwa Afrika. Mwaka huu dunia itatafakari maendeleo ya ahadi zisizo kifani ilizotoa mwaka 2002. Malengo ya Maendeleo ya Milenia yalilenga kupunguza kwa nusu umasikini duniani ifikapo 2015. Lakini leo hii tumemaliza theluthi ya muda huo na nchi tajiri ziko nyuma sana katika utekelezaji wa ahadi zao kwa nchi masikini. Hakuna mahali ambapo hali hiyo inadhihirika zaidi kama Afrika ambapo dunia iko nyuma sana katika hatua za kutimiza ahadi zake za dhati. Ikiwa tunataka hali hii ibadilike sharti tuchukue hatua sasa.

Lakini siyo kiza tupu. Kwani mwaka 2005 ndipo pia inaanza kueleweka vema kwa dunia kwamba mambo yanaanza kubadilika kwenye bara hili – kwa serikali za Afrika kuonyesha mwelekeo mpya – kwa serikali moja-moja na kwa pamoja – kupitia Umoja wa Afrika na mpango wake wa Ushirikiano kwa Maendeleo ya Afrika (NEPAD). Hatimaye, Afrika imekusudia kujikwamua.

Mwaka mmoja uliopita, Waziri Mkuu wa Uingereza alikusanya watu 17 na kuunda Tume ya Afrika. Tulialikwa kama watu binafsi na siyo wawakilishi wa serikali au asasi. Wengi wetu wanatoka Afrika na tuna uzoefu mbalimbali kama viongozi wa siasa, watumishi wa serikali na katika sekta ya binafsi. Jukumu tulilojipa ni hili: Kubaini changamoto zinazoikabili Afrika na kutoa mapendekezo ya wazi juu ya kusaidia kuleta mabadiliko na kupunguza umasikini.

Tulianza kwa kutambua kwamba sharti Afrika iendeshe maendeleo yake. Nchi tajiri hazina budi kuunga mkono, kwani ni kwa maslahi yetu sote kufanya dunia nzima kuwa mahali pa ustawi zaidi na salama – ingawa jumuia ya kimataifa itachangia kwenye shabaha hizi kwa njia mbalimbali. Lakini kilicho wazi ni kwamba iwapo Afrika haitajenga mazingira mwafaka kwa maendeleo, basi kiwango chochote cha msaada kutoka nje kitashindwa kuleta mabadiliko.

Mapendekezo yetu yamejengwa kwenye mambo mawili: Tulichunguza kwa makini ushahidi wote uliopo ili kugundua kipi kinawezekana na kipi hakiwezekani. Vilevile tulitafuta ushauri, tena kwa kiwango kikubwa, ndani na nje ya Afrika; kutoka serikalini, jumuia za kijamii, wasomi na wale waliomo katika sekta za umma na za binafsi.

Tumekutana na watu binafsi na vikundi kutoka kila kanda na nchi 49 kutoka Afrika na kutoka nchi za kundi la nchi tajiri zenye viwanda (G8), China, India, na Ulaya. Tumepokea karibu mawasilisho 500 na tumefanya juhudi maalum kushauriana na Waafrika wanaoishi nje ya bara hili. Tunawashukuru kwa dhati watu binafsi na vikundi kwa michango yao.

Ripoti yetu imo katika sehemu mbili: Kwanza, **Hoja,** ambayo inajielekeza kwa hadhira pana na ambayo inatoa kwa uwazi kabisa wito wa kuchukua hatua. Pili, **Uchambuzi na Ushahidi,** ambayo inajenga kiini na msingi wa mapendekezo yetu ili yawe na mashiko mbele ya umma. Mapendekezo yetu yamo katikati ya sehemu hizi mbili.

Ripoti yetu imeandikwa kwa ajili ya hadhira mbalimbali. Tunalenga kwa wale wanaotoa maamuzi katika Afrika ambao sharti sasa waendeshe programu ya mabadiliko waliyojiwekea. Tunalenga nchi tajiri zenye viwanda na zenye nguvu duniani ambazo viongozi wake watakutana kama Kundi la G8 huko Gleneagles, Scotland, Julai 2005

ambako wanapaswa kuonyesha mfano wa kuchukua hatua tofauti na msimamo wao wa sasa. Tunalenga jumuia ya kimataifa ambayo sharti ithibitishe kuchukua hatua kubwa na za haraka juu ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia kwenye Umoja wa Mataifa, Septemba mwaka huu – na ambayo inapaswa kuchukua hatua thabiti kwenye mazungumzo ya Shirika la Biashara Duniani yatakayofanyika Desemba huko Hong Kong.

Aidha, tunalenga watu wa Afrika na dunia kwa ujumla. Kwani ni hao wanaopaswa kudai kuchukuliwa kwa hatua. Ni king'ang'anizi chao pekee ambacho kinaweza kufanya viongozi wao wa kisiasa kuchukua hatua thabiti na endelevu.

Hatua tunazopendekeza ni mpango madhubuti wa Afrika. Sharti zitekelezwe kwa pamoja. Mwaka 2005 ni wa kuchukua maamuzi ambayo yatadhihirisha kwamba tuko makini juu ya kugeuza ndoto yetu – ya Afrika yenye nguvu na ustawi – kuwa ya kweli.

Tony Blair (Mwenyekiti)

Fola Adeola
K Y Amoako
Nancy Kassebaum Baker
Hilary Benn
Gordon Brown

Ji Peiding
William Kalema
Trevor Manuel
Benjamin Mkapa
Linah Mohohlo

# Yaliyomo


| | Ukurasa |
|---|---|
| **Utangulizi: Juu ya Ripoti hii** | 2 |
| **Finyazo** | 5 |
| **Muhtasari Maalum** | 8 |
| **Sehemu 1: Hoja** | 13 |
| **Mapendekezo** | 63 |

# Finyazo

| | |
|---|---|
| ACP | Nchi za Afrika, Karibea na Pasifiki |
| ADB | Benki ya Maendeleo ya Afrika |
| ADEA | Chama cha Maendeleo ya Elimu Afrika |
| AECF | Mfuko wa Kukuza Biashara Afrika |
| AGOA | Sheria ya Maendeleo na Fursa Afrika |
| AIDS | Ukosefu wa Kinga Mwilini (UKIMWI) |
| AMU | Umoja wa Waarabu wa Maghrebu |
| APCI | Juhudi za Kuinua Uwezo wa Uzalishaji Afrika |
| APEC | Ushirikiano wa Kiuchumi wa Asia na Pasifiki |
| APRM | Mbinu za Uhakiki-Rika Afrika |
| ART | Dawa za Kurefusha Maisha |
| ASF | Jeshi la Akiba la Afrika |
| ATT | Mkataba wa Biashara ya Silaha |
| AU | Umoja wa Afrika |
| CAFOD | Shirika la Kikatoliki la Maendeleo ya Kimataifa |
| CAP | Sera ya Pamoja ya Kilimo |
| CEMAC | Jumuiya ya Uchumi na fedha ya Afrika ya Kati |
| CEN-SAD | Jumuiya ya Nchi za Sahel-Sahara |
| CEPGL | Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Maziwa Makuu |
| CET | Ushuru wa Nje wa Pamoja |
| CGIAR | Kikundi cha Ushauri wa Kilimo wa Kimataifa |
| CHGA | Tume ya VVU/UKIMWI na Utawala Afrika |
| COMESA | Soko la Pamoja la Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika |
| CPIA | Sera ya Nchi na Tathmini ya Kisiasa |
| CSR | Wajibu wa Kijamii wa Shirika |
| CWS | Mfumo wa Hadhari wa Bara (la Afrika) |
| DFID | Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza |
| DRC | Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo |
| DIT | Wizara ya Biashara na Viwanda ya Uingereza |
| EAC | Jumuia ya Afrika Mashariki |
| EBA | Kila Kitu Isipokuwa Silaha |
| ECA | Tume ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa kwa Afrika |
| ECCAS | Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika ya Kati |
| ECOSOC | Baraza la Uchumi na Maendeleo ya Jamii la Umoja wa Mataifa |
| ECOWAS | Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika Magharibi |
| EFA | Elimu kwa Wote |
| EIB | Benki ya Raslimali ya Ulaya |
| EITI | Juhudi Dhahiri za Kukuza Viwanda Sindikaji |
| EPA | Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi |
| EU | Umoja wa Ulaya |
| EUREP-GAP | Makubaliano ya Wachuuzi wa Ulaya Kuhusu Kilimo Bora |
| FATF | Kikosi cha Kazi cha Masuala ya Fedha |
| FDI | Uwekezaji wa Moja kwa Moja toka Nje |
| FTA | Mkataba wa Biashara Huria |
| GATS | Makubaliano ya Jumla ya Biashara ya Huduma |
| GATT | Makubaliano ya Jumla ya Ushuru na Biashara |

| | |
|---|---|
| GAVI | Umoja wa Chanjo Duniani |
| GCOS | Mfumo wa Uchunguzi wa Hali ya Hewa Duniani |
| GDP | Zao Ghafi la Ndani |
| GER | Kiwango Ghafi cha Uandikishaji |
| GIS | Mfumo wa Taarifa za Kijiografia |
| GNI | Pato Ghafi la Taifa |
| GNP | Zao Ghafi la Taifa |
| GSB | Juhudi Endelevu za Kibiashara |
| GSP | Mfumo Jumuifu wa Aula |
| HIPC | Nchi Zenye Madeni Makubwa |
| HIPC AAP | Mpango wa Utekelezaji na Taathmini wa Nchi Zenye Madeni Makubwa |
| HIV | VVU |
| HMT | Hazina ya Uingereza |
| IAC | Baraza la Vyuo |
| IBLF | Mkutano wa Viongozi wa Biashara ya Kimataifa |
| ICF | Fursa za Uwekezaji |
| ICT | Tekinolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKINOHAMA) |
| IDA | Chama cha Maendeleo ya Kimataifa |
| IDP | Mkimbizi wa Ndani |
| IFF | Fursa za Fedha Kimataifa |
| IFFim | Fursa za Fedha za Chanjo Kimataifa |
| IFI | Asasi ya Fedha Kimataifa |
| IGAD | Mamlaka ya Maendeleo Baina ya Serikali |
| ILO | Shirika la Kazi Duniani la Umoja wa Mataifa |
| IMF | Shirika la Fedha la Kimataifa |
| IOC | Tume ya Bahari ya Hindi |
| IPPF | Fursa za Uandaaji wa Miradi ya Miundombinu |
| LDC | Nchi Masikini Sana |
| LIC | Nchi yenye Pato Dogo |
| MCT | Uambukizi wa Mama kwa Mtoto |
| MDG | Lengo la Maendeleo la Milenia |
| MFI | Asasi za Mitaji Midogo |
| MFN | Taifa Linalopendelewa Zaidi |
| MIGA | Wakala Dhamini wa Uwekezaji |
| MIIU | Kitengo cha Uwekezaji wa Miundombinu ya Manispaa |
| MRU | Umoja wa Mto Mano |
| NATO | Umoja wa Kujihami wa Nchi za Magharibi |
| NEPAD | Ushirikiano Mpya kwa Maendeleo ya Afrika |
| NGO | Asasi Zisizo za Kiserikali |
| NTB | Kikwazo Kisicho cha Kiushuru |
| OAU | Umoja wa Nchi Huru za Afrika |
| OCHA | Ofisi ya Uratibu wa Maswala ya Kibinadamu ya Umoja wa Mataifa |
| ODA | Msaada Rasmi wa Maendeleo |
| OECD | Shirika la Ushirikiano wa Uchumi na Maendeleo |
| OECD/DAC | Shirika la Ushirikiano wa Uchumi na Maendeleo/Kamati ya Misaada ya Maendeleo |
| OED | Idara ya Tathmini ya Utendaji |
| PARIS21 | Ushirikiano wa Kitakwimu kwa Maendeleo ya Karne ya 21 |
| PEFA | Uwajibikaji wa Fedha na Matumizi ya Umma |
| PEM | Menejimenti ya Matumizi ya Umma |
| PFM | Menejimenti ya Fedha za Umma |
| PIDG | Kikundi cha Maendeleo ya Miundombinu Binafsi |

| | |
|---|---|
| PPIAF | Fursa za Ushauri wa Miundombinu na Umma na Binafsi |
| PPP | Usawa wa Uwezo wa Manunuzi |
| PRGF | Fursa za Ukuaji na Upunguzaji Umasikini |
| PRI | Bima ya Majanga ya Kisiasa |
| PRSP | Mkakati wa Upunguzaji Umasikini |
| REC | Jumuia ya Uchumi ya Kikanda |
| ROSC | Ripoti ya Uzingativu wa Viwango na Misimbo |
| SACU | Umoja wa Forodha wa Nchi za Kusini mwa Afrika |
| SADC | Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika |
| SALW | Silaha Ndogo na Nyepesi |
| SDR | Haki Maalum za Utoaji Fedha |
| SDT | Huduma Maalum na ya Upendeleo |
| SIDA | Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden |
| SME | Miradi Midogo na ya Kati Kiuchumi |
| SPS | Viwango vya Usafi |
| STAP | Mpango wa Muda mfupi wa Utekelezaji |
| SUF | Fursa za Kuboresha Makazi Yasiyopimwa Mijini |
| SWAP | Mkataba wa Sekta Nzima |
| TB | Tiibi (TB), Kifua Kikuu |
| TRIPS | Haki Miliki Taaluma za Biashara |
| UK | Uingereza |
| UN | Umoja wa Mataifa |
| UNAIDS | Programu ya Pamoja ya Umoja wa Mataifa Dhidi ya VVU/UKIMWI |
| UNCAC | Makubaliano ya Umoja wa Mataifa Dhidi ya Rushwa |
| UNCTAD | Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Biashara na Maendeleo |
| UNDP | Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa |
| UNEP | Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa |
| UNESCO | Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa |
| UNFCCC | Makubaliano ya Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Hali ya Hewa |
| UNFPA | Mfuko wa Idadi ya Watu ya Umoja wa Mataifa |
| UNGA | Baraza la Umoja wa Mataifa |
| UNGASS | Kikao Maalum cha Umoja wa Mataifa |
| UN-HABITAT | Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa |
| UNHLP | Jopo la Mabingwa wa Umoja wa Mataifa la Maswala ya Matishio, Changamoto na Mabadiliko |
| UNICEF | Shirika la kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa |
| UNIDO | Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa |
| UPC | Uhitimu wa Elimu ya Msingi kwa Wote |
| URAA | Makubaliano ya Uruguai Kuhusu Kilimo |
| WAEMU | Umoja wa Uchumi na Fedha wa Nchi za Afrika Magharibi (pia UEMOA) |
| WHO | Shirika la Afya Duniani |
| WSIS | Mkutano wa Kilele wa Dunia wa Teknolojia na Habari |
| WTO | Shirika la Biashara Duniani |
| YBI | Shirika la Biashara za Vijana la Kimataifa |
| YEN | Mtandao wa Ajira kwa Vijana |

# Muhtasari Rasmi

***Umasikini wa Afrika na kudorora ndio msiba mkubwa kuliko yote kwa Afrika. Umasikini wa kiwango hicho unahitaji jibu la nguvu. Na Afrika – kwa ngazi ya nchi moja, kanda na bara zima – inajenga misingi imara ya kukabiliana na matatizo yake. Miaka ya hivi karibuni imeshuhudia uboreshaji katika kukua kwa uchumi na utawala. Lakini Afrika inahitaji yote hayo mawili kwa kiwango kikubwa zaidi ili iweze kukabili umasikini. Kufanya hivyo kunahitaji ushirikiano kati ya Afrika na nchi zilizoendelea; ushirikiano ambao utazingatia kikamilifu uanuwai na mazingira maalum ya Afrika.***

Kwa upande wake, sharti Afrika iharakishe mabadiliko. Na nchi zilizoendelea sharti ziongeze na kuboresha misaada yao na kuacha kufanya mambo yanayozuia maendeleo ya Afrika. Nchi zilizoendelea zinastahili kusaidia Afrika kwa kuwa ni jukumu lao kimaadili na kwa kuwa zinasukumwa na nia thabiti itokanayo na maslahi yao binafsi. Tunaamini kwamba huu ndio wakati mwafaka ambapo msaada mkubwa kutoka nje unaweza kuwa wa manufaa; vilevile huu ndio wakati muhimu kwa dunia kuunga mkono juhudi za Afrika.

Hatua zinazopendekezwa na Tume ndizo mpango madhubuti wa kuendeleza Afrika. Matatizo ambayo njia hizo zinazingatia yanaingiliana. Ni duara la maangamizi yanayoimarishana (vicious circle). Matatizo hayo sharti yakabiliwe kwa pamoja. Ili ifanye hivyo, Afrika inahitaji uwezo mkubwa katika medani mbalimbali na kwa wakati mmoja. Washirika hawana budi kufanya kazi pamoja kutekeleza mapendekezo kwa moyo, uvumilivu na kasi; kila mmoja akilenga namna ya kutoa mchango wenye mafanikio zaidi.

## Urekebishaji wa Mifumo: Utawala na Uwezeshaji

Historia ya Afrika katika miaka 50 iliyopita imetiwa doa na maeneo mawili ya udhaifu. Maeneo haya ni uwezo (mdogo) – uwezo wa kuandaa na kutekeleza sera, na **uwajibikaji** – jinsi ambavyo dola linapaswa kuwajibika kwa watu wake. Maboresho katika maeneo haya ni jukumu la nchi za Afrika na watu wake. Lakini hatua za vitendo za nchi tajiri ni muhimu pia.

Ujenzi wa uwezo huchukua muda mwingi na huhitaji moyo. Udhaifu huletwa na mifumo na vishawishi dhalili, ukosefu wa taarifa, ukosefu wa stadi za ufundi, kutokuwa na watumishi wenye ujuzi na ukosefu wa fedha. Tunapendekeza kwamba wafadhili wafanye uwekezaji mkubwa wa kuboresha uwezo wa Afrika, kwa kuanzia na mifumo ya elimu ya juu, hasa katika sayansi na teknolojia. Hawana budi kusaidia kujenga mifumo na watumishi kwa ngazi ya taifa na ngazi ya tawala za mitaa, lakini pia kwa ngazi ya bara la Afrika na mashirika ya kanda, hasa Umoja wa Afrika na mpango wake wa NEPAD. Wafadhili hawana budi kubadili tabia zao na kuunga mkono vipaumbele vya serikali za Afrika badala ya kuweka mbele taratibu zao na shauku yao maalum katika kuhujumu juhudi za kujenga uwezo wa nchi.

Uboreshaji wa uwajibikaji ni jukumu la viongozi wa Afrika. Wanaweza kufanya hivyo kwa kupanua wigo wa ushirikishaji wa watu wa kawaida katika hatua mbalimbali serikalini, na pia kuimarisha asasi kama bunge, serikali za mitaa, vyama vya wafanyakazi, mifumo ya haki na vyombo vya habari. Wafadhili wanaweza kusaida katika hili. Wanaweza pia kusaidia kujenga uwajibikaji katika bajeti ili watu wa Afrika waweze kuona jinsi fedha zinavyokusanywa na wapi zinakotumika.

Uwazi wa aina hiyo unaweza kusaidia kukabili ufisadi ambao serikali za Afrika sharti ziung'oe. Nchi zilizoendelea zinaweza pia kusaidia katika hili. Fedha na mali ya umma vilivyoibwa na viongozi wala rushwa na kupelekwa nchi za nje, sharti virejeshwe. Benki za nje zitakiwe kisheria kutoa taarifa juu ya akaunti zinazotiliwa shaka. Wale wanaotoa hongo sharti nao washughulikiwe na makampuni ya nje yaliyomo kwenye biashara ya mafuta, madini na viwanda vingine vya uchimbaji, sharti yafanye malipo yao kuwa wazi zaidi, kiasi kwamba yanaweza kupekuliwa kwa manufaa ya umma. Makampuni ambayo yanahonga yanyimwe mikopo katika biashara zao za nchi za nje.

Bila maendeleo katika utawala, mabadiliko mengine yote yatakuwa ya mafanikio haba.

## Umuhimu wa Amani na Usalama

Hatua ya juu mno ya kuvunjika kwa utawala ni vita. Afrika imekumbwa na migogoro ya kivita kuliko bara lolote katika miongo minne iliyopita. Katika miaka ya karibuni hali imekuwa ahueni katika nchi nyingi, lakini katika sehemu nyingine migogoro ya kivita bado ni kikwazo kikubwa kuliko vyote katika maendeleo. Uwekezaji katika maendeleo ni uwekezaji katika amani.

Njia bora ya kukabili migogoro – kwa kuokoa maisha na fedha – ni kujenga uwezo wa dola na jamii za Afrika wa kuzuia na kusimamia migogoro hiyo. Hii ina maana ya kutumia misaada ipasavyo ili kukabili vyanzo vya migogoro. Ina maana ya uboreshaji wa menejimenti ya mapato ya serikali kutoka maliasili na utekelezaji wa makubaliano ya kimataifa juu ya usimamizi wa "raslimali za migogoro" ambazo huchochea uadui. Vilevile ina maana ya kuzuia biashara ya silaha ndogo.

Mashirika ya kanda ya Afrika na UN yanaweza kusaidia kuzuia na kusuluhisha migogoro wakati mivutano itakaposhindikana kumalizwa kwenye ngazi ya taifa, kwa mfano kwa njia ya kutoa tahadhari mapema juu ya mgogoro, usuluhishi au kwa kupeleka majeshi ya

kulinda amani. Wafadhili wanaweza kusaidia katika hili kwa kutoa fedha kwa UA na mashirika ya kanda ya Afrika; na kwa kuunga mkono uundwaji wa Tume ya Umoja wa Mataifa ya kujenga amani. Uratibu na uwezeshaji kifedha wa ujenzi wa amani na maendeleo katika maeneo yaliyokuwa na migogoro, sharti uboreshwe ili kuzuia maeneo hayo kurejea upya katika mgogoro.

## Bila kubagua mtu: Uwekezaji katika watu

Umasikini siyo tu ukosefu wa matumizi. Watu masikini hawahusishwi katika utoaji maamuzi na hawapewi huduma za msingi ambazo serikali zinastahili kuwapa. Watu masikini sana katika Afrika sharti wapate huduma za kliniki na shule. Hili ni suala la haraka ambalo pia ni la haki ya msingi ya binadamu na haki ya kijamii. Bali pia ni suala la kiuchumi: Nguvukazi yenye afya na ujuzi itazalisha zaidi na kutimiza wajibu wao kwa heshima. Uwekezaji kwa ajili ya kukua kwa uchumi una maana ya ujenzi mpya wa mifumo ya afya na elimu ya Afrika ambayo sehemu yake kubwa hivi sasa iko kwenye hatua ya kusambaratika. Hili linahitaji uwekezaji mkubwa kifedha. Hata hivyo hili siyo tu suala la raslimali. Linahusu pia utendaji na matokeo yake. Haya yanaongezewa nguvu pale jamii zinaposhirikishwa katika kutoa maamuzi juu ya mambo yanayozihusu.

Ugharimiaji vizuri wa ahadi ya jumuia ya kimataifa wa elimu kwa wote utawezesha kutoa elimu ya msingi kwa wasichana na wavulana wote katika nchi za kusini mwa jangwa la Sahara na kuwawezesha kupata stadi zinazohitajika katika Afrika ya sasa. Elimu ya sekondari, elimu ya juu na elimu ya ufundi, elimu ya watu wazima na vyuo vya walimu havina budi kusaidiwa katika mfumo mzima wa elimu. Wafadhili wanahitaji kugharimia kile walichoahidi, ikiwa ni pamoja na gharama zinazotokana na kuondolewa kwa karo katika shule za msingi.

Utokomezaji wa magonjwa yanayozuilika katika Afrika utategemea hasa ujenzi mpya wa mifumo ya kutoa huduma ya afya kwa jamii ili kuweza kukabili ipasavyo magonjwa kama kifua kikuu na malaria. Hili litahitaji uwekezaji mkubwa katika watumishi, mafunzo, utengenezaji wa dawa mpya, huduma bora za uzazi na uondoaji malipo kwenye huduma ya tiba ambayo sharti yalipwe na wafadhili hadi nchi husika zitakapokuwa na uwezo. Ugharimiaji wa huduma ya maji na majitaka sharti uongezwe ili kubadili hali mbaya ambayo imekuwepo kwa miaka mingi.

Aula (kipaumbele) kiwe jinsi ya kuainisha huduma zinazohitajika kukabili janga la VVU na ukimwi ambao unaua watu wengi zaidi katika Afrika kuliko sehemu nyingine yoyote duniani. Lakini hii, sharti ifanywe kupitia mifumo iliyopo kuliko mifumo mipya inayokinzana. Aidha, serikali hazina budi kusaidiwa kulinda watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu na makundi mengine ambayo, katika hali ya kawaida, yangeachwa nje ya mkondo wa maendeleo. Karibu nusu ya msaada wa nyongeza tunaopendekeza unastahili kutumiwa katika afya, elimu na VVU na ukimwi.

## Kukua kwa Uchumi na Upunguzaji Umasikini

Afrika ni masikini kwa kuwa uchumi wake haujakua. Sekta za umma na binafsi zinapaswa kufanya kazi pamoja kujenga mazingira ambayo yatafungulia ujasiriamali wa watu wa Afrika, kuleta ajira na kuhimiza watu binafsi na makampuni ya ndani na nje kuweka vitega uchumi. Yanahitajika mabadiliko katika utawala kufanya mazingira ya uwekezaji kuwa thabiti. Nchi zilizoendelea hazina budi kusaidia mpango wa NEPAD wa UA katika kujenga ushirikiano kati ya sekta za umma na binafsi ili kujenga mazingira mwafaka kwa ajili ya kukua kwa uchumi, vitegauchumi na ajira.

Ukuaji wa uchumi pia utahitaji uwekezaji mkubwa katika miundombinu ili kuvunja vikwazo vya ndani ambavyo vinaikwamisha Afrika. Wafadhili hawana budi kugharimia mara dufu uwekezaji katika miundombinu – kuanzia kwenye barabara na shughuli ndogo za umwagiliaji hadi ujenzi wa barabara kuu, reli, miradi mikubwa ya nishati na teknolojia, habari na mawasiliano (TEKINOHAMA). Uwekezaji huo sharti uhusishe maendeleo vijijini na katika makazi machafu na ya ujenzi wa ovyo mijini, ambao kama haukufanyika watu masikini wa Afrika hawataweza kushiriki katika ukuaji wa uchumi. Na sera za ukuaji sharti zihusishe – na siyo kubagua – makundi masikini sana kuliko yote. Itabidi uwepo msisitizo maalum kwa kilimo na katika kusaidia wajasiriamali wadogo, kwa kulenga hasa wanawake na vijana. Ili ukuaji huu uweze kuwa endelevu, sharti utunzaji wa mazingira na hatari zitokanazo na mabadiliko ya hali ya hewa viwe sehemu muhimu za mipango ya wafadhili na serikali. Mpango huu wa ukuaji unachukua theluthi ya jumla ya rasilimali za nyongeza tunazopendekeza.

## Biashara Zaidi na ya Haki

Afrika inakabiliwa na vizingiti viwili vikubwa katika biashara. Haizalishi bidhaa za kutosha zenye ubora au bei nzuri kuiwezesha kuingia kwenye masoko ya dunia. Na inakabiliwa na vikwazo vya biashara visivyokubalika, ambavyo kwa uwazi au uficho, hutoza kodi bidhaa za Afrika zinapoingia kwenye masoko ya nchi zilizoendelea.

Ili kuboresha uwezo wake wa kufanya biashara, Afrika inahitaji kufanya mabadiliko ya ndani. Sharti iboreshe miundombinu yake ya uchukuzi ili iwe rahisi kusafirisha bidhaa. Sharti ipunguze na irahisishe mifumo yake ya kodi kati ya nchi na nchi. Haina budi kurekebisha urasimu mkubwa uliopo, taratibu za kuchosha za forodha, na kuondoa ufisadi unayofanywa na watumishi wa umma. Sharti ihakikishe kwamba ni rahisi kuanzisha biashara. Lazima iendeleze uunganishaji wa uchumi katika jumuia za uchumi za kikanda katika bara hili. Wafadhili wanaweza kusaidia kugharimia mabadilko haya.

Bali nchi tajiri nazo sharti zivunje vikwazo ambavyo zimeziwekea bidhaa za Afrika, hasa katika kilimo. Vikwazo hivi vinaumiza raia katika nchi masikini na tajiri. Nchi tajiri sharti zikomeshe ruzuku zinayotoa kwa wakulima wake na biashara za kilimo. Ruzuku hii inawapa nafuu wakulima katika nchi zilizoendelea na kukuza ushindani wa bidhaa zao dhidi ya wakulima masikini wa Afrika. Nchi tajiri sharti zipunguze ushuru na vikwazo vingine vya biashara dhidi ya Afrika, ikiwa ni pamoja na kuacha kanuni za kujali zaidi "bidhaa zitokako" – kanuni ambazo hufanya bidhaa za Afrika zinyimwe upendeleo zinaostahili. Na sharti zionyeshe lengo hili kwa kukamilisha mazungumzo ya biashara ya kimataifa yanayoendelea huko Doha kwa njia ambayo haitakuwa inazifanya nchi tajiri kutaka zifanyiwe kile ambacho nchi masikini zinaomba. Unahitajika uangalifu mkubwa kuhakikisha kwamba watu masikini kuliko wote wanasaidiwa kunufaika na fursa mpya na kusaidiwa kuhimili vishindo vya mfumo ulio wazi zaidi wa biashara duniani. Afrika haina budi kupewa fedha ambazo zitaisaidia kujirekebisha na kujiweka tayari kwa mazingira mapya ya mfumo wa biashara uliobadilika.

## Fedha Zitatoka Wapi: Rasilimali

Ili kusaidia mabadiliko ambayo tayari yameanza katika Afrika, tunaomba nyongeza ya msaada wa dola bilioni 25 kila mwaka ifikapo 2010. Kutegemea uhakiki wa maendeleo wakati huo, kutakuwa na hatua ya pili itakayohitaji dola 25 bilioni kwa mwaka ifikapo 2015. Kuhakikisha kwamba fedha hizo zimetumika ipasavyo kutategemea mambo mawili: Kwanza, utawala bora katika Afrika sharti uendelee kupiga hatua. Lakini pili, wafadhili sharti waendelee kuimarisha, kwa kiwango kikubwa, ubora wa misaada na jinsi inavyotolewa. Hii ina maana kwamba kuwepo misaada zaidi, inayotabirika na

isiyoambatana na vikwazo, na kwamba taratibu za wafadhili hazichoshi tawala za Afrika ambazo tayari zimechoka. Misaada hii sharti pia iwe inachukuana na misaada ya wafadhili wengine na yote ikiwa inalingana na aula, taratibu na mifumo ya serikali za Afrika. Aidha, sharti misaada hiyo itolewe katika njia ambayo inaziacha serikali katika hali ya kuwajibika haswa kwa watu wake.

Mabadiliko haya hayategemewi tu kwa mfadhili mmoja-mmoja bali pia kwa mashirika ya kimataifa yaliyoko Afrika na duniani kote. Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) inahitaji kuongezewa nguvu, na majukumu ya Tume ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa (ECA) kwa Afrika yanahitaji kuendelezwa. Mashirika haya yanapaswa pia kuwajibika kwa wanahisa na wateja wao na kuipa Afrika sauti katika maamuzi.

Nchi tajiri hazina budi kuwa na ratiba ya kutoa asilimia 0.7 ya mapato yao ya mwaka kwa ajili ya misaada. Ili kuweza kutoa kiwango cha misaada inayohitajika hivi sasa, misaada hii sharti ipewe aula kupitia Fursa za Kifedha za Kimataifa (IFF) Mapendekezo ya kiutendaji sharti yafanywe ili kupata njia mpya za kupata fedha, kwa mfano ushuru wa kimataifa kwenye safari za anga ambao unaweza kuingiza fedha kwa matumizi ya muda wa kati na mrefu.

Kwa nchi masikini katika eneo la kusini mwa jangwa la Sahara ambazo zinahitaji misaada, shabaha haina budi kuwa ufutaji madeni kwa asilimia 100 na haraka iwezekavyo. Hii haina budi kuwa sehemu ya utoaji misaada kwa nchi hizi – ikiwa ni pamoja na zile ambazo hazimo kwenye mpango wa sasa wa kusamehewa madeni – ili kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDG) ya kupunguza umasikini kwa nusu ifikapo 2015 kama ilivyopendekezwa na jumuiya ya kimataifa kwenye mikutano ya Monterrey na Kananaskis.

## Hitimisho

Hatua madhubiti za kiwango kinachohitajika kukabili changamoto hizi zinaweza tu kuchukuliwa kupitia utaratibu mpya wa ushirikiano. Katika miaka ya nyuma njia za mikataba na masharti zilijaribiwa na kushindwa. Tunachopendekeza ni njia mpya ya maendeleo iliyojengwa kwenye misingi ya kuheshimiana na mshikamano, na yenye mizizi katika uchambuzi makini wa kinachotekelezeka. Kwa kuzingatia maendeleo mazuri ya hivi karibuni katika Afrika, hili linaweza kuongeza kasi ya maendeleo kuelekea kwenye dunia ya haki ambamo Afrika ni sehemu muhimu.

# Sehemu ya Kwanza

## Hoja

***Xamul aay na, laajtewul a ko raw.***
***Kutojua ni vibaya. Kutotaka kujua ni vibaya zaidi.***

*Methali ya Kiafrika maka*

***Batta li a ifi ise agoura li arin egun.***
***Aliyevaa viatu aweza kutembea kwenye miiba.***

*Methali ya Kiafrika*

Dunia imejaa utajiri kwa viwango ambavyo havijawahi kuonekana katika historia ya binadamu. Tofauti na utajiri wa miaka ya nyuma, ambao ulikuwa mikononi mwa watu wachache na binafsi waliobahatika na wale katika tabaka bora, utajiri wa sasa unashirikisha idadi kubwa ajabu ya watu wa kawaida duniani. Ukuaji katika nyanja mbalimbali na utandawazi vimeleta hali za juu za maisha kwa mabilioni ya wanaume na wanawake.

Hata hivyo siyo utajiri ambao kila mmoja anafaidi. Katika Afrika mamilioni ya watu wanaishi katika umasikini wa kutupwa na udhalili. Watoto wana njaa, miili yao imedumazwa na kulemazwa na utapiamlo. Hawawezi kusoma wala kuandika. Nisikuambie udhoofu wa miili yake wanalazimika kunywa maji machafu. Wale wanaoishi katika miji ya Afrika inayosambaa haraka na iliyojaa vibanda vya ovyo ni majirani wa malundo ya uchafu unaonuka na wanavuta hewa chafu.

Tunaishi katika dunia ambamo dawa na mbinu za matibabu vimeangamiza magonjwa mengi yaliyokera nchi zilizoendelea. Lakini katika Afrika watoto milioni nne wenye umri chini ya wa miaka mitano hufa kila mwaka. Theluthi mbili ya vifo hivyo hutokana na magonjwa ambayo gharama zake kuyaponya ni kidogo sana. Kwa mfano, malaria ndio ugonjwa unaoua watoto wengi wa Afrika na nusu ya idadi ya vifo hivyo. Ingeweza kuzuiwa iwapo wazazi wangepata dawa, ambayo gharama yake haizidi dola moja ya Marekani kwa dozi.

Tunaishi katika dunia ambako wanasayansi wanaweza kubaini viini vya uhai wa mtu na wamevumbua teknolojia ya kutengeneza viungo vya binadamu katika maabara. Wakati katika Afrika wanawake wapatao 250,000 wanakufa kila mwaka kutokana na matatizo ya ujauzito au wakati wa kujifungua.

Tunaishi katika dunia ambamo mtandao wa Intaneti kufumba na kufumbua, unaweza kusafirisha taarifa ambazo ubongo wa binadamu hauwezi kuhimili. Lakini katika Afrika, kila siku watoto wapatao milioni 40 hawana uwezo wa kwenda shule.

Tunaishi katika dunia ambamo, baada ya kukabiliwa na gonjwa linaloangamiza kuliko magonjwa yote yaliyowahi kuonekana – UKIMWI – imetengeneza dawa za kurefusha maisha (ARD). Lakini katika Afrika ambako watu milioni 25 tayari wameambukizwa, dawa hizo hazipatikani kwa urahisi. Hii ina maana kwamba watu milioni mbili watakufa kwa UKIMWI mwaka huu. Nchini Zambia, ifikapo mwaka 2010 kila mtoto wa tatu atakuwa yatima!

Tunaishi katika dunia ambamo nchi tajiri hutumia karibu dola za Marekani bilioni moja kila siku – kiasi kinacholingana na mapato ya watu wote wa Afrika – kama ruzuku kwa makampuni yanayotengeneza vyakula ambavyo havihitajiki. Lakini katika Afrika, njaa ni sababu kuu ya vifo kuliko jumla ya vifo vitokanavyo na magonjwa yote kwa pamoja.

Tunaishi katika dunia ambamo kila ng'ombe katika Ulaya anapata dola 2 kila siku kwa njia ya ruzuku – Kiasi ambacho ajabu kabisa, ni zaidi ya mara mbili ya mapato katika Afrika. Ng'ombe wa Japan anapata karibu dola 4.

Tofauti baini ya maisha ya wanaoishi katika nchi tajiri na masikini wanaoishi Afrika ndiyo kashfa kubwa kabisa ya nyakati zetu. Ili uzito wa udhalimu huu uweze kuelezeka vema unaweza kusema tunatumia mamilioni: lakini hatuna budi kukumbuka kwamba kila nyuma ya takwimu kuna mtoto mmoja anayethaminiwa na kupendwa. Kila siku mtoto huyo, na maelfu ya wengine kama yeye, anapambana ili aweze kupumua – ili waweze kuishi – na kwa maumivu na uchungu mkubwa atashindwa na kufa.

Utandawazi sharti uwe na maana pia ya haki kwa watu wote. Watu wa dunia wana silika ya hamu ya kusaidia wale waliomo katika matatizo. Mwitikio kwa janga la tsunami lililokumba pwani ya Bahari ya Hindi ulidhihirisha hivyo. Zaidi ya watu 300,000 walikufa wakati tetemeko la ardhi la aina yake katika miaka ya karibuni liliposukuma mawimbi baharini na kuharibu kila kitu kilichokuwa njia mwake hadi mwambao. Lilikuwa tukio maalumu la kuogofya na watu wa dunia waliitikia kwa michango ya fedha kwa kiwango ambacho hakijawahi kuonekana kokote.

Kuna tsunami kila mwezi katika Afrika. Lakini Wimbi lake la magonjwa na njaa linachukua maisha ya watu kimyakimya Katika bara hilo. Siyo tukio la kishindo na la kutia shauku na mara nyingi halionekani kuwa ni habari katika televisheni. Wahanga wake hufa kimyakimya, mbali ya macho ya jamii, wakiwa wamejificha katika makazi yao dhalili. Lakini Bali wanapukutika kwa wingi kama waliokufa kwa tsunami.

Macho ya dunia yaweza kuwa yameelekezwa kwingine lakini macho ya historia yametukodolea. Vizazi vijavyo vitaangalia nyuma katika historia na kushangaa ni vipi dunia iliyajua haya na ikashindwa kuchukua hatua.

## Kila mmoja anajua Afrika inahitaji nini…

Wakati Waziri Mkuu wa Uingereza, Tony Blair alipozindua Tume hii, watu wengi walihoji: "Tunahitaji Tume? Mbona kila mmoja anajua kile ambacho Afrika inahitaji!" Kwa hiyo tuliwauliza watu watwambie. Tulifanya mashauriano Afrika nzima na katika miji mikuu ya nchi tajiri. Tumechunguza utajiri mkubwa wa uchambuzi wa miaka 50 iliyopita na makosa ambayo yamedhihirika katika utoaji mikopo, maendeleo na menejimenti ya uchumi. Matokeo yake ni kwamba hivi sasa tumo katika hali bora ya kusema lipi linawezekana na lipi haliwezekani na kujifunza kutokana na kushindwa na mafanikio yaliyopita. Ripoti yetu imejengwa kwenye ushahidi na utendaji yenye mapendekezo yanayotokana na uchambuzi mwanana, hoja zinazotekelezeka na ushahidi.

Vilevile tumejitahidi kuwa waaminifu kabisa. Tunaoandika ni Makamishina 17, wengi wao wakiwa Waafrika; wengine ni watu binafsi kutoka baadhi ya nchi tajiri duniani, na tumejitahidi kusema ukweli mtupu popote pale tulipokumbana nao.

Tumekuwa wakweli na wawazi kuhusu rushwa, uzembe na migogoro katika Afrika. Vilevile tumekuwa wazi kuhusu ukosoaji wa mataifa yaliyoendelea. Sera zao zimeundwa rasmi kunufaisha matajiri bila kuwafikiria masikini. Wamesita kufuta madeni ambayo yanaendelea kufanya mzigo wa Afrika kuwa mzito kila kukicha. Mara nyingi sera za misaada yao zimeonekana kuwa zimeandaliwa kukidhi matakwa ya kisiasa na maendeleo ya viwanda vya nchi zilizoendelea na siyo kupunguza umasikini katika Afrika. Sehemu

kubwa ya historia ya kujihusisha kwa nchi tajiri katika Afrika ni historia ya ahadi za kusikitisha zilizovunjwa.

Hata hivyo hii si hadithi ya lawama peke yake. Tunajielekeza pia kwenye hitilafu ambazo zinatokana jiografia, hali ya hewa na historia ya Afrika; na tunaangalia kile ambacho Afrika na nchi zilizoendelea wanaweza kufanya kuondoa hitilafu hizo. Tumezingatia pia mabadiliko makubwa katika uchumi na siasa duniani katika kipindi cha miongo miwili tangu njaa kubwa ya mwaka 1984/85 nchini Ethiopia, wakati matangazo ya moja kwa moja kuhusu njaa, vifo na umasikini yaliwafikia wakazi wa dunia kupitia asilimia 98 ya wenye televisheni duniani. Picha hizo ziliifanya dunia iione Afrika kama ni mahali pa watu waliokata tamaa na tegemezi. Lakini ingawa fikra hizo bado zipo, kama kawaida zinaendelea kupitwa na wakati. Katika kipindi cha miaka 20 mambo yamebadilika kwa kiwango kikubwa katika Afrika na duniani kote.

Kwa kuanzia, Vita Baridi (kati ya mataifa makubwa) vimeisha. Huo ndio umekuwa mwisho pia wa tabia ya nchi hizo kusaidia madikteta wala rushwa waliotumia uchumi wa Afrika bila chembe ya fikra kuhusu maendeleo ya uchumi au ya watu masikini wa bara hili. Tabia ya madikteta hao iliimarisha fikra za wafadhili kwamba misaada hutumika vibaya au haisaidii kitu. Katika Afrika Kusini mfumo wa ubaguzi wa rangi umesambaratika, na kuleta matumaini mapya kwa bara zima. Mwisho wa ubaguzi wa rangi umeikumbusha Afrika na dunia kwamba hakuna udhalimu unaoweza kudumu milele. Matukio ya kusikitisha ya Septemba 11 mwaka 2001 katika miji ya New York na Washington yamefanya wengi katika nchi tajiri kutafakari kuhusu uhusiano kati ya umasikini wa dunia na usalama wa nchi zao. Kinachotokea kwa raia masikini sana katika nchi masikini sana duniani kinaweza kuathiri moja kwa moja raia tajiri sana katika nchi tajiri sana duniani. “Iwapo jamii huru haiwezi kusaidia wengi ambao ni masikini,” kama alivyowahi kusema Rais John F. Kennedy wa Marekani, “basi haiwezi kulinda wachache ambao ni tajiri.” Ukijumuisha yote haya, basi hati hii linakuwa azimio la maslahi yetu kwa pamoja – nchi tajiri na nchi masikini.

Leo hii, kuliko wakati wowote mapema, tunategemeana; siyo kwa shabaha ya riziki bali kwa usalama wetu. Kama Rais George W. Bush alivyosema, “Umasikini usioisha na ukandamizaji vinaweza kuondoa matumaini na kukatisha tamaa. Na serikali zinaposhindwa kutimiza mahitajio ya msingi ya watu wake, madola hayo yaliyoshindwa yanaweza kuwa vichaka vya ugaidi... katika mataifa mengi duniani, umasikini unafanya serikali nyingi kushindwa kuwa na madaraka kuhusu mipaka ya nchi zao, kushindwa kulinda nchi na kushindwa kusimamia utekelezaji wa sheria zao. Maendeleo ni nyenzo ya kujenga matumaini, ustawi na usalama.” Leo hii, utajiri wa watu tajiri sana katika nchi tajiri sana umefungamana na majaliwa ya watu masikini sana katika nchi masikini sana duniani ingawa wote hawajuani na hawatakutana.

Na mabadiliko hayajaisha. Mielekeo ya ruwaza za uzalishaji na utumiaji mafuta ina maana kwamba Marekani ichukue takriban asilimia 25 ya mafuta yake kutoka Afrika katika miaka 10 ijayo. Katika maoni ya kimataifa, Asia – hasa nchi kubwa za China na India – inakuja juu kama nguvu kubwa ya uchumi. Kwa mfano, vitegauchumi vya China na maslahi yake mengine kibishara, sasa vimeenea Afrika kote. Katika sehemu nyingi duniani, enzi ya tasnia kama sharti la maendeleo kwa kiasi kikubwa imerukwa kutokana na mapinduzi katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA), ambayo ukamilifu wa athari zake bado haujajulikana. Yote haya yana maana kwamba wakati umefikiwa kutafakari upya nafasi ya nchi zilizoendelea katika kusaidia Afrika kuleta maendeleo yake.

Tunajaribu kutoa maelezo katika ripoti hii. Ni maelezo changamani yasiyoepukika kwani masuala mengi yanahusiana; hili likiathiri jingine, na hayawezi kushughulikiwa kwa upekepeke bali kwa pamoja. Njia tunayofuata katika kichaka cha mwingiliano huu ni hii. Tunaanza kwa kuiambia dunia jinsi tatizo linavyoonekana kwa jicho la Mwafrika, kwani tamaduni za bara hili zimekuwa zikitupwa kando katika haraka ya kutoa na kutekeleza

ufumbuzi unaoletwa kutoka nchi zilizoendelea. Halafu tunaonyesha jinsi ambavyo Afrika inapaswa kubadilika katika maeneo ya utawala, amani na usalama na jinsi nchi zenye utajiri wa viwanda zinavyopaswa kubadili tabia zao. Tunazingatia ni kipi kinahitajika katika kusaidia watu, hasa afya zao na elimu na jinsi ya kuhakikisha kwamba watu masikini sana wanahusishwa katika maendeleo ya uchumi na jamii. Tunatoa maoni kuhusu masuala muhimu ya jinsi ya kufanya uchumi wa nchi za Afrika ukue; vilevile jinsi ya kuhakikisha kwamba watu masikini wanaweza kushiriki katika kukuza uchumi na kunufaika na ukuaji huo; watunga sera sharti wakati wote wafikirie athari za sera zao kwa watu masikini. Kisha tunajielekeza kwenye biashara, kuangalia vikwazo vinavyofanya Afrika isiuze bidhaa zaidi nchi za nje na jinsi ambavyo vikwazo hivyo vinaweza kuondolewa. Aidha, tunatafakari uhusiano kati ya Afrika na nchi tajiri katika nyanja za biashara, misaada na madeni – na jinsi wafadhili wanavyopaswa kubadili njia zao za kufanya biashara katika Afrika. Tunatoa mapendekezo maalumu katika kila moja ya nyanja hizi. Mapendekezo hayo yanatangulizwa hapa lakini yatafafanuliwa zaidi katika **Sehemu ya Pili** ya ripoti yetu. Tunahitimisha kwa kuzingatia jinsi ambavyo tunaweza kufanya mapendekezo yetu yawe ya kutekelezeka na kufuatilika na kuhakikisha kwamba yanatekelezwa ipasavyo.

## Kitu kipya kutoka Afrika

Tunaanza kwa kusema ukweli kuhusu Afrika. Hii ina maana kwamba sharti tuonyeshe penye mafanikio na kushindwa. Dalili za awali zinajitokeza kuonyesha kwamba mambo yanaanza kubadilika toka nchi moja hadi nyingine katika Afrika. Miaka 20 iliyopita lilikuwa jambo la kawaida kwa nchi za Afrika kuwa chini ya tawala za kidikteta; leo hii serikali za aina hiyo ni chache sana. Demokrasia inashamiri. Katika miaka mitano iliyopita, zaidi ya theluthi mbili za nchi kusini mwa jangwa la Sahara zimefanya uchaguzi katika mfumo wa vyama vingi vya siasa; baadhi ya chaguzi zilikuwa huru na za haki zaidi kuliko nyingine lakini kukiwa na mifano mizuri ya upokezanaji wa serikali kwa njia ya amani. Katika maeneo mengi, amani imechukua nafasi ya vita.

Pale ambako yamefanyika mabadiliko, kizazi kipya cha viongozi wa kisiasa kimeibuka na wengi wanaeleza azma yao ya kuleta maendeleo kwa watu wao. Wanaonekana wamejiweka tayari kuleta mabadiliko pia katika taasisi za Afrika. Umoja wa zamani wa Nchi Huru za Afrika (OAU) ambao ulikuwa na sera ya "kutoingiliana" katika mambo ya ndani ya nchi, sasa umebadilika na kulwa Umoja wa Afrika ambao una sera ya "kujali" raia wanaoteseka katika nchi jirani ambazo haziheshimu demokrasia, haki za binadamu na zisizothamini umuhimu wa amani. Umoja huo umeanzisha programu ya NEPAD ambayo inachukulia utawala bora kuwa kitu cha lazima kwa maendeleo ya Afrika. umeanzisha Mbinu za Uhakiki-Rika Afrika (APRM) kukaguana kutafuta kujua sera zipi na mifumo ipi ya serikali imeonekana kufanikiwa mahali pengine. Juhudi zote hizi na asasi zote zinahitaji muda kukua na kuthibitisha umuhimu wake; lakini dalili za awali zinatia moyo. Hapa ndipo msaada kutoka jumuia ya kimataifa unaweza kutumika kuleta mabadiliko.

Katika Afrika, kama ilivyo mahali pengine, kuna kiungo muhimu kati ya maendeleo kisiasa na kiuchumi. Pamoja na kudorora kwa bara hili kwa miongo mitatu, mwaka 2003 ukuaji ulivuka asilimia 5 katika nchi 24 zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara. Kuna ujasiriamali mpya na tabaka la kati vimeanza kujitokeza katika nchi nyingi. Vikundi mbalimbali vya ushinikizaji na asasi nyingi za kijamii zimeanza kubadili mazingira yanayozizunguka na zimeanza kujifunza jinsi ya kudai uwajibikaji kutoka serikalini. Kitu kingine cha kuvutia ni jukumu la Waafrika wanaoishi katika nchi zilizoendelea. Kiwango cha fedha zinazopelekwa Afrika kutoka kwa jamaa wanaoishi nje bado ni kidogo, ikilinganishwa na kanda nyingine za nchi zinazoendelea, lakini kimeongezeka ghafla katika miaka ya hivi karibuni. Kila mahali kuna dalili za awali zinazoweza kuwa msukumo kwa mabadiliko.

a Asia. Kwani Afrika palik

kote kuanza, katika miaka

Wakati jua lilipoanza kuzan

Lakini utajiri mkubwa wa Afrika uliiletea tatizo la kuendelea. Reli na barabara ambazo zilijengwa wakati wa ukoloni zililenga kusafirisha madini na malighafi nyingine kutoka sehemu za ndani za Afrika kwenda kwenye bandari tayari kwa kusafirishwa kwenda Ulaya. Hazikukusudiwa kuunganisha sehemu moja ya bara hili na sehemu nyingine au kujenga Viungo baina ya bara hili na Mashariki. Ukilinganisha ramani ya reli za Afrika na ile ya India utaona kwamba reli za India zinaunganisha sehemu mbalimbali za bara hilo dogo la Asia; zile za Afrika zinaunganisha maeneo ya uchimbaji madini na bandari. Leo hii gharama za uchukuzi za Afrika – ndani ya nchi, kati ya nchi na nchi na kimataifa – ziko mara mbili zaidi ya gharama katika nchi za Asia. Kusafirisha gari dogo kutoka Japan hadi Abijan kunagharimu dola 1,500, lakini kusafirisha gari hilohilo kutoka Abijan hadi Addis Ababa kunagharimu dola 5,000.

Kipindi cha ukoloni kilileta matatizo mengine zaidi. Ugawanyaji Afrika katika nchi za sasa ulitokana na maslahi ya nchi za Magharibi na siyo matakwa ya Waafrika. Mistari iliyochorwa kwenye ramani na mataifa makubwa ya Ulaya mjini Berlin mwaka 1884 ingali na madhara ya kina. Jumuia nyingi za kiasili zimegawanywa katika nchi mbili, tatu au hata nne. Mahali pengine makundi ambayo yanatofautiana sana, baadhi yao yakiwa maadui wa asili, yalilundikwa pamoja katika muungano wa wasiwasi; wengi wao wakiwa hawana hata lugha moja ya kuwawezesha kuongea. Ukoloni ulipendelea baadhi ya makundi na kujenga matabaka. Athari za ya baadhi ya ugawanyaji wa aina hii zingali hai leo hii, kama ilivyodhihirika katika Rwanda, ambako mahusiano kati ya Wahutu na Watutsi, ambao tofauti zao za mimbari zilikuzwa wakati wa ukoloni, yalizaa mauaji ya halaiki ya mwaka 1994.

"Acha kila mmoja awe na mlima mkubwa," ndivyo alivyonukuliwa kusema Malkia Viktoria wa Uingereza walipokuwa wanafikiria ugawanyaji wa ardhi kati ya nchi ambazo leo zinajulikana kama Kenya na Tanzania. Matokeo yake ni kwamba mataifa mengi ya sasa ya Afrika hayana mshikamano wowote wa kiasili, kijiografia, kisiasa na kiuchumi. Ukilinganisha na India ambako uliwekwa mfumo thabiti wa utawala, basi Afrika ilitelekezwa. Afrika ilitoka katika kipindi cha ukoloni ikiwa na mifumo dhaifu ya utawala na miundombinu dhaifu kuliko makoloni mengine. Mipaka ya kisiasa imekuwa vikwazo vya kiuchumi.

Huo ndio ulikuwa urithi wa Afrika. Maana yake ni kwamba ilianzia kwenye nafasi dhaifu katika mbio zake za kutafuta maendeleo. Hata hivyo, katika miaka ya 1960, miaka michache baada ya uhuru, wastani wa mapato ya Afrika ulipanda. Bali wakati matatizo ya miaka ya 1970 yalipoanza, mapato ya Mwafrika wa wastani yalipungua. Ni katika muongo huo Afrika iligeuka kuwa moja ya viwanja vya vita kwa waliokuwa wakiwakilisha migogoro ya mabwana wa Vita Baridi. Pande zote mbili za mabwana wa Vita Baridi ziliunga mkono madikteta wakubwa ambao hawakuwa na hamu ya kuendeleza uchumi wa nchi zao bali uporaji mali za nchi walizotawala na kuweka mabilioni ya dola katika akaunti zao binafsi katika mabenki yaliyoko nchini Uswisi.

Muongo huo ulizidi t kukuza matatizo ya Afrika. Wakati Asia ya Kusini ilikuwa na kazi ya kupanua mashamba yaliyoko chini ya umwagiliaji, kiwango cha ardhi ya umwagiliaji katika Afrika kilibaki kilekile. Kwa zaidi ya miaka 20 kiwango cha ardhi chini ya umwagiliaji kimebakia kwenye asilimia 4 wakati katika Asia ya Kusini kimepanda na kufikia asilimia 40. Asia iliwekeza katika barabara za vijijini na nishati, mazao mapya na sayansi na teknolojia. Hapa pia, Afrika ilibaki nyuma.

Moja ya mambo ambayo Afrika ilishindwa kufanya katika kipindi hiki ilikuwa kutoanza kupanua uchumi na kuacha kuendelea kutegemea mazao ambayo hayajasindikwa. Leo hii nchi nyingi za Afrika bado zinategemea bidhaa chache na zilezile za kuuza nje. Hii inaziacha katika hatari ya kubadilika mara nyingi, au kwa kipindi kirefu, kwa bei za bidhaa wanazouza. Kuanzia mwaka 1980 hadi 2000, bei ya sukari ilishuka kwa asilimia 77, kakao kwa asilimia 71, kahawa kwa asilimia 64 na pamba kwa asilimia 47. Bei za bidhaa za Afrika ni nyepesi kubadilika kwa karibu mara nne zaidi ya zile za bidhaa za nchi zilizoendelea.

Ulinganishi mwingine kati ya Asia na Afrika unaonyesha kuwa Afrika ina matatizo mengi. Nchi zinazoendelea zimefanya mabadiliko makubwa katika miaka 20 iliyopita. Kiwango cha bidhaa za viwandani katika soko la nje kimepanda kutoka asilimia 20 hadi 80. Asia ndiyo inaongoza. Imeendeleza miundombinu ya viwanda, stadi na utamaduni kupenda wa kujifunza, vitu ambavyo Afrika haina. Hivi sasa jukumu la kuingia katika masoko mapya ni gumu kwa Afrika kuliko ilivyokuwa huko nyuma. Mduara mwingine wa maangamizi.

Yote haya yamekuwa na athari kwa Afrika. Wawekezaji wa ndani na nje wameichukulia Afrika kuwa kitu kimoja – vita katika nchi moja siyo tu kuhusu nchi jirani bali kwa bara zima. Matokeo yake ni kwamba Afrika inaonekana kwa watu wa nje kuwa siyo mahali panapovutia ambako wanaweza kuwekeza fedha zao. Na kila senti inayopatikana Afrika inachombezwa kutoka nje.. Karibu asilimia 40 ya akiba ya Afrika inatunzwa nje ya bara hili, ikilinganishwa na asilimia 6 kwa Asia ya Mashariki na asilimia 3 kwa Asia ya Kusini. Kama fedha zilivyo ndivyo watu walivyo. Kwa miaka kadhaa, Waafrika wengi waliosoma wamekuwa wakikimbia nchi zao kwa kuwa wanakatishwa tamaa na hali ya kutoweza kutumia ujuzi wao kikamilifu. Wanaweza kupata malipo makubwa zaidi na kuishi maisha bora zaidi mahali pengine. Afrika inapoteza wastani wa wataalamu 70,000 kila mwaka wanaohamia nchi zilizoendelea katika kile kinachoitwa uhamaji wa wataalamu Zambia imepoteza madaktari 400 kati ya 1,600 iliyokuwa nao katika miaka ya karibuni.

Nguvukazi yenye afya na ujuzi ni muhimu kwa mafanikio ya kazi yoyote ya kiuchumi. Huduma ya Afya na elimu ni haki za kuzaliwa za kila mtoto lakini ni muhimu pia kwa afya ya taifa. Nchi haziwezi kuendelea iwapo wenye hadhi ya juu katika jamii ndio pekee watakaopata elimu. Ni vigumu kwa Nchi zenye afya mbaya na viwango vya chini vya elimu kupata maendeleo ya uchumi.

Hapa pia rekodi ya Afrika kuhusu maendeleo ya watu ni hafifu ikilinganishwa na Asia ya Mashariki na Kusini. Miongo ambamo Asia ilikuwa inawekeza vitegauchumi – 1970 na 1980 – ilikuwa miaka ya matatizo, wakati serikali za Afrika zikipunguza bajeti za tiba na elimu kwa kushurutishwa na Shirika la Fedha Duniani (IMF). Kuna ushahidi kwamba sera za IMF na Benki ya Dunia katika miaka ya 1980 na mapema 1990 hazikujali ni kwa kiwango gani zingeathiri watu masikini wa Afrika. Mifumo mingi ya afya na elimu ilianza kuparaganyika. Na yote haya yalikuja wakati Ukimwi umeanza kuangamiza watu wengi. Hili pia linaonyesha mduara mwingine wa maangamizi na mitego ya umasikini. Bila kuwa na kliniki na shule zinazofanya kazi, huwezi kupata nguvukazi yenye afya na ujuzi; na bila nguvukazi ya aina hiyo utakuwa umepoteza moja ya matakwa muhimu ya kujenga misingi ya kukua kwa uchumi; na bila ukuaji wa uchumi hakuna fedha za kuwekeza katika kliniki na shule.

Tatizo la Afrika ni kwamba miduara yote hii ya maangamizi imeshonana. Ndiyo maana kuikabili kunahitaji hatua kubwa katika sehemu zote na kwa wakati mmoja.

## Uhusiano kati ya Afrika na nchi zilizoendelea

Kuna mienendo mitatu ambayo mara kadhaa huwa inakinzana, ambayo inatawala mahusiano kati ya Afika na mataifa tajiri yenye viwanda. Hii inahusisha biashara, madeni na misaada. Katika miongo michache iliyopita, Afrika imeshuhudia mgawao wake katika biashara ya dunia ukishuka kutoka asilimia 6 mwaka 1980 hadi chini ya asilimia 2 mwaka 2002. Katika mtazamo huo Nchi tajiri zenye viwanda hazijatoa msaada wowote. Hakika hicho kimekuwa kikwazo cha makusudi . Umoja wa Ulaya, Japan, Marekani na nchi nyingine tajiri hutoa ruzuku kubwa kwa kilimo. Hatua hii ndiyo husababisha kushuka kwa bei za bidhaa, zitokanazo na ruzuku hizo kwenye soko la dunia. Wakulima wa Afrika hawawezi kuzalisha mazao ambayo yatakuwa na bei itakayoshindana na bei za bidhaa zilizogharimiwa kwa kodi za walipa kodi wa nchi tajiri zenye viwanda. Nchi tajiri zimelalamika katika Shirika la Biashara la Dunia (WTO) na malalamiko yao yamekubaliwa.

Lakini urekebishaji wa sera za Umoja wa Ulaya (EU) na sera ya kilimo ya Marekani, vinalegalega . Ama kwa hakika kiwango cha fedha ambacho nchi tajiri zilitumia kama ruzuku ya kilimo kwa mwaka 2002 — nyingi ya hizo zikiwa katika biashara kubwa za kilimo, ni sawa na mapato ya watu wote katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Hiyo ni zaidi ya tatizo lenyewe la biashara. Nchi tajiri hutoza kodi bidhaa zinazouzwa kwao. Kwa mfano, mazao ya kilimo yanayouzwa Ulaya sharti yalipe kodi ya wastani wa asilimia

yeyote wa bustani anavyoweza kushuhudia, hakutakuwa na kukua kama hakuna mazingira muwafaka. Katika kilimo cha bustani hii ina maana kuwa na udongo unaofaa, viwango sahihi vya hali ya hewa, maji na mwanga. Kiuchumi, kwa kuwa ukuaji kimsingi unaendeshwa na sekta binafsi, basi serikali zinahitaji kuweka mazingira ambamo watu wa kawaida – wawe wakulima wadogo au mameneja wa mashamba makubwa – wanaweza kufanya kazi zao za kila siku bila kusumbuliwa, na kutambua kwamba ni muhimu kuwekeza katika siku zijazo. Hali hiyo ndiyo inakosekana katika Afrika yote.

Kazi ya serikali ni kuweka mazingira ya uchumi ambayo yanavutia uwekezaji. Hii ina maana ya kuwepo kwa shughuli za msingi kama ulinzi, uwekaji sera bora za uchumi katika sheria za nchi, ukusanyaji wa kodi na utoaji huduma za kutosha za umma kama afya na elimu. Ina maana pia ya kuhakikisha kwamba miundombinu inajengwa – barabara, reli, maji, umeme na mawasiliano. Lakini kuna aina nyingine za miundombinu isiyoshikika, kwa mfano, mifumo ya sheria ya kulinda haki za msingi za kumiliki mali, haki za binadamu, kuheshimu mikataba, kutunza amani na kuwa mhakiki wa serikali.

Kazi hii inavuka mipaka ya shughuli za moja kwa moja za serikali na kuingia katika eneo pana la utawala. Ni kuhakikisha kwamba asasi nyingine zinaundwa, kwa mfano, mahakama huru, mfumo unaofaa na usio wa upendeleo wa majeshi ya polisi na magereza, na mifumo mingine mingi ya fedha na udhibita kwambSile benki kuu, ofisi za kusajili ardhi, na mashirika/makampuni ya kuendeshmbSituo vya forodha. Yote haya yanahitaji watumishi wa serikali wenye ujuzi na mameneja katika ngazi ya taifa na ile ya serikali za mitaa. Hawa wanahitaji kupewa mafunzo na zana za kazi kwambSile vifaa vya kutunzia /kumbukumbu, mafaili, mifumo ya hesabu, simu na kompyuta. Bila yote haya, uwezo wa serikali wa kufanya kazi zake katika dunia ya sasa utakuwa mfinyu sana.

Ni mifumo hiyo ya utawala, na uwezo wa kuifanya ifanye kazi ambavyo vinakosekana kwa kiwango kikubwa katika Afrika. Na ili kufanikisha hilo, sharta utendaji wa serikali uwe wazi kiasi kwamba unaweza kuhakikiwa. Kujua ni kiasi gani cha fedha kimepatikana na jinsi gani kinatarajiwa kutumika, kunawapa raia uwezo na haki ya kuzitaka serikali zitoe maelezo.

Suala la utawala bora na ujenzi wa uwezo ndilo tunaona ni tatizo kubwa miongoni mwa matatizo yanayoikabili Afrika. Hadi hapo hayo yatakapokuwa yametekelezwa, Afrika itaendelea kudumaa kiuchumi.

## Kwa nini iwe sasa?

Historia ndefu ya kudorora kwa Afrika inaweza kufanya baadhi ya watu kupendekeza kwamba hakuna haja ya kuchukua hatua kali za mageuzi. Hiyo siyo sahihi. Afrika haiwezi kusubiri. Mpango tunaowasilisha hapa unahitaji utekelezaji wa sasa.

Sababu dhahiri kuliko zote ya kufanya haraka ni kwamba watu katika Afrika wanakufa kila siku. Hali duni walizonazo zina maana ya kuendelea kuwa na mateso. Utu na heshima ya kawaida binadamu inasisitiza kwamba kuchelewa kuchukua hatua haliwezi kuwa chaguo letu.

Lakini kuna sababu nyingine. Bila kuchukua hatua tunakaribisha matatizo makubwa kwa siku zijazo. Kadri matatizo ya Afrika yatakavyobaki bila kutatuliwa ndivyo yatakavyoendelea kuwa magumu. Maambukizo ya ukimwi yataongezeka iwapo hayatakabiliwa. Hali kadhalika kwa magonjwa mengine ya kuambukizwa kama Tibii ambao unaenea kama mafua na ambao hivi sasa umesambaa katika bara la Afrika kwa kiwango cha mgonjwa mmoja kila baada ya nukta moja. Umasikini husababisha kuchukua huleta hatua za kujikimu kwa muda mfupi kwambSile kuuza mali za nyumbani au kukata miti, mambo ambayo yanadhoofisha misingi ya kuondokana na hali hii ambamo Afrika imezama. Kuna madhara makubwa ya baadaye, na yasiyorekebishika, yanayofanywa kwa mazingira na kutishia kuleta ukosefu wa chakuka katika siku za usoni.

Miji mikubwa iliyojaa na ya vibanda inakua haraka kila siku katika Afrika katika njia inayoashiria wasiwasi na migogoro ya kijamii katika miaka ijayo. Vurumai hizi za mjazano mijini ni mfano halisi wa gharama za kuchelewa kuchukua hatua. Idadi ya watu Afrika inakua kwa kasi. Asilimia 37 ya Waafrika hivi sasa wanaishi mijini na kiwango hicho kitaongezeka kufikia asilimia 50 katika miaka 20 ijayo. Kwa mwelekeo wa sasa, mwaka 2030 Afrika litakuwa "bara la miji." Tayari watu milioni 166 wanaishi katika miji yenye vibanda vinavyoibuka. Hali ya maisha katika maeneo haya inafanywa kuwa mbaya zaidi na ukosefu wa maji, mifumo ya majitaka, umeme, mifumo ya ukusanyaji taka na ukosefu wa huduma nyingine kutoka mamlaka za halmashauri zisizo na zana za kutosha, au zisizo tayari kukabili hali hiyo. Katika miji kama Nairobi, asilimia 60 ya watu wanaishi kwenye eneo la asilimia 5 tu ya ardhi. Na miji hii ya vibanda vya ovyo imejaa vijana, wasio na kazi na waliokata tamaa. Miji ya Afrika inakuwa bomu la chuki, hasira, mivurugano na kutoridhika.

Pamoja na matatizo haya yote, hatua za mapema zikichukuliwa zinaweza kusaidia kusimamia mikondo hii. Wakati wasichana watakapopata elimu, wakati mapato yatakapoongezeka, wakati huduma za afya ya uzazi zitakapopatikana na wakati wazazi watakapojua kwamba kiwango cha vifo vya watoto wao kinapungua, ndipo viwango vya kuzaa vitakapopungua. Yote haya yanaweza kupatikana haraka kama historia za Bangladesh na India zilivyoonyesha.

Kutochukua hatua kunaleta hatari nyingine. Wale viongozi wapya wa Afrika ambao wamedhamiria kufanya mabadiliko — wamefanya mageuzi katika uchumi na katika kukabili rushwa; —mambo ambayo yamekuwa magumu kisiasa. Viongozi hao wanaweza kuondolewa madarakani iwapo wananchi hawataona matunda ya kazi hizo. Hii inaweza kuwa na maana kwamba baadhi ya mabadiliko yaliyonuiwa kuboresha maisha katika Afrika katika kipindi cha muda wa kati na muda mrefu, yanaweza kuvurugwa na hali kurejea ilikokuwa. Viongozi wengine wanaofuata wanaweza kuzuiwa kufanya mambo hayo. Ndiyo maana msaada kutoka nchi zilizoendelea ni suala la haraka ili kutekeleza mabadiliko haya.

Leo hii Afrika ina fursa bora zaidi ya kufanya mabadiliko kuliko ilivyokuwa kwa miongo yote. Lakini hali ya baadaye imo katika imani nzuri. Nchi tajiri sasa zina nafasi ya kuamua kuwa mizani ielekee kwenye uwezekano wa mafanikio na siyo uwezekano wa kushindwa. Hatari za kuchelewa ni kubwa mno kuliko zile za kuchukua hatua thabiti na za haraka.

## Katika Mtazamo wa Kiafrika

Uliza swali kubwa: "Maendeleo ni nini? Utapata majibu tofauti katika tamaduni tofauti. Wengi katika nchi za Magharibi huona maendeleo kuwa ni sehemu kama Afrika kuwa na viwango vya maisha kama nchi zilizoendelea. Katika Afrika unaweza kuambiwa kwamba maendeleo ni kuwa na ustawi wa maisha, furaha na ushirikiano katika jamii. Katika nchi za Magharibi, maendeleo ni kuwa na utashi wa kuchagua utakacho; katika Afrika ni kuongeza heshima ya mtu katika jamii. Wale wanaotaka kuleta maendeleo katika Afrika sharti waingize maana hii katika sera zao, vinginevyo watashindwa.

Tatizo ni kwamba katika mjadala kuhusu maendeleo, ingawa sote tunatumia maneno yaleyale, mara nyingi hatumaanishi kitu kilekile. Tamaduni mbalimbali hubaini mawazo yao ya uhuru wa kisiasa na kiuchumi katika njia tofautitofauti. Kwa sababu hiyo Tume iliamua kufikiria kwanza suala la utamaduni kabla ya kugusa uchambuzi wa kisiasa na kiuchumi.

Tunapozungumzia utamaduni tunakwenda mbali zaidi ya fasihi, muziki, dansi, sanaa, uchongaji, uigizaji, filamu na michezo. Kwa kundi lolote la kijamii, yote haya ni sehemu ya furaha ya pamoja ya watu hai. Lakini utamaduni ni zaidi ya sanaa. Ni kuhusu ruwaza za pamoja za utambulishi. Ni jinsi maadili ya jamii yanavyowasilishwa katika jamii husika na jinsi mtu mmojammoja anavyokuwa sehemu ya jamii. Utamaduni ni jinsi yaliyopita yanavyoingiliana na yajayo.

Afrika kabla ya kuja kwa wakoloni ilikuwa ya watu waliojumuika katika koo. Tamaduni zao zilikuwa na nguvu. Zilijengwa kwenye udugu na dhana kwamba kila mmoja katika ukoo aliwajibika kwa mwenzake. Tabia nyingi za aina hii, kwa mfano uhusiano kati ya wakubwa na wadogo, bado zipo hadi leo. Ndio maana utamaduni wa "mzee" ambao huhitajia mtu mkubwa, mwenye uwezo katika ukoo, kuwa kiongozi wa wana-ukoo wengine – jambo ambalo huwa halitiliwi maanani na waandaaji wa sera za maendeleo. Uhusiano kati ya mlezi na mlelewa usitupiwe mbali na kuchukuliwa kuwa kiini cha vishawishi vya upendeleo na rushwa; kwa hakika uhusiano huo ndio unadhihirisha dhana ya Kiafrika ya jamii..

Kwa maana hii, utamaduni siyo kitu cha nyongeza tu. Sharti ujengwe kwenye uelewa wetu, uchambuzi wetu na katika hatua zote. Hii ndiyo sababu mojawapo tangu mwanzo tulisisitiza kwamba Tume ya Afrika sharti ifanye ushauriano kwa mapana, katika Afrika na katika nchi zilizoendelea. Kama mmoja wa Makamishna kutoka Afrika Kusini, Trevor Manuel, Waziri wa Fedha, alivyosema akikariri methali ya Kiafrika, "Hadi hapo simba watakapotoa kauli yao, historia pekee itaendelea kuwa ya wawindaji." Mashauriano tuliyofanya yalishirikisha watu wanaoishi katika miji ya vibanda, mijini katika Afrika Mashariki, wanawake wa vijijini kutoka Afrika Magharibi na wafanya maamuzi wa ngazi za juu waliochaguliwa na wasiochaguliwa katika Afrika na nchi tajiri duniani. Wote tuliwauliza swali lilelile: Kipi kinawezekana katika Afrika na kipi hakiwezekani?

Mara nyingi mambo mawili yalisisitizwa: Kwanza, haja ya kutambua uanuwai wa Afrika. Likiwa bara la pili duniani kwa ukubwa, Afrika ina zaidi ya nchi 50 ambamo kuna mchanganyiko wa utajiri mkubwa wa watu, tamaduni, uchumi, historia na jiografia. Afrika ni bara lenye sehemu nyingi, kama msemo wa Kifaransa unavyosema – "les Afriques" – Afrika nyingi. Hii ina maana kwamba hapawezi kuwa suluhisho moja kwa matatizo yote na kwa sehemu zote za Afrika.

Ujumbe wa pili ulikuwa kwamba nguvu ya Afrika imo katika mifumo yake ya kijamii ambayo haionekani kwa watu wa nje. Kinachoonekana kwa wafadhili kuwa hali ya utawala huria hakika ni mfumo makini. Hii ni mifumo ambayo watu wa Magharibi hawakufunzwa kutambua. Waafrika wanaendelea kuishi – na wengine kufanikiwa – wakati wana mapato kidogo na kazi chache katika uchumi rasmi. Wanafanya hivyo kwa kutumia mfumo changamani wa mahusiano ya kijamii ambayo hufanya maamuzi kuhusu nani, katika mazingira ya dharura, apate mtaji wa kuanzia biashara ndogo au apate mkopo usio na riba. Mifumo hii yaweza isiwe rasmi lakini inaonyesha jinsi watu wa Afrika wanavyoweza kushiriki katika shughuli ambazo wanaona zina shabaha na mwelekeo.

Kingine kilicho wazi ni kwamba, katika sehemu nyingi, mifumo kama hiyo inachukuliwa kuwa mbadala wa dola. Huu ni ukweli ulio wazi katika sehemu kama Somalia ambako dola ilikwishaanguka. Lakini kote Afrika kuna "dola zilizoshindwa," kwa maana kwamba yameshindwa kuweka mifumo ya msingi ya kisheria na kiuchumi, au kutoa huduma za jamii kama afya na elimu ambazo wananchi wangetegemea kupata. Kuna kutoamini na kubeua wanasiasa. Katika lugha ya Wolof, neno *politig* limepata maana ya uwongo. Wapiga kura wameishiwa imani. Idadi ya watu wanaokwenda kwenye vituo vya kupigia kura imeshuka Afrika kote.

Kwa walio wengi, dola ni kitu kisicho muhimu au mzigo. Kwao, uaminifu na uwajibikaji bado uko kwenye familia, ukoo au kabila. Hata hivyo, kitu kipya kinaingia pale penye ombe. Ni dini. Dini imekuwa muhimu katika Afrika, bali hivi sasa wengi wanajiunga na madhehebu ya Kikristo hasa ya Kilokole. Wengine wanajiunga na madhehebu ya Kiislam hasa yale ya nadharia ya Wahhabi ya utakaso, wakichochewa na fedha kutoka Saudi Arabia. Aidha, kuna uamshaji mkubwa wa dini za asili za Afrika zikiwa ni pamoja na vikundi vya siri vya ufundaji. Pale ambako dola haliwezi kutimiza matakwa ya jamii, madhehebu ya dini

kupelekwa katika sehemu mbalimbali za nchi hiyo kwani makanisa ndio miundombinu pekee iliyoshikamana kitaifa. Katika Senegal, madhehebu ya Mouride Brotherhood yamepanuka na kuhudumia karibu theluthi mbili ya idadi ya watu nchini humo; miongoni mwao yakiwa na kikundi cha Kiislamu cha Sufi, makundi ya wenye shauku ya biashara na waumini wake wengine wanaoishi nje ambao huleta nyumbani viwango vikubwa vya fedha. Dini, hasa madhehebu ya Kiislam na Kikristo, ndiyo ufunguo wa utandawazi. Saudi Arabia na nchi za Ghuba zimekuwa sehemu ya kipua cha Biashara cha Afrika na kanda za mapokezi ya wafanyakazi wa Afrika wanaokwenda kufanya kazi katika nchi hizo. Aidha, madhehebu mengi ya Kilokole yana uhusiano na makanisa makubwa katika Marekani.

Hii ina angalau athari mbili kwa maendeleo katika Afrika. Dini inaweza kuwa mfano wa dola. Kama dola ya Kiafrika inataka kuwa yenye nguvu na yenye kutoa matunda yanayotarajiwa, inahitaji kuelewa ni kitu gani kinachofanya dini ijenge uaminifu na miundombinu, ilete fikra kwamba inaweza kutoa matunda ya kiroho na ya kidunia. Bila shaka dini inaweza kutumiwa vibaya, lakini inaweza pia kuwa mshiriki katika maendeleo. Viongozi wa dini wana athari kubwa kwenye tabia na mwelekeo wa jamii, mahusiano ya kijamii, uwajibikaji wa mtu binafsi na uadilifu katika mahusiano kimwili. Hivi karibuni serikali ya Ethiopia ilipata maamuzi kutoka kwa Mkuu wa Kanisa la Orthodox la nchi hiyo, ambayo yanatoa ruhusa kwa wakulima kufanya kazi kwa siku 160 za mwaka. Awali ilichukuliwa na waumini wa kanisa hilo kwamba hizo zilikuwa ni siku za sherehe za kidini na kufanya kazi katika siku hizo ingekuwa dhambi. Tangu hapo uzalishaji katika kilimo umepanda kwa zaidi ya asilimia 20 kwa mwaka. Katika Kenya wafanyakazi katika taaluma ya tiba tayari wanatumia waganga wa asili kueneza elimu ya UKIMWI afya ya msingi. Wachungaji na mapadri, viongozi wa dini na maimamu wanashiriki kikamilifu katika kupambana na ukimwi. Lakini hii isichukuliwe kwamba ni jaribio la kuwashirikisha viongozi wa dini na waganga wa asili kusambaza ujumbe wa tamaduni za nje. Jumuia ya kimataifa itahitaji kutumia njia tofauti kuweza kutambua nafasi ya dini katika maisha ya Mwafrika.

Hoja iliyozagaa kuhusu utamaduni, na ambayo si ya kweli, ni kwamba ni kielelezo cha uasili usiobadilika. Wale wenye mawazo haya mara nyingi huona utamaduni wa Afrika kuwa ni wa kurudi nyuma, wa kikabila na kwa hiyo unadhuru maendeleo. Mara nyingi wanasema kwamba utamaduni wa Afrika ni nguvu isiyowiana ambayo inarudisha nyuma maendeleo ya kiuchumi. Hii ni kinyume cha ushahidi uliopo. Historia inaonyesha kwamba tamaduni za Afrika zimekuwa nyepesi kupindukia katika kupokea mambo mapya, zikichukua athari nyingi kutoka nje, shuruti nyingi, na bado zikaweza kutafuta njia za kukabiliana na hali ngumu ya maisha kimazingira na kijamii. Siyo yote yalichukuliwa ambayo ni mazuri. Aidha, tamaduni nyingi za Afrika bado zinalea tabia ya ubaridi, au zinachochea udhalilishaji wa wanawake, au hutoa heshima kwa wakubwa kwa kiwango kikubwa kiasi kwamba zinawasahau vijana, ambao hivi sasa ndio nusu ya watu wote wa Afrika. Lakini mwenendo wa utamaduni unaelekeza kwamba watu wanaweza kuhakiki na kukosoa yale ambayo wamerithi. Funzo ni kwamba utamaduni ni kichocheo cha mabadiliko ya kiuchumi na kijamii. Kwa hakika jinsi simu za mkononi zinavyobadili maisha katika Afrika ni mfumo dhahiri. Matumizi ya simu za mkononi yanaongezeka kwa kasi zaidi kuliko sehemu yoyote nyingine duniani. Asilimia 75 ya simu zote katika Afrika ni zile za mkononi. Kichocheo kikubwa cha matumizi ya simu hizi kimekuwa haja ya kuwa na taarifa za kifamilia, lakini simu hizi pia zinatumiwa kusaidia watu masikini katika sehemu za mbali kutoka mijini, kutafuta kazi bila kulazimika kwenda mwendo mrefu. Bali teknolojia mpya inaleta pia faida nyingine zisizo wazi moja kwa moja.

Kwa mfano katika jamii za wafugaji katika Tanzania, ambako mabucha hayawezi kuweka nyama nyingi kutokana na kutokuwa na umeme au kutomudu kununua friji, mara nyingi nyama ilikuwa inaisha mapema kwa kuwa iliwekwa kidogo. Siku hizi wateja wanatumia simu za mkononi kuagiza kiasi cha nyama wanachotaka kabla ya siku ya kwenda kuichukua. Hii inawezesha wenye mabucha kununua kiasi cha nyama kinachohitajika

kukidhi mahitaji ya wateja wao na hivyo kujenga mfumo thabiti wa ugavi. Watoa huduma za simu kwa watumiaji wa pikipiki sasa wameanza uunganishaji wa simu hizo katika sehemu za vijijini nchini Afrika Kusini. Tayari ushahidi umeanza kuonekana kwamba ukusanyaji wa data kwa njia ya simu za mkononi una uwezekano wa kuongeza ufanisi katika bajeti za afya, kama ilivyodhihirika nchini Uganda ambako mipango ya majaribio imeonyesha kuokoa asilimia 40 ya matumizi.

Bara la Afrika liko mbele zaidi ya nchi nyingi duniani katika matumizi ya kadi za simu za kulipia kwanza. Waafrika katika nchi zilizoendelea wananunua kadi hizi na kuwapelekea jamaa zao Afrika kwa kutuma namba za kadi kwa njia ya simu za mkononi. Wapokeaji wanaweza pia kuuza kadi hizo (namba) kwa wengine. Kwa njia hii, kadi zimekuwa njia ambamo fedha zinaweza kupitia kutoka nchi zilizoendelea kwenda Afrika bila kulipia huduma kama inavyokuwa kwenye njia za kawaida za kusafirisha fedha.

Simu ya mkononi ni miundombinu isio bayana na inakuza uwezekano wa mabadiliko ambayo hayakufikiriwa katika utamaduni, miundombinu na siasa za Afrika. Utafiti umeonyesha kwamba kama asilimia 20 ya watu wote katika nchi ina uwezo wa kubadilishana habari na mawazo kwa njia ya simu ya mkononi – kuongea na kuandikiana ujumbe – huwa vigumu kwa tawala za kidikteta kuendelea kushika madaraka. Mabadiliko ya aina hii yanapasa kutupa tahadhari kuhusu uwezekano wa maendeleo mengine ambayo ni vigumu kuyaona kwa sasa na ambayo yanaweza kudhoofisha baadhi ya dhana za awali katika fikra zetu kuhusu maendeleo. Ripoti kama hii sharti iache nafasi ya kutegemea kisichotegemewa.

Wale wasiojali utamaduni wana uwezekano mkubwa wa kushindwa katika Afrika. Hili ndilo somo walilopata watu kutoka nje ambao waliendesha warsha kuhusu UKIMWI nchini Angola. Walikuja kutoa elimu juu ueneaji na uzuiaji. Waliondoka wakiwa wamepata uelewa mpya wa desturi kama kufunda, kupiga chale, udugu wa kuchanjiana, jinsi ya kukata kitovu cha mtoto, ndoa za wake wengi, ndoa za kimila na tiba za asili. Hapo ndipo walielewa kwa nini elimu na mipango yao ya kuchochea ufahamu haikufanikiwa kushawishi watu wengi kutumia kondomu au kupunguza kiwango cha ueneaji wa VVU. Hawakujua vya kutosha kanuni za kitamaduni na thamani inayowekwa katika ngono.

Wale wanaojua utamaduni wanaweza kutafuta njia mpya za kufanikiwa. Kabla ya vita vya wenyewe kwa wenyewe kuweka Somalia katika vurugu ya utawala wa mabwana-vita, utulivu ulikuwa unasimamiwa na mahakama za jadi za wazee zilizoitwa Tol. Mahakama hizi zilifanya kila ukoo kuwajibika kwa makosa ya kila mwanaukoo – mtu mmoja akiiba, ukoo mzima unatozwa faini. Katika sehemu nyingi za nchi hii uwezo wa Tol umefutwa na malodi wa vita. Lakini katika Somaliland, mahali pa ustawi, wa wastani mfumo wa Tol siyo tu kwamba umeendelezwa, bali umeingizwa katika utaratibu wa bunge. Wengi wanaamini kwamba kuendelezwa kwa mfumo huo wa zamani ni moja ya mambo muhimu yanayochangia uimara wa Somaliland. Siyo rahisi kwa mwana-nadharia za kisiasa kubuni mfumo chotara kama huu. Lakini kwa mchanganyiko wa mifumo ya utawala ya Kiafrika na ile ya nchi za Magharibi, huu ndio mfumo uliothibitika kwamba unafaa. Changamoto ni kutumia tamaduni za Afrika kutafuta mifumo chotara mingine inayoweza kutumika katika bara hili.

Somo la jumla tunalopata ni kwamba maelekezo kutoka nje hufanikiwa pale tu yanapokuwa yamechanganywa na njia na taratibu za utendaji za Afrika. Maelekezo hayo hushindwa pale ambapo yanadharau, au kushindwa kuelewa, matarajio ya wale wanaotaka kusaidiwa. Jumuia ya kimataifa sharti ifanye juhudi kuelewa thamani, kanuni na wajibu wa tamaduni za Afrika, na katika uandaaji wa sera zao, waonyeshe unyumbufu, uwazi na unyenyekevu.

## Urekebishaji wa Mifumo: Utawala na Ujenzi wa Uwezo

Msingi mkuu wa maendeleo ni dola ililo na katiba thabiti inayoweka urari katika maslahi ya raia wake wote na ambayo inatenganisha madaraka ya mahakama, bunge na serikali. Hii ndiyo huleta mfumo ambamo sekta binafsi inaweza kujenga ukuaji wa uchumi ambao, kama haukupatikana, basi maisha ya watu masikini hayawezi kuboreshwa. Hii ina maana ya dola ambayo ina uwezo wa kulinda amani na usalama na kulinda uhuru na haki za binadamu za raia wake, kutunga sera ambazo zitawezesha watu wa kawaida kujenga maisha bora, na dola kuweza kutoa huduma za umma zinazohitajika kwa raia wake.

Utawala siyo tu jinsi serikali inavyofanya kazi zake. Ni uwanja mzima ambamo dola inafanya kazi, ikiwa ni pamoja na maeneo kama bunge, mahakama, vyombo vya habari na taasisi za jamii ambazo hubaki bila kutetereka pale serikali inapobadilika. Linalofuata ni kuhusu sera za serikali. Lakini pia ni kuhusu iwapo serikali ina watumishi na mifumo na taratibu za kuweza kutunga sera zake, na uwezo wa kuzitekeleza kwa ushirikiano wa raia wake.

Kuna kipimo kingine cha dola; hiki ni jinsi gani serikali inavyowajibika kwa watu wake sera na vitendo. Aina fulani ya demokrasia ni muhimu sana hapa. Lakini hii ni zaidi ya uchaguzi unaokuja kila baada ya miaka mitano ili kubadilisha viongozi. Waafrika wengi hawaoni uhalali wa katiba za nchi zao, ambamo mizania ya serikali, bunge na mahakama mara baada ya uhuru, ilitupwa katika kapu moja la serikali na kusababisha kuwapo mfumo wa chama kimoja katika miaka iliyofuata. Viongozi wengine hupuuza katiba na kubaki kwenye madaraka kwa vipindi virefu zaidi ya inavyoruhusiwa kikatiba. Waafrika wanapaswa kushughulikia masuala haya na nchi zilizoendelea hazina budi kutoa misaada ya kiufundi na kifedha.

Ingawa hili halifurahishi, bali kwa uwajibikaji kuleta mafao yanayotarajiwa, sharti sera, matendo na mifumo ya serikali viwe wazi kwa uhakiki. Uwazi huu siyo suala la tabia; sharti uwazi uwe sehemu ya mifumo ambamo dola inafanya kazi zake.

Kwa bahati njema kuna uelewa wa yote haya miongoni mwa serikali za Afrika. Hivi sasa wanafanya kazi kwa karibu zaidi kukabili hili kupitia UA. Nchi zipatazo 24, zikiwakilisha asilimia 75 ya watu wote wa Afrika, tayari zimetia saini makubaliano yatokanayo na mpango wa NEPAD ya kuanzisha APRM kusaidia kugundua udhaifu na kupendekeza hatua za kuuondoa. Shabaha ni kuhakikisha kuwepo kwa sera nzuri na utekelezaji kwa kupeana taarifa kuhusu lipi linawezekana na lipi haliwezekani. Shinikizo kutoka kwa waliomo katika kundi moja ni motisha kubwa kwa utendaji. Utaratibu huu umo katika hatua za mwanzo lakini hatua zilizokwishachukuliwa zinatia moyo na Tume inapendekeza kuwa nchi tajiri ziuunge mkono. Kwa kiwango kidogo cha fedha, utaratibu huu wa APRM waweza kuleta mabadiliko muhimu. Maelezo zaidi kuhusu hili, kama ilivyo kwa mapendekezo yetu yote, yamewekwa katika Sehemu ya Pili ya ripoti hii.

### Uwezo wa kufanikisha

Utawala bora ni zaidi ya kuwa na sera nzuri. Serikali zinapaswa kuwa na uwezo wa kuweka sera hizo katika vitendo. Mambo kadhaa ya kiutendaji hukwamisha uwezo wa dola za Afrika kufanya hivyo. Afrika haijawa na fedha za kuwekeza katika mifumo ya teknolojia, afya na elimu, barabara, umeme, mawasiliano ya simu, makazi, maji na majitaka. Haina mifumo bora ya kukusanya data ambazo kama hazikupatikana, sera za serikali haziwezi kuandaliwa vizuri wala kufuatiliwa kwa usahihi. Mara nyingi watumishi wake, katika serikali kuu na serikali za mitaa, hawana ujuzi/ wa kuchambua taarifa changamani au kupanga na kuandaa bajeti. Mifumo ya menejimenti na vishawishi vya kazi imekuwa ya hali ya chini mno. Watumishi wa serikali wanaswagwa na wimbi la ukimwi. Nchini Zambia walimu wanakufa haraka kuliko wanavyoweza kuandaliwa.

Katika miaka ya hivi karibuni, wafadhili wa kimataifa wamejaribu kuwekeza katika kujenga uwezo wa kuandaa na kutoa huduma. Lakini matokeo yake yamekuwa ya hapa na pale.

Tumeangalia sababu za hali hii. Mageuzi yamekuwa ya kidogokidogo badala ya kuwa sehemu ya mkakati mpana. Serikali za Afrika hazijajizatiti katika mageuzi hayo na wafadhili walitoa misaada kwa njia ambayo haikuwa yenye kuleta manufaa. Badala ya kuongeza uwezo wa wizara za serikali za Afrika, wafadhili waliunda vitengo vya kutekeleza mradi mmojammoja. Inawezekana utaratibu huu ukafaa kwa muda mfupi, lakini kwa muda mrefu, kupata watu wa nje kuja kufanya kazi ulizoombea msaada, hakusaidii kuboresha ujuzi wa watumishi wa serikali.

Hapa panahitaji mtazamo tofauti kabisa. Hivi sasa nchi nyingi za Afrika ndizo zinaunga mkono kikamilifu mpango wa NEPAD ambao unaweka mkazo kwenye kuimarisha asasi. Mahali pa kuanzia sharti pawe serikali za Afrika kuandaa mikakati mipana ya kujenga uwezo katika tawala zake. Jumuia ya kimataifa haina budi kuunga mkono mikakati hii na kuhakikisha kwamba juhudi za wafadhili mmojammoja hazidhoofishi mikakati hii. Uwezo huu hauna budi kujengwa katika wizara na katika ngazi ya serikali za mitaa. Lakini pia unahitajika kwenye ngazi ya bara katika UA na katika mashirika ya kikanda ya kiuchumi ambamo nchi za Afrika hufanya kazi pamoja.

Kubadilisha urasimu halitakuwa suala la usiku mmoja. Wafadhili hawana budi kutambua kwamba katika nchi nyingi za Afrika mabadiliko yatachukua muda mrefu, yatakwenda polepole na yatakuwa na utata. Hii ina maana kwamba nchi tajiri hazina budi kutoa misaada katika njia ambayo itaruhusu serikali za Afrika kuwa na mipango ya muda mrefu kuliko ilivyo sasa. Bila mipango ya muda mrefu ya kuonyesha jinsi fedha zitakavyoingia kwa ajili ya kulipa mishahara na kukarabati miundombinu, serikali zitasita kujenga shule au kuajiri walimu. Aidha, wafadhili sharti wajiepushe na udokozi wa watumishi wa serikali ambao wana vipaji vya juu na hivyo kudhoofisha zaidi mifumo. Serikali za Afrika nazo zishughulikie suala la udhaifu katika menejimenti, ukosefu wa vishawishi vya kufanya mambo kwa taratibu zinazostahili na kwa ubora zaidi. Muhimu pia ni haja ya kuvutia, kumotisha na kuendelea kuhifadhi watumishi wenye ujuzi. Utafiti umeonyesha kwamba nchini Malawi, asilimia 25 ya walimu walioanza kazi katika sehemu za vijijini Januari 1999 walikuwa wameacha kazi ilipofika Oktoba mwaka huo.

Upungufu wa wafanyakazi wenye ujuzi katika Afrika ni tatizo kubwa. Hili linatokana na mfumo wa elimu ya juu kuwa imo katika mgogoro. Mkazo mkubwa katika Afrika katika miaka ya karibuni umekuwa kwenye elimu ya msingi. Athari za utaratibu huo zimekuwa kutotilia maanani elimu ya sekondari na elimu ya juu ambako tunapata madaktari, wauguzi, walimu, maofisa wa polisi, wanasheria na wafanyakazi wa serikali kwa siku zijazo. Vyuo vikuu vya Afrika sharti viwe mahali pa kuandalia watu binafsi wenye ujuzi ambao bara hili linahitaji zaidi. Kuna upungufu mkubwa wa ujuzi wa mambo ya sayansi ambayo inahitajika kwa ajili ya kukabili matatizo ya Afrika. Afrika inahitaji asasi za viwango vya juu vya elimu na utafiti ambazo zitavutia wanafunzi, watafiti na walimu kutaka kujifunzia na kufanya kazi Afrika. Hivi sasa kuna wanasayansi Waafrika na wahandisi wanaofanya kazi nchini Marekani kuliko katika Afrika. Unahitajika mpango wa muda mrefu wa uwekezaji ili kuvipa nguvu vyuo vikuu vya Afrika na kusaidia maendeleo ya asasi zinazofanya vizuri katika maeneo ya sayansi, uhandisi na teknolojia, ikiwa ni pamoja na taasisi za teknolojia za Afrika.

### Uwajibikaji kwa wananchi

Kuna sharti jingine muhimu linalohitajika kwa ajili ya utawala bora. Hili ni uwajibikaji ambao una maana ya mfumo ambao unahakikisha kwamba serikali zinawajibika kwa watu wake kwa namna zinavyoendesha nchi. Mara nyingi katika miaka iliyopita, serikali za Afrika hazikuwajibika kwa watu wake wote bali kwa wale wenye nafasi katika jamii, vyama vya siasa, makabila au makundi mengine. Mara kadhaa wameweka mbele matakwa ya wafadhili wa kimataifa kuliko yale ya raia wao.

Serikali hazina budi kuwajibika kwa watu wake wote ikiwa pamoja na wale walio masikini sana na wanaoishi katika mazingira magumu na yasiyo salama. Hivi sasa serikali hazionekani kufanya hivyo. Shirika la *Globescan* lililoajiriwa na Tume hii, limeonyesha kwamba, kwa Waafrika wengi, wanaona serikali za nchi zao ndizo kiini cha matatizo: asilimia 49 ya wale waliohojiwa walilaumu wanasiasa wao; hii ikiwa mara tatu zaidi ya waliolaumu wakoloni (asilimia 16) au nchi tajiri ambao walikuwa asilimia 11.

Nnchi zlizoendeleaaazinwezyapmiakuszaidai -imarlisaisektja yiengneimuhimui ambvyai na

v ya wkuilik,iiikunidiivaabzashmrk,iivama v ya wufanykhaz,o maShirikayaaaaendeleo,:

v yma v yaaikiaaaaik,isass izyakaidnie naiikunidiiiengneiv yakijamiia–iivyoteizin jukaum:

Ruiswmo nauwhaz: mikunidimwengo yakijamiiaywanki tkka.Idaidi yisass ihiziizyakijamiialimpa dai katikamuongo:

Ildiviongozkiiwa siasa w4azyakuwtajbliswm, shmrtdiramia w4ao natasrifai kmsilakuhusui

vishivyaminrik,imigonganzoyaaaasInhi yyabzinfs i auukosefu9wkauaminrfu9 katikamhtumizi:ynafedhmizyaummka.Hapyap

mpkaoi ya serikaliiaaaafungu yyabajetla.Uwhazihkufanyaiona wnei kwambikuna:

wnachamsa wasass izyashir,i ambizo iizyaka aidai katikaAafrik,iklamojldvvyakkatika nch:azlizoendeleaa.Ukosefu9huu9w

iina hughuilkjwmokkatika jina ambvyai nufanya esabui zsifahamikei kwaummkaa

mangamiizyakaAafikRuiswmokiaaakdyakuhabujhudzyakaboreshutawlajkina

masikini sana, kwa kuwa yanachepua fedha kutoka kwenye utoaji wa huduma muhimu ambazo wanahitaji kuliko mtu yeyote katika jamii, na wana uwezekano wa kutumia asilimia kubwa ya mapato yao kwa ajili ya hongo. Afrika imeanza kukabili hili. Wanasiasa wake wamekubali, kupitia APGM kukadiria utendaji wao kwa kulinganisha na kanuni na viwango vya kimataifa vilivyokubaliwa, ikiwa ni pamoja na uwazi katika mipango ya matumizi na fedha zenyewe. Aidha, watahitaji kutumia viwango hivi kwa kuzingatia mazingira ya Afrika, kwani vingi vimeandaliwa kwa ajili ya nchi ambazo tayari zimeendelea sana kuliko Afrika na ambazo zina uwezo tofauti na zinakabiliwa na changamoto tofauti za kiuchumi.

Uoza wa rushwa umeenea katika jamii nzima na kwa ngazi zote. Lakini, ili kutoa hadhari kwa shabaha ya yenye nguvu, inafaa kukabili rushwa ambayo ni ya kiwango kibaya sana. Jumuia ya kimataifa inaweza kusaidia kwa njia mbili: Kwanza, haina budi kufuatilia fedha zilizoibwa na viongozi wa Afrika wala rushwa, ambazo hivi sasa ziko katika mabenki ya nje na kuzirudisha katika nchi ambako ziliibwa. Hili litapeleka ujumbe wa wazi kwa viongozi wa sasa na wale wa siku zijazo kwamba hawataruhusiwa kujiineemesha kutokana na ufisadi. Pili, nchi tajiri sharti ziweke hatua mbalimbali za kufanya wizi wa mali ya umma kuwa jambo gumu na kwa kuanzia, kuzuia makampuni yao kutoa hongo. Hata hivyo, kama dikteta Mobutu Sese Seko wa Zaire alivyosema, "Rushwa ni tendo la pande mbili – mtoaji na mpokeaji."

Tunajadili viwango vikubwa vya fedha hapa. Inakadiriwa kwamba kiasi kilichoibwa na hivi sasa kinashikiliwa katika mabenki ya nje, kinazidi nusu ya deni la nje la bara zima la Afrika. Baya zaidi, kiasi ambacho watu binafsi wanashikilia katika akaunti za benki za nje ni mabilioni ya dola za Marekani. Nchi zilizoendelea zinapaswa kuzitaka benki zilizomo katika uwezo wake kisheria, kutoa taarifa kuhusu akaunti hizo na kurudisha fedha hizo kwa mamlaka husika. Hatua zinahitajika katika maeneo matano yanayoingiliana:

**Kuzuia:** Kwanza zinahitajika hatua za kuzuia wizi wa mali. Sharti sheria za Afrika zifanye hilo kuwa kosa. Taasisi za fedha za kila nchi sharti ziwe na mifumo ya kukabiliana na fedha isiyo katika mzunguko halali.

**Utambuaji:** Sharti mifumo iboreshwe ili kuweza kutambua kwamba lini fedha katika akaunti husika imepatikana kwa njia isiyo halali. Nchi tajiri zimejenga vikwazo vya kukabiliana na fedha isiyo ndani ya mzunguko halali katika vita vyao dhidi ya ugaidi na madawa ya kulevya. Njia hiyo yaweza kutumika hapa. Benki hazina budi kutaarifu nchi za Afrika pale zitakapoona biashara za kutilia mashaka.

**Ushikiliaji mali/fedha:** Sharti sheria zifanyiwe marekebisho kufanya iwe rahisi kushikilia mali katika hatua ya mapema zaidi kwenye upelelezi wa jinai, na ili kuzuia fedha kuhamishwa wakati upelelezi unaendelea.

**Uchukuaji mali:** Iwekwe mifumo itakayowezesha kuchukuliwa kwa mali iliyoibwa bila sharti la kupata hukumu katika kesi ya jinai. Serikali zote za nchi zilizoendelea hazina budi kuanzisha sheria za kuwezesha kuchukua mali bila sharti la hukumu kwanza katika shauri la jinai, na kutafuta njia za kupunguza idadi ya rufaa ambazo zinapoteza muda.

**Urejeshaji mali:** Mataifa ambako kuna benki zinazotunza fedha zilizoporwa, hayana budi kuweka utaratibu wa kisheria wa kurudisha fedha hizo kwa taifa ambako ziliporwa.

Mataifa tajiri hayana budi kutoa msaada wa kiufundi kukuza uwezo wa Afrika katika maeneo haya.

Lakini rushwa inavuka matendo ya viongozi wachache mafisadi. Ipo katika kila ngazi. Kinachowasumbua watu masikini ni rushwa ndogo. Kwa ngazi ya chini kabisa, hilo ni suala la serikali za Afrika kudhihirisha utashi wa kisiasa wa kukabili rushwa. Lakini pia kuna mengi ambayo jumuiya ya kimataifa inaweza kufanya. Sharti juhudi zielekezwe kwa mtoa hongo na mpokea hongo. Makubaliano mengi mno ya kimataifa kuhusu kuzuia hongo tayari yapo kwa ajili ya kukabili rushwa. Hayana budi kutekelezwa kwa dhati. Makubaliano ya Umoja

wa Mataifa dhidi ya Rushwa (UNCAC) – sheria ya kwanza ya kimataifa kutambua haja ya mataifa yote kukubaliana kuhusu urejeshaji wa mali – hayajaridhiwa na mjumbe hata mmoja wa kundi la nchi tajiri zenye viwanda, G8. Mapatano haya yanaweza kuanza kutumika pale tu yatakapokuwa yameridhiwa na mataifa 30. Haina maana kwa nchi zilizoendelea kusikitikia rushwa katika Afrika wakati zenyewe hazichukui hatua maalumu zinazohitajika kuikabili.

Uwazi ni muhimu hasa katika nchi ambazo zina utajiri wa madini. Ushahidi wote unaonyesha kwamba mafuta, kwa mfano, hutajirisha tabaka la watawala. Kwa sehemu kubwa ya wananchi, utajiri wa madini mara nyingi huonekana tu kuongeza rushwa, umasikini na kuyumba kisiasa. Wapiga kura wa Afrika wanahitaji kudai kwamba vitabu vya mapato ya serikali kutokana na uchimbaji wa madini viwe wazi kwa ajili ya uhakiki wa umma.

Nayo jumuia ya kimataifa inalo jukumu hapa. Pamoja na kuchukua hatua kali moja kwa moja dhidi ya hongo, inaweza kutaka viwepo viwango vya juu (vya utendaji/uwazi) katika makampuni yaliyoko katika nchi zinazoendelea. Pale ambapo hakuna sheria zinazotawala makampuni ya nje, kanuni na viwango vitumike kuongoza tabia na mwenendo. Wabia na walaji hawana budi kutumia uwezo wao kuhakikisha kwamba kanuni na viwango hivyo vinafuatwa.

Juhudi pekee inayotia matumaini katika eneo hili ni ile ya Juhudi Dhahiri ya Kukuza Viwanda vya Usindikaji (EITI) ambayo inatekelezwa katika nchi kadhaa za Afrika. Chini ya juhudi hii, makampuni ya mafuta, gesi na uchimbaji huweka wazi malipo yote ambayo yanatoa kwa serikali na serikali zinatangaza kile ambacho zimepokea kutoka kwa makampuni. Raia mmojammoja au vikundi vinavyofuatilia vinaweza kuhakiki taarifa hizo. Mpango huu bado ni mchanga na bado kuna kazi ya kubainisha vema maana ya kutekeleza mpango huu. Inawezekana usiweze kutatua matatizo yote mara moja, lakini ni hatua muhimu kuelekea kwenye uwajibikaji mkubwa. Jumuiya ya kimataifa na serikali zaidi za Afrika hazina budi kuunga mkono juhudi hizi na kuhimiza nchi zote zenye utajiri wa raslimali hizi kuwa sehemu ya EITI kama zilivyofanya nchi za Nigeria, Ghana, Jamhuri ya Congo na Sao Tome na Principe. Kuwa sehemu ya EITI ni pamoja na kugharimia mafunzo ya watumishi wa serikali na mifumo mingine ili juhudi hizi ziweze kufanikiwa. Asasi za kijamii zinazofuatilia juhudi hizi nazo zitahitaji misaada kama hiyo. Lakini sekta za mafuta na uchimbaji siyo pekee ambako fedha zinapotea kutokana na kutokuwa na menejimenti bora na rushwa. Sekta nyingine, kama misitu na uvuvi, zinaweza pia kunufaika kutokana na uwazi katika mapato, na jumuia ya kimataifa haina budi kusaidia katika hili.

Eneo moja ambalo linaumia sana kutokana na rushwa ni lile la ununuzi – jinsi serikali zinavyonunua bidhaa na huduma. Matumizi mabaya ya utaratibu huu yana mikondo mingi. Wakati tenda za sekta ya umma zinapotangazwa, hongo zinazofahamika kwa njia ya kifisadi kama “bonasi ya utiaji saini” huweza kuombwa au kutolewa. Ankara za awali zinaweza kubadilishwa ili kuweka gharama za uwongo. Siyo wanasiasa na maofisa wa serikali peke yao wanaoleta matatizo haya, bali pia maofisa wa benki, wanasheria, wahasibu na wahandisi wanaofanya kazi kwenye mikataba ya umma. Rushwa hii iliyotapakaa huongeza kiasi cha asilimia 25 ya gharama za ununuzi kwa serikali na mara nyingi matokeo yake yamekuwa kazi duni na manunuzi yasiyo ya lazima. Jukumu la kukabili haya limo mikononi mwa viongozi wa Afrika ambao sharti wadhihirishe utashi wa kisiasa wa kufuata kile ambacho tayari wameanzisha. Lakini jumuiya ya kimataifa inaweza pia kusaidia katika hili. Haina budi kuhimiza njia za wazi zaidi za kuuza bidhaa na huduma katika Afrika na katika nchi zilizoendelea. Vyombo vya nchi tajiri vya kutoa mikopo kwa ajili ya biashara nchi za nje – asasi na taasisi zinazosaidiwa na serikali katika kutoa mikopo, dhamana, muamana na bima kwa makampuni binafsi ambayo yana vitega uchumi au yanafanya biashara katika nchi zinazoendelea – yanaweza kufanya suala la kutotoa rushwa kuwa moja ya masharti ya kupata fedha.

Hizi ndizo hatua muhimu zinazohitajika kuhusu utawala. Tume hii imehitimisha, baada ya kutafakari ushahidi wote, kwamba mpaka hapo kutakapokuwa na mabadiliko katika maeneo haya, basi mabadiliko mengine ambayo tutapendekeza – katika biashara duniani, madeni na misaada – yatakuwa ya mafanikio haba.

## Haja ya kuwa na amani na usalama

Watu wapatao 1,000 hufa kila siku katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo – idadi kubwa zaidi kuliko yote tangu Vita Vikuu vya Pili. Na dunia haijui. Huu ni moja ya migogoro mingi ya Afrika. Katika miongo ya karibuni Afrika imepitia katika mapinduzi ya kikatili, vita vya muda mrefu vya wenyewe kwa wenyewe na mitafaruku ya kisiasa ya umwagaji damu kuliko sehemu yoyote ile duniani. Baadhi ya haya, kama vurugu huko Darfur, yametangazwa sana. Bali kuna migogoro midogo isiyohesabika kama ile kati ya wakulima na wafugaji ambayo iko katika sehemu nyingi za Afrika, ambayo ina madhara yaleyale. Vurugu zinaleta vifo vingi Afrika kama yafanyavyo magonjwa.

Kibinadamu, hii ni gharama kubwa kupindukia. Mamilioni ya maisha yameteketea. Watu wapatao milioni tatu walikufa katika miaka minne ya vita vya wenyewe kwa wenyewe katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo peke yake. Kutokana na migogoro ya ndani ya Nigeria, kwa mfano, watu wapatao 10,000 walipoteza maisha kati ya mwaka 1999 na 2003 na wengine wapatao 800,000 walipoteza makazi yao. Watu wengi zaidi wemelazimika kukimbia makazi yao katika Afrika kuliko mahali pengine popote duniani, na wengi wa hawa wakitua katika makazi yasiyopimwa mijini ambayo tayari yana wakazi wengi kupita kiasi. Utapiamlo na magonjwa vinaongezeka. Na wengi wanaoumia zaidi ni masikini na wanaoishi katika mazingira yasiyo salama. Vita havileti madhara kwa watu peke yake. Vinaharibu barabara, madaraja, zana za kilimo, mawasiliano ya simu na mifumo ya maji safi na maji taka. Vita hufanya shule na hospitali zifungwe. Hupunguza kasi ya biashara na maisha ya kiuchumi na wakati mwingine kusimamisha shughuli hizo. Mfumo mzima wa jamii unachanwachanwa.

Migogoro ina matukio mapana zaidi. Ukosefu wa amani Afrika unadhoofisha usalama wa dunia. Mataifa ambayo yamedhoofishwa na migogoro yameongeza idadi ya wakimbizi kwa ngazi ya kimataifa. Aidha, yanageuka kuwa makao salama ya mashirika ya kigaidi duniani. Katika mazingira kama haya inaweza kuonekana mzaha kuzungumzia mategemeo. Bali mambo yanaanza kubadilika katika Afrika. Kuna matumaini ya amani katika sehemu nyingi ambazo zilikuwa zimevurugika kwa vita katika Afrika, kwa mfano Angola na Sierra Leone. Kuna dalili za matumaini hata katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Sudan na Somalia. Nchi kama Msumbiji, ambayo ilifananishwa na vurugu na mateso, imedumisha amani kwa zaidi ya mwongo mmoja sasa. Tunaendelezaje mabadiliko haya?

### Kinga ni bora kuliko tiba

Hadi sasa mahali pa jumuiya ya kimataifa kuingilia katika migogoro pamekuwa kwenye kutoa misaada ya kijeshi au misaada ya kibinadamu. Bali Tume hii imehitimisha kwamba sharti wafadhili waweke mkazo zaidi kwanza katika kujenga misingi kwa ajili ya usalama wa kudumu wa watu na kusaidia taasisi za Afrika katika juhudi za kuzuia kutokea kwa mapigano. Hii ni kwa sababu kadhaa.

Wakati uhasama wa kutumia silaha umeanza, huwa ni vigumu na ghali kuumaliza – hujenga hatari kubwa ya vurugu katika siku za usoni. Hata kama mapigano yamesimama/yameisha, ushahidi ni kwamba serikali zenye wasiwasi huendelea kuwa na bajeti kubwa ya matumizi ya jeshi. Hii ina maana kwamba raslimali zinachopolewa kutoka kwenye ujenzi wa jamii ambao unakabili baadhi ya matatizo ya kijamii ambayo huenda ndiyo yalikuwa chanzo cha mapigano. Hivyo, nchi ambazo zimepitia katika vita vya

wenyewe kwa wenyewe zina uwezekano wa juu wa kuingia tena katika vita katika kipindi cha miaka mitano. Migogoro ya kivita ni duara jingine la maangamizi ya Afrika.

Gharama ni kubwa pia kwa jamii ya kimataifa. Mara nyingi, mataifa wafadhili huitikia migogoro ya kivita kwa kupeleka majeshi ya kulinda amani na kupitia kazi za kuleta maendeleo wakati mapigano yameisha. Hii ni gharama kubwa. Bajeti ya UN ya shughuli za kulinda amani katika Afrika kwa mwaka mmoja hadi Juni 2005 ni dola bilioni 2.86. Isitoshe, ziko gharama za misaada kwenye maeneo ya vita. Afrika ilipokea karibu dola bilioni 7 katika misaada ya kibinadamu kati ya 1995 na 2001. Kiasi kikubwa cha fedha hizo kilikuwa kwa ajili ya mwitikio wa migogoro.

Vita vina maana ya kujenga upya miundombinu muhimu. Gharama za vifaa vilivyoharibiwa wakati wa vita vya Rwanda ilikuwa dola bilioni moja. Ujenzi mpya wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo unakadiriwa kuwa dola bilioni 20 na hata uchumi ukianza kukua kwa nguvu hivi sasa, itachukua miongo kadhaa kwa nchi kurudia kiwango kilichofikiwa ilipopata uhuru mwaka 1960. Tafiti kadhaa zimeonyesha kwamba kinga ya migogoro inagharimu kidogo kuliko kuingilia kati kumaliza migogoro. Moja ya makadirio ni kwamba ingegharimu dola bilioni 1.5 kuzuia kuzuka mapigano nchini Somalia ikilinganishwa na dola bilioni 7.3 zilizogharimia uingiliaji kati baada ya mapigano kuanza. Askari 5,000 tu wenye uwezo mkubwa wa utekelezaji wangeweza kuokoa nusu milioni ya maisha katika Rwanda. Ushahidi unaonyesha kuwa kinga inawezekana.

Kwa nini basi hapajawa na mkazo kwenye kinga? Kwa kiwango fulani ni kwa sababu ya kile kinachoitwa “utangazaji wa CNN”. Nafasi ya juu inayotolewa na vyombo vya habari kwa baadhi ya dharura, inaweka shinikizo kubwa kwa wanasiasa wa kimataifa kuitikia dharura hizo na wanawapa maslahi ya kisiasa kwa kufanya hivyo. Kwa upande mwingine, kujenga mifumo inayokabiliana na hatari ya kuingia kwenye migogoro inaweza isivutie na kuwa habari kubwa, lakini inafaa sana na haina gharama kubwa. Jumuia ya kimataifa haina budi kuwekeza zaidi katika kuzuia migogoro iwapo inataka kuona Afrika ikichukua fursa hii kwa ajili ya maendeleo na ustawi.

Njia bora ya kufanya hivyo ni kuimarisha mifumo ambayo inaweza kuzuia mivutano isifikie hatua ya migogoro. Mfumo dhahiri kuliko yote kwa kazi hii ni kuwa dola madhubuti lenye mifumo ya kusuluhisha ugomvi kati ya watu binafsi au vikundi kabla haijafikia hatua ya kuwa mapigano. Hapa, Afrika imekuwa na tatizo mara mbili. Ina vyanzo vingi vya wasiwasi na mivutano mikubwa na pia mifumo yake ya kukabiliana nayo ni dhaifu.

Sababu za vyanzo vya mivutano katika Afrika zinatofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine. Bali kuna mazingira kadhaa yanayofanana. Asasi dhaifu na utawala mbovu ni hatari, kama ilivyo utawala wa mabavu, umasikini, ukosefu wa usawa na ubaguzi wa jamii ndogo kwa kutozishirikisha katika utawala. Mataifa ambayo yana viwango vikubwa vya rushwa na viwango vya chini vya uwajibikaji ndiyo yenye uwezekano wa kuwa na migogoro ya mara kwa mara. Hivyo ndivyo ilivyo pia mifumo ya uchumi ambayo inategemea zao moja au mawili yasiyosindikwa kwa ajili ya mapato yake. Kuna kiungo kikubwa kati ya mafuta na utajiri mwingine wa madini, na hatari ya kuzuka kwa migogoro. Mivutano juu ya upatikanaji wa ardhi, maji na raslimali nyingine zisizokuwa za thamani sawa, nayo ni sababu ya migogoro. Aidha, lakini muhimu makundi kama vile ya kikabila, asili au dini, hutumiwa mara nyingi katika kushindania madaraka.

Juu ya hayo, kuna ongezeko kubwa la silaha ambazo zimetapakaa Afrika nzima. Katika baadhi ya nchi bunduki aina ya AK-47 Kalashnikov, ambayo ina sifa ya usahihi katika kufanya mashambulizi, inaweza kununuliwa kwa dola 6. Silaha, hata hivyo, siyo chanzo cha vurugu na migogoro, bali ni kichocheo. Wakati mivutano inapogeuka na kuwa mapigano, ni usambazaji wa silaha ndogo unaofanya migogoro kuwa ya mauaji zaidi. Pale bunduki ya AK-47 inapokuwa silaha badala ya mikuki na mishale, kiwango cha vifo kinakuwa kikubwa zaidi.

kufuatilia biashara raslimali za migogoro na kuhakikisha kwamba vikwazo dhidi ya biashara hiyo vinaimarishwa.

**Jukumu la makampuni ya kigeni katika maeneo yenye migogoro:** Tabia njema ya makampuni ya nje inaweza kuboresha mazingira ya amani na usalama wa Afrika. Mara nyingine, bila kukusudia, makampuni huajiri mashirika ya ulinzi kulinda shughuli zao. Majeshi haya ya binafsi yanaweza kujihusisha na uvunjaji wa haki za binadamu. Silaha zao zinaweza kupokonywa na vikundi vya waasi. Wanaweza kuleta wasiwasi zaidi kwa kuajiri kundi moja la kijamii kwa nia ya kukomoa kundi jingine.

Lakini baadhi ya makampuni huchochea migogoro kwa makusudi. Hulipa fedha nyingi kwa serikali za ukandamizaji au mabwana wa vita; mengine husaidia hata katika ununuzi wa silaha. Baadhi ya matendo haya, kwa mfano uhongaji wa maofisa, moja kwa moja ni makosa ya jinai. Mengine kama kuhamisha wenyeji kutoka kwenye ardhi yao, tena kwa kutumia nguvu, ni makosa ya jinai pia chini ya sheria ya kimataifa. Bali matendo yao mengi siyo jinai – na hivi sasa kanuni za mwenendo wa makampuni, kama vile Mwongozo wa Makampuni ya Kimataifa wa Shirika la Ushirikiano wa Uchumi na Maendeleo (OECD), hazitoi maelezo yaliyo wazi vya kutosha juu ya nini makampuni yafanye katika mazingira kama haya. Miongozo kama hii sharti iandikwe upya ili iingize vipengele vinavyohusu jinsi ya kuzuia kuleta, au kuchochea migogoro. Chombo kipya cha kudumu katika UN ambacho kimetajwa hapo juu, sharti kipewe jukumu la kufuatilia utekelezaji wa miongozo hii, bila umotishaji kwa kukabiliana na kila anayeivunja.

**Ujenzi wa uwezo wa kuzuia na kutatua migogoro:** Migogoro hushughulikiwa vema na wale walio karibu nayo. Vyombo na mifumo ya ndani ya nchi au ya kitaifa ndiyo hatua ya kwanza ya kukabiliana na migogoro. Wakati mifumo hii inaposhindwa, ndipo mashirika ya kikanda na kimataifa yanapochukua jukumu la kuzuia na kutatua migogoro ya kivita na kulinda uhai wa raia. Katika miaka ya karibuni, Jumuia za Uchumi za kanda za Afrika na UA, zimekuwa zikishughulikia hili. Vyombo hivi vinajenga uwezo wake wa kugundua migogoro na kupatanisha, na kuweka ulinzi wa amani kwa kutumia majeshi iwapo hiyo inahitajika. Jumuiya ya kimataifa imedhamiria hivi karibuni kuimarisha uwezo wa ulinzi wa amani katika Afrika. Ahadi hizi hazina budi kutekelezwa kupitia, kwa mfano, misaada ya mafunzo na vifaa kwa ajili ya Jeshi la Akiba la Afrika (ASF) – jeshi la kulinda amani ambalo linaundwa na UA. Zaidi ya hayo, jumuiya ya kimataifa sharti iongeze uwekezaji katika kuzuia migogoro na katika njia zisizo za kijeshi za kumaliza migogoro.

Mataifa yaliyoendelea hayana budi kusaidia mashirika ya kanda ya Afrika katika mifumo ya kutoa tahadhari, upatanishi na ulinzi wa amani. Jumuiya ya kimataifa nayo haina budi kuwasaidia kwa kuwapa rasilmali za kuendeshea shughuli maalum, kama vile upatanishi, tume za kutafuta ukweli na ulinzi wa amani. Uchangiaji kifedha wa mara kwa mara – nje ya fedha zilizopangwa rasmi – kupitia, kwa mfano, ugharimiaji kwa nusu Mfuko wa amani wa Umoja wa Afrika kila mwaka – utawezesha taasisi kama hizo kupata haraka rasilmali pale zitakapohitajika. Kazi za asasi kama vile za kidini hazina budi kuchukuliwa na UA na mashirika ya kanda kusaida kugundua na kusuluhisha migogoro.

Umoja wa mataifa una jukumu muhimu katika kusaidia juhudi za mashirika hayo ya kanda – na kwa uwezo wake kuzuia na kuamua migogoro ya kivita. Jumuiya ya kimataifa haina budi kusaidia kuundwa kwa Tume ya Kulinda Amani ya Umoja wa Mataifa kama ilivyopendekezwa hivi karibuni na Jopo la Mabingwa wa Umoja wa Mataifa la Masuala ya Matishio, Changamoto na Mabadiliko (UNHLP). Chombo hiki kitafanya kazi ya kuzuia, kupanga na kuratibu mipango ya ujenzi wa amani katika kipindi kinachofuata mgogoro. Umoja wa Mataifa unafasili ujenzi wa amani kuhusisha kila kitu kutoka uzuiaji wa migogoro hadi ujenzi wa taasisi na miundombinu ya mataifa yaliyoharibiwa na vita – na vilevile kuhitaji kukabili vyanzo vya mgogoro kama vile ukosefu wa usawa katika uchumi, udhalimu wa kijamii na ukandamizaji wa kisiasa.

Wanachama wa UN hawana budi pia kuunga mkono mageuzi yanayofanywa katika usimamizi na utafutaji wa fedha kwa shughuli za kulinda amani za umoja huo ili kuongeza kasi ya usambazaji wa askari. Hawana budi kuongeza juhudi ya kuwafunza askari wao kazi za kulinda amani – ikiwa pamoja na kuipa aula Afrika katika uundaji wa "makundi ya vita" unaoandaliwa na EU ili kuweza kuitikia kwa haraka maombia kwzsaada wa kijeshia kwAfrika.

### Baada ya vita kumalizika

Vita vinapomalizika, amani haiji mara moja. Mara nyingi, matatizo mapya hutokea baada ya kuwanyang'anya silaha askari na kuwaruhusu kwenda makwao. Matatizo haya ni pamoja na jinsi ya kuwaingiza upya katika jamii, askari wanaorejea na wakimbizi ambao hukuta nyumba zao tayari zimekaliwa na watu wengine ambao hawawakaribishi. Na matatizo ya zamani hujitokeza upya, kama vile dhuluma na chuki ambavyo ndio vilisababisha migogoro. Yote haya ni zaidi ya miundombinu iliyoharibiwa, ukosefu wa taasisi zinazofanya kazi na umaskini uliopindukia. Hii ndiyo inafafanua kwa nini nusu ya nchi zilizotoka kwenye migogoro hurejea kwenye migogoro katika kipindi cha miaka mitano.

Ujenzi wa amani baada ya migogoro ni jukumu kubwa linalohusisha mahitaji mengi yanayoshindana. Utaratibu wa kimapokeo katika hili umekuwa kusisitiza kwamba sharti amani ije kwanza na maendeleo ya uchumi baadaye. Lakini kinachofaa zaidi kuleta amani ya kudumu ni tofauti. Ni dhahiri kwamba sharti usalama urejeshwe kwanza. Lakini wapiganaji hawahitaji tu kunyang'anywa silaha, wanahitaji kupewa kazi na mafao ya amani. Vivyo hivyo kwa wakimbizi ambao wanarejea nyumbani. Uchumi wa vita unapaswa kuondolewa na kuweka badala yake fursa za kiuchumi. Sharti hatua zichukuliwe kuzuia wale, kama mabwana wa vita, ambao wana maslahi katika kuharibu hatua zozote zile za kuleta amani. Mahitaji maalum ya wanawake sharti yafikiriwe kwa kuwa ubakaji na matendo mengine ya kiharamia dhidi ya wanawake – ambayo yanashamiri sana wakati wa vita – yana madhara makubwa ya muda mrefu. Mipango maalum itahitajika kwa ajili ya "askari watoto". Njia zote hizi ni za muda mrefu na zimechangamana kupindukia, ikiwa na maana kwamba ucheleweshaji wa mara kwa mara kati ya shughuli za kujenga amani na kuanza kwa maendeleo ya kijamii na uchumi, sharti uepukwe.

Upatanishaji ni muhimu kama ulivyo ujenzi katika kuondoa madhara ya vita kwa jamii. Huu unachukua mifumo mingi. Ulio wazi zaidi ni kuanza kushughulikia uvunjaji wa haki za binadamu ili waliokumbwa na mikasa waanze kuhisi kuna haki. Kwa hiyo,wzsaada mkubwa kwa sekta ya haki ni muhimu. Ujenzi mpya sharti uepuke kurejesha mambo ambayo yalikuwepo kabla ya vita na ambayo huenda yalikuwa miongoni mwa sababu za migogoro. Hatua za kuleta amani zina hulka ya kuwa za kisiasa mno na huhitaji msaada endelevu katika upatanishaji hata baada ya kuwa na mkataba wa amani.

Kufaulu katika ujenzi wa amani katika kipindi baada ya vita hutegemea mambo mawili: uratibu na mipango, na fedha. Uratibu na mipango waweza kuboreshwa kwa kuundwa kwa Tume ya Kulinda amani ya Umoja wa Mataifa. Na nchi zinazotoka kwenye migogoro zinahitaji fedha ili kuziwezesha kuanza mapema juhudi za ujenzi mpya na maendeleo. Msaada wa aina hii unahitaji kuendelea kwa miaka ipatayo 10 baada ya vita kumalizika.

Hii ni jumla ya mapendekezo changamani na yenye malengo. Lakini njia ambazo huendeleza migogoro ya kivita ni za muda mrefu, zilizochangamana na ambazo hazina ufumbuzi rahisi. Iwapo tunaweza kuanza kuangalia masuala haya kwa pamoja,wzaisha ya baadaye ya watoto wa Afrika yanaweza kuwa tofauti kabisa.

## Asiachwe mtu nje: Uwekezaji katika watu

Wasiwasi wetu kwenye Tume umehusu hasa watu maskini sana wa Afrika. Huko Ethiopia kaya ambazo ni fukara kupindukia huitwa "wale wanaopika maji." Huko Ghana wanaitwa "wale wenye vikapu viwili" – kimoja cha kuombea wakati wa njaa na kingine cha kuombea wakati neema.

Karibu moja ya sita ya wakazi wa bara la Afrika – hiyo ni zaidi ya wanaume, wanawake na watoto milioni 100 – ni maskini wa kudumu. Ni watu wanaoishi katika umaskini kiasi uliong'ang'ania kwamba hawawezi kujikwamua kwa kutumia raslimali walizonazo. Wanategemea kazi ya siku. Wana elimu ndogo na vitu vichache vya thamani. Kipindi kigumu cha kuugua kinaweza kusababisha wauze walichonacho ili wale. Mgogoro mdogo tu unaweza kuwatokomeza kwenye njaa na ufukara zaidi.

Ni watu binafsi na kaya zilizonaswa katika duara la maangamizi la umaskini. Mara nyingi wanachagua kulima mazao ambayo hayazai sana kwa kuwa ndiyo yasiyo na hatari ya kukauka wakati mvua zisipopatikana. Hawathubutu kujenga matumaini. Na maduara ya maangamizi ya umaskini huwazamisha katika vina virefu zaidi. Wakati wazazi wanashindwa kuwekeza katika afya, elimu, ufundi au lishe ya watoto wao, watoto hao watakuwa na hali ngumu na labda kuwa maskini pia. Msemo mwingine wa kiafrika unaoelezea vyema maduara haya ya umaskini; huko Zimbabwe wanazungumzia "umasikini unaotaga mayai."

Lakini umaskini, mara nyingi, ni zaidi ya ukosefu wa vitu. Watu maskini sana ni wale ambao wametengwa na kuwekwa mbali na raslimali za misaada ambazo hutolewa na serikali, mashirika ya kutoa misaada au hata mifumo isiyo rasmi ya misaada katika jamii.

Mara nyingi hii imetokana na ubaguzi. Baadhi ya watu wanatengwa kutokana na utambulisho wao – kama wanawake, kama wasiojiweza, au mtu wa kabila au asili ya kundi tofauti. Baadhi wanabaguliwa kutokana na lugha au unyanyapaa kutokana na ugonjwa kama vile Ukimwi. Wengine wanabaguliwa kwa kuwa ni wadogo kiumri, yatima, albino, vikongwe, wakimbizi, watu wa asili fulani au wahamahamaji. Wote hawana uwezo wa kupambana na kutengwa huko.

Makundi mawili kati ya haya, hakika siyo ya wachache – wanawake na vijana. Wanawake wanaweza kuwa ndio watunzaji na wazalishaji wa kwanza katika Afrika lakini wanatengwa katika kupata taarifa, huduma na katika vyombo vya utoaji wa maamuzi. Vijana wa umri wa chini ya miaka 17 sasa wanakadiriwa kuwa ndio asilimia 50 ya idadi yote ya wakazi wa Afrika, lakini hawana sauti katika maamuzi mengi yanayowahusu.

Nafasi ya wanawake ndiyo inasikitisha sana, siyo tu kuhusu suala la haki za binadamu, bali kwa kuwa ushahidi unakubali kwamba wanatoa mchango mkubwa kwa uhai wa uchumi kuliko wanaume. Wanawake ndio uti wa mgongo wa uchumi wa vijijini katika Afrika, wakisimamia asilimia 70 ya chakula, sehemu kubwa ya mazao ambayo kaya zinauza, na nusu ya mifugo ukiongezea kuandaa chakula, kuchanja kuni, kuchota maji, utunzaji wa watoto na utunzaji wa wagonjwa na wazee. Wanawake hutumia sehemu kubwa ya mapato yao wanayomiliki kwa mahitaji ya familia, hasa kwa watoto, wakati wanaume hutumia kiasi kikubwa kwa manufaa yao binafsi.

Bado wanawake wana fursa chache za kuingiza mapato; wana uwezekano mdogo wa kwenda shule; wamekuwa watu wa kubugudhiwa na kufanyiwa vurugu; na wanapokuwa wajane hunyang'anywa kila kitu. Utafiti uliofanywa Namibia umeonyesha kuwa asilimia 44 ya wajane walipoteza ng'ombe, asilimia 28 walipoteza mifugo, asilimia 41 walipoteza zana za kilimo katika migogoro na wakwe zao. Katika nchi nyingi za Afrika, wajane hupoteza haki zote za kulima kwenye ardhi ya waliokuwa waume zao.

Changamoto za Afrika haziwezi kukabiliwa ipasavyo hadi hapo ubaguzi unaowakabili wanawake utakapokuwa umeondolewa. Sharti wanawake washshirikishwe na uwezo wa stadi zao uendelezwe. Wanawake ni sehemu muhimu ya ufumbuzi wa matatizo ya Afrika. Ndivyo ilivyo pia kwa makundi mengine yanayoachwa nje, kwani kwa sehemu fulani ushirikishwaji unapunguza mivutano ambayo huleta migogoro, lakini pia kwa sehemu kubwa, ushahidi umeonyesha kwamba maendeleo hushamiri iwapo hakuna anayeachwa nje.

## Elimu kwa wote

Elimu kwa wote ni kichwa cha ahadi za kusisimua kuliko zote ambazo jumuiya ya kimataifa iliishawahi kutoa. Kwenye UNHLP mjini Dakar, Senegal mwaka 2000, mataifa yaliahidi kutoa elimu ya msingi bure kwa kila mtoto duniani ifikapo 2015. Ujinga kwa watu wazima uwe umepunguzwa kwa nusu na wasichana wawe wamepewa fursa sawa na wavulana katika shule za msingi na sekondari ifikapo 2005. Mwaka 2002 zilianzishwa juhudi za kutoa raslimali zinazohitajika kutekeleza ahadi hii.

Maendeleo kadhaa yamepatikana. Idadi ya wanafunzi katika shule za msingi Afrika iliongezeka kwa asilimia 48 kati ya 1990 na 2001. Lakini huduma ni haba na za hapa na pale. Sehemu za vijijini bado ziko nyuma. Wasichana, watoto wasiojiweza na yatima bado wanapuuzwa. Watoto wapatao milioni 40 hawako shuleni. Pamoja na kauli nzito ya Elimu kwa Wote (EFA), jumuiya ya kimataifa haijatoa fedha zinazolingana na ahadi zake. Sasa wafadhili wanahitaji kutoa nyongeza ya kiasi cha dola 7 – 8 bilioni kila mwaka kutimiza kile walichoahidi na kuhakikisha kwamba sekta nzima inapata fedha za kutosha – kuanzia shule za msingi hadi sekondari na elimu ya juu, ikiwa ni pamoja na elimu ya watu wazima na elimu ya ufundi stadi. Hii itawezesha kufutwa kwa karo katika shule zote za msingi Afrika.

Fedha hizi sharti zitumike katika maeneo matatu ya kipaumbele:

**Walimu wengi madarasani:** Afrika ina viwango vikubwa vya upungufu wa walimu. Lesotho ina moja ya tano ya idadi ya walimu wanaohitaji, na Ghana itahitaji mara nne ya walimu waliopo iwapo watoto wote wa umri wa kwenda shule wataandikishwa kuanza shule. Matokeo ya upungufu wa walimu siyo tu kuwa na madarasa yenye wanafunzi wengi bali kushuka kwa ubora wa elimu. Sharti fedha nyingi ziwekezwe katika kufundisha walimu, uwezeshaji walimu na wafanyakazi wengine kubaki kazini na uendelezaji wa taaluma. Nchi wafadhili na mashirika ya fedha ya kimataifa sharti yabadili sera zao ili kuruhusu matumizi ya kawaida ya serikali – ikiwa ni pamoja na mishahara ya walimu – yatokane na misaada.

**Wasichana zaidi madarasani:** Tafiti zimeeleza kwamba kupeleka wasichana shuleni ni muhimu sana kwa maendeleo. Uzalishaji kiuchumi huongezwa kwa kuelimisha wasichana. Viwango vya vifo vya watoto na wajawazito hushuka. Lishe na afya huwa bora. Ueneaji wa VVU hupunguzwa. Kuwapa wasichana mwaka mmoja zaidi wa elimu husukuma juu ujira wao kwa asilimia kati ya 10 na 20. Na uwekezaji wa maana ni uwekezaji katika kizazi kijacho. Uondoaji karo shuleni utasaidia hasa wasichana, kama ilivyo chakula cha bure shuleni na misaada mingine ya kuwapa motisha. Kuondolewa kwa karo mashuleni nchini Uganda kuliongeza, kwa karibu mara dufu, idadi ya wasichana maskini shuleni. Wafadhili hawana budi kusaidia katika hili hadi nchi zitakapokuwa zimepata uwezo, na serikali za Afrika zinahitaji kuwa na mipango itakayowezesha kupatikana kwa haki zaidi kwa wasichana.

**Ufundishaji mambo muhimu:** Mitaala ya elimu katika Afrika nzima sharti iwe ya maana. Kwa kiwango kikubwa, mihtasari iliyopo sasa inakomea kwenye masomo ya nadharia. Masomo ya kuwezesha mtu kupata stadi za kufaa kwa ajili ya kuendeleza tabia za ujasiriamali au kutafutia kazi, hayapewi uzito. Stadi za maisha za kukabiliana na VVU na Ukimwi ni muhimu. Uendelezaji wa mitaala katika Afrika sharti uendeshwe na kila nchi kwa kuangalia kazi za taasisi za elimu katika kanda za Afrika.

### Ufufuaji wa huduma za Afya za Afrika

Mmoja kati ya watoto sita wa Afrika hufa kabla ya kufikisha umri wa miaka mitano. Hii inatokana hasa na mifumo ya utoaji huduma ya afya ambayo iko katika hali ya kuporomoka kufuatia kudhoofika kwa miaka mingi ya uwekezaji hafifu.Wastani wa matumizi ya afya kwa mtu mmoja katika Afrika kwa mwaka 2001 ulikuwa kati ya dola 13 na 21; katika nchi zilizoendelea ni zaidi ya dola 2,000 kwa mtu kwa mwaka. Lakini bado kuna dalili ya matumaini. Baada ya Azimio la Abuja mwaka 2000, asilimia 45 ya nchi za Afrika zimeongeza bajeti ya afya, baadhi yao wakifanya vizuri zaidi kwa kufikia zaidi ya asilimia 10 ya matumizi ya serikali. Wafadhili hawana budi kusaidia katika hili kwa kutoa nyongeza ya dola 10 bilioni kila mwaka ifikapo 2010 za kuongeza hadi dola 20 bilioni kwa mwaka ifikapo 2015 wakati mifumo ya afya itakapoimarika. Bila kuchukua hatua hapa, vitegauchumi vingi katika katika sekta ya afya vitakwama. Maendeleo ya maana yanaweza kupatikana katika kipindi kifupi kwa wafadhili kuunga mkono mipango ya kuimarisha misingi ya mifumo ya afya ambayo imewekwa katika programu za NEPAD. Maeneo yafuatayo sharti yapewe kipaumbele:

**Tatizo la wafanyakazi wa afya:** Kufundisha madaktari, wauguzi na watoa huduma wengine katika sekta ya afya na kuhakikisha kwamba wanaendelea kuwepo, ni jukumu lililopuuzwa. Idadi yao ni ndogo lakini ubora wa kazi pia uko chini. Wengi kati ya walio bora wamevutiwa kufanya kazi nje ya Afrika. Wengine – wakiwa wamekatishwa tamaa kufanya kazi bila dawa au zana nyingine wanazohitaji – wamepata kazi za huduma ya afya zenye mishahara minono nje. Mabadiliko makubwa yanahitajika. Idadi ya wafanyakazi wa afya katikaAfrika inapaswa kuongezwa mara tatu zaidi kwa kufundisha nyongeza ya wafanyakazi milioni moja katika muongo mmoja. Mishahara haina budi kuongezwa kuhakikisha kwamba watumishi hawashawishiwi kuacha kazi zao.

**Dawa:** Afrika inahitaji dawa na chanjo kwa gharama inayoweza kumudu. Hii ina maana ya kununua dawa kwa wingi ili kupunguza gharama. Ina maana ya kutoa vishawishi kwa makampuni ya kutengeneza dawa kufanya uchunguzi wa magonjwa yanayoisibu Afrika, badala ya kuelekeza juhudi zao kwa magonjwa ya nchi tajiri. Wafadhili wanapaswa kufanya kununua hmatuka mchika hali zamatumizsibu AfwingiTc (makampuni ya kutengeneza artat zeothakikwu

s a

Tanzania kunaweza kugharimu dola 31milioni. Kuondolewa kwa malipo kwa wagonjwa nchini Uganda kumefanya matumizi ya kliniki yaongezeke zaidi ya mara mbili; na watu maskini sana ndio wengi. Nchi tajiri hazina budi kusaidia kuondolewa kwa gharama kwenye huduma za afya hadi hapo serikali za Afrika zitakapokuwa na uwezo wa kugharimia. Huduma ya msingi ya afya inapaswa kuwa ya bure kwa watu maskini.

**Utokomezaji wa magonjwa yanayozuilika:** Afrika inateswa na magonjwa mengi ambayo yanaweza kuzuiwa kabisa. Theluthi mbili za watoto wote wa Afrika wanaokufa wakiwa chini ya umri wa miaka mitano wanaweza kuokolewa na tiba ya gharama ya chini kama Vitamini A, maji ya dripu na vyandarua vilivyowekwa dawa ili kupambana na malaria. Moja ya kumi ya magonjwa yote yanayowasumbua watoto wa Afrika yanasababishwa na minyoo tumboni iliyoambukiza watu milioni 200 na ambayo inaweza kutibiwa kwa senti 25 za dola kwa kila mtoto. Wengi wa wanawake 250,000 wanaokufa kila mwaka kutokana na matatizo ya mimba au wakati wa kujifungua (ikilinganishwa na 1,500 Ulaya) wangeweza kuokolewa iwapo serikali za Afrika na wafadhili wangeweka msisitizo mkubwa juu ya huduma ya afya ya uzazi.

### Upanuzi wa huduma za maji na usafi

Zaidi ya milioni 300 – kama asilimia 42 ya idadi yote ya wakazi wa Afrika – hawana njia ya kupata maji salama. Karibu asilimia 60 bado hawana uwezo wa mazingira bora ya msingi. Kupatikana kwa maji kungewaondolea wanawake na wasichana adha ya kwenda kwa miguu wastani wa kilometa sita kuteka maji, na kungewapa muda zaidi wa shughuli za familia, shule na kazi nyingine za uzalishaji. Bila maji safi, dawa za kurefusha maisha kwa wenye ukimwi haziwezi kuleta matokeo yanayotarajiwa, maziwa ya unga hayawezi kutumiwa kwa usalama kuzuia uambukizwaji wa VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Usimamizi bora wa maji unaweza kupunguza, kwa kiwango kikubwa, mazalio ya mbu wanaoeneza malaria. Bali misaada kwa sekta hii imeshuka kwa asilimia 25 tangu 1966. Kushuka huku kumetokana na kutoona mbali ambako sharti kubadilishwe mara moja ili kutoa kipaumbele kwa nchi zinazohitaji zaidi misaada. Nchi za kundi la G8 tayari zina mpango kamambe wa maji kwa Afrika. Huu ndio wakati wa kutekeleza ahadi hizo.

### Ulinzi wa wasiojiweza

Njia nyingine ya kusaidia watu maskini ni kwa dola kulipa kwa fedha taslimu posho kwa watoto, wajane na yatima, watu wenye ulemavu au wazee wanaopata pensheni. Huu "ulinzi wa kijamii" unaweza kutolewa kwa njia isiyo ya fedha taslimu, kwa mfano kwa njia ya huduma za bure za afya za msingi na elimu, chakula cha bure shuleni, mifumo ya dhamana ya kupata kazi au utoaji mafunzo ya stadi kwa watu maskini. Huduma hii yaweza kutolewa pia kwa kutetea haki za watu, hasa za wanawake na watoto kuhusu urithi na ulinzi dhidi ya ukatili majumbani na ubakaji.

Serikali nyingi za Afrika zinaongeza hatua za ulinzi wa kijamii kwa kuwa ushahidi wote unaonyesha kuwa ni nafuu – ni rahisi sana kuliko gharama za kukabili mgogoro baada ya kutokea. Mahudhurio shuleni yameongezeka kwa asilimia 90 nchini Zambia tangu kutolewa kwa posho za dola 6 kwa mwezi kwa wazee wanaolea watoto waliokuwa wanaishi katika mazingira yasiyo salama na lishe imekuwa bora. Ikijumuishwa na uendeshaji, gharama inakuwa dola 100 kwa kila kaya kwa mwaka badala ya dola 250 kwa mwaka kwa msaada wa chakula. Wafadhili wa kimataifa wanastahili kuunga mkono aina hii ya mabadiliko katika mbinu na kutoa fedha zinazoweza kuleta faida ndogo lakini kwa watu wengi. Wafadhili hawana budi kutoa dola 2 bilioni kwa mwaka, kwa kuanzia, na kupanda hadi dola 5 hadi 6 bilioni kwa mwaka, kwa yatima, watoto wasio na makazi salama na watoto waliokuwa katika majeshi. Fedha hizi hazina budi kulipwa kupitia kwenye familia na jamii zinazotunza asilimia 90 ya yatima. Kwa jinsi mzigo wa Ukimwi unavyozidi kuwa mzito, mifumo hii itaanguka iwapo haitapata misaada.

## Kwa nini janga la Ukimwi ni kubwa zaidi Afrika

Janga la ukimwi linalokabili dunia nzima lina makali ya kipekee kwa Afrika ambako wanaishi asilimia 62 ya vijana wa umri kati ya miaka 15 na 24 wenye VVU. Kiwango cha ugonjwa huu uluoenea kote duniani kinavunja moyo. Tayari watu wapatao milioni 25 wamekufa na viwango vya umri wa kuishi katika baadhi ya nchi za kusini mwa Afrika, vimerudi kuwa kama vile vya kabla ya mwaka 1950. Watu wengine 25 milioni wanaishi na VVU ikiwa ni pamoja na asilimia 40 ya idadi ya watu nchini Botswana. Maana ya yote haya kiutu, kijamii na kiuchumi hayajawa wazi vizuri.

Ukimwi hauteketezi kizazi kimoja. Unashammbulia vizazi vitatu – mtu anayeishi na VVU au mgonjwa wa ukimwi, lakini pia watoto ambao wamezaliwa na VVU na mababu ambao wanabanwa na utoaji huduma kwa watoto na uzalishaji wa chakula ambao unadhibitiwa na umri wao mkubwa.

Ukimwi una madhara pia kwenye uchumi. Hasa unaathiri wale waliomo kwenye umri wa kufanya kazi. Asilimia 90 ya watu wanaoishi na VVU na ukimwi wako kati ya umri wa miaka 15 na 49. Hii ina maana kwamba, kwa makadirio ya mbele, kati ya asilimia 20 na 40 za nguvu kazi itapotea katika nchi ambazo zimezongwa sana na Ukimwi. Ukimwi unashambulia katika njia ambazo hazikutarajiwa. Wakulima nchini Zimbabwe ambao waliona mifumo yao ya umwagiliaji ilikuwa haiendi vizuri, waligundua kwamba viungo vya shaba nyeupe vya mabomba ya maji vilikuwa vimeibwa na vinatumika kutengenezea mikono ya majeneza.

VVU na Ukimwi huathiri kwa kiwango kisicholinganifu, wanawake ambao mara nyingi huwa na jukumu kubwa katika kuleta maendeleo. Kati ya watu 25 milioni wanaoishi na VVU na Ukimwi katika Afrika, karibu asilimia 57 ni wanawake, ikilinganishwa na asilimia 47 sehemu nyingine duniani. Takwimu kutoka Zambia zinaonyesha kwamba vijana wa kike wana uwezekano wa mara tatu wa kupata maambukizi kuliko vijana wa kiume. Wanawake wana uwezekano mkubwa zaidi wa kibaolojia wa kuambukizwa lakini sababu kuu za hatari ni za kijamii: kuanza mapema mahusiano ya kujamiiana, hadhi ya chini kiuchumi na kutokuwa na uwezo wa kung'ang'ania kutumia kondomu.

Urithi wa yote haya ni idadi kubwa ya yatima. Mwaka 2003 Afrika ilikuwa na yatima 43 milioni, 12 milioni kati ya hao wakiwa wanatokana na Ukimwi. Bali idadi hiyo inaelekea kuongezeka – hadi 18 milioni ifikapo mwaka 2010 na kukua zaidi angalau katika mwongo mwingine. Mapana ya athari hizi kijamii yanasikitisha sana – huko Zambia asilimia 71 ya watoto makahaba ni yatima.

Athari za kijamii na kiuchumi za VVU na Ukimwi zimeenea. Wale waliopata mavuno mazuri ndio hukopesha wale ambao hawakupata, lakini katika maeneo ambako kuna matukio mengi ya Ukimwi, kiwango cha ziada kwa ajili ya kukopesha wasionacho kimepungua sana. Kaya ambazo zimeathirika kwa VVU zina akiba ndogo sana na huwekeza kidogo na watoto wao mara nyingi hufukuzwa shule. Katika miaka 20 ijayo uchumi wa nchi zinazoendelea ambazo zimeathirika sana kwa Ukimwi utakuwa umekua kwa theluthi moja tu ya ambavyo ungekuwa umekua.

Hadi hivi karibuni VVU na Ukimwi vimekuwa havipewi kipaumbele na wafadhili, lakini viwango vya ugharimiaji sasa vinapanda. Hata hivyo ni muhimu kwa jumuia ya kimataifa kutochukulia ukimwi kama tatizo la tiba. Kukabili ugonjwa huu kunahitaji mifumo ya afya iliyo imara na dawa. Lakini pia kunahitajika mwitikio wa kitamaduni na kiuchumi. Katika moja ya mashauriano yetu tulisikia maelezo ya kusikitisha ya mwanamke wa Nairobi aliyeeleza kwamba itamchukua miaka mitano kusalimu amri kwa Ukimwi, lakini itachukua miezi michache tu kwa mtoto wake kufa kwa ukosefu wa chakula; kwa hiyo kufanya ngono isiyo salama kwa ajili ya kupata fedha, lilikuwa jambo la kimantiki, kwa kuwa ndiyo ilikuwa njia pekee ya kuendelea kuweka mtoto wake hai. Hiyo ndiyo mantiki ya kuogofya ya umaskini.

Ukimwi hautatokomea hadi hapo wanaoukabili watakapozingatia sababu za kiutamaduni za umasikini na uwezo wa kuchagua, mila na imani, utambuzi wa maisha na kifo, uchawi na adhabu za mababu waliokufa, ngazi za madaraka na kanuni za jinsia, miiko ya jamii na kanuni za kuchezwa, udhibiti wa ashiki za mwanamke na matakwa ya urijali kwa mwanaume, na shinikizo la wajane kuolewa na ndugu wa karibu wa mwanaume aliyekufa kwa Ukimwi hivi karibuni. Wafanyakazi wa afya sharti wakabiliane na masuala kama haya, waunde ushirikiano na viongozi wa dini na waganga wa asili ambao mara nyingi huwa na uelewa wa utamaduni, jinsia na mahusiano kimadaraka.

Yote haya yatahitaji gharama ya nyongeza. Lakini ahadi zilizopo, ambazo zilitokana na azimio la UN juu ya VVU na Ukimwi, bado hazijatekelezwa kikamilifu. Hii ni kwa sababu, wafadhili kwa mara nyingine, hawatoi kile walichoahidi. Hii pia ni kwa sababu wanaotoa misaada wana mitazamo inayosigana, hawa wakitetea kutofanya ngono na wengine wakitetea matumizi ya kondomu. Ni kwa sababu pia wafadhili wanalundikana katika sehemu moja, huku wakiacha mianya ikijotokeza sehemu nyingine. Hapa ni muhimu kwa nchi tajiri kukubaliana juu ya msimamo mmoja – wakiwa na mpango maalum wa utoaji fedha, makubaliano juu ya majukumu ya kila mmoja na msimamo mmoja wa tabia njema. Lakini fedha zaidi zinahitajika pia. Hivi sasa hakuna raslimali za kutosha kutoa mpangilio unaofaa wa utoaji huduma za kinga na tiba. Wafadhili wa kimataifa hawana budi kuongeza mara moja fedha ili kukidhi mahitaji ya sasa. Fedha hizo zinahitaji kuongezeka hadi angalau dola 10 bilioni kwa mwaka katika kipindi cha miaka mitano. Mapambano dhidi ya VVU na Ukimwi sharti yapewe kipaumbele cha kwanza na jumuiya ya kimataifa.

### Kupata Matokeo

Raslimali kubwa zitahitajika katika maendeleo ya watu ili kuleta mabadiliko. Karibu nusu ya misaada zaidi tunayopendekeza inastahili kutumika katika afya, elimu na VVU na Ukimwi. Lakini kupata matokeo hapa, kama ilivyo katika maeneo mengi mengine, siyo suala la kutupa fedha kwenye matatizo. Matumizi bora ya raslimali hizi mpya zinazoingia yatahitaji mikakati thabiti ya utoaji fedha na ufuatiliaji wa matokeo. Hadi hapo, serikali za Afrika sharti ziendelee kuimarisha utawala na kuhakikisha ushiriki wa watu wa kawaida na jamii katika kufikia maamuzi juu ya maendeleo. Iwapo jumuiya ya kimataifa itakubaliana na hilo kwa kutekeleza ahadi zake, basi matokeo yatakuwa makubwa – kukamilisha matakwa kibinadamu na katika kujenga msingi wa ukuaji kiuchumi.

## Kuelekea kwenye ukuaji wa Uchumi

Miaka thelathini iliyopita Botswana ilikuwa moja ya nchi maskini sana na zilizotegemea zaidi misaada duniani. Leo, nchi hii ambayo haikupakana na bahari ni moja ya nchi zilizofanikiwa sana katika Afrika. Imepitia hatua thabiti za ukuaji wa uchumi hadi kufikia kuwekwa sasa katika kundi la nchi zenye 'mapato ya kati.'

Hilo siyo jambo la kushangaza, watu wengi wanaweza kusema. Hata hivyo, Botswana ina almasi. Lakini mara nyingi Afrika hugeuza hekima ya mapokeo kichwa chini miguu juu. Angalia bara zima na utaona kuwa ni nchi zenye madini mengi sana na utajiri mwingine ambazo zimo katika matatizo kupindukia. Katika nchi nyingi, raslimali huleta vita. Hutajirisha tabaka la juu lakini kwa watu wengi rasliamli hizo huongeza rushwa, huharibu mazingira na kuleta udhaifu kisiasa. Matumizi kwa ajili ya elimu na afya yako chini katika nchi hizo. Lakini Botswana imekwepa mwelekeo huo.

Afrika ndiyo ukanda maskini sana kuliko yote duniani. Kwa zaidi ya miaka 30 iliyopita watu wake, kwa wastani, hawajaona ongezeko lolote kwenye mapato yao. Ujumbe ni wazi: Bila kukua kwa uchumi, Afrika haiwezi kupunguza umasikini kwa kiwango cha maana. Hapa tena, Botswana ndiyo ushahidi. Tasnia ya almasi inaajiri karibu asilimia mbili ya wafanyakazi

wachache wa Botswana ambao kazi zao zinatambulika katika uchumi wa nchi. Bali mapato kutoka tasnia ya almasi na kuingia kwenye hazina ya serikali, yamewekezwa na siyo kufujwa. Uchumi umekua na idadi ya watu wanaoishi katika umaskini mbaya imeshuka kwa kasi. (Na bado, Botswana vilevile inaonyesha tishio kubwa linalokabili ukuaji na maendeleo ya Afrika – ina moja ya viwango vya juu vya VVU na Ukimwi katika Afrika).

Kwa hiyo Afrika haijalaaniwa kuwa na makuzi goigoi. Botswana siyo mfano pekee. Katika muongo uliopita, nchi 16 za kusini mwa jangwa la Sahara zimekua kwa wastani wa zaidi ya asilimia nne, ikiwa ni pamoja na 10 zenye viwango vya zaidi ya asilimia tano na tatu zenye viwango vya zaidi ya asilimia saba. Tume hii inaamini kwamba mapendekezo haya tunayotoa hayana budi kuwezesha nchi za Afrika kupata na kuendeleza viwango vya ukuaji vya asilimia saba ifikapo mwisho wa mwongo huu.

Ni vigezo gani vinavyofanana vilivyosababisha mafanikio haya? Utafiti wetu wa ushahidi uliopo unatuongoza kuhitimisha kwamba, kwa mara nyingine, utawala ndio kiini. Ni sekta ya binafsi ambayo kwa kiwango kikubwa ndio husimamia kukua kwa uchumi. Bali hata dola lina jukumu muhimu pia – kwa vile linaweza kujenga mazingira ambamo moyo wa ujasiriamali unaweza kushamiri. Uchambuzi wetu unapendekeza kwamba kuna mambo matatu muhimu ambayo sharti yafanywe na dola. Sharti ijenge mazingira ya uchumi na siasa ambayo yanachochea watu kuwekeza. Sharti iwekeze kwa kiwango kikubwa katika miundombinu, ikiwa ni pamoja na kilimo. Na sharti liwe na mbinu za kushirikisha watu maskini katika ukuaji kwa kuwekeza katika afya na elimu yao, kukabili vyanzo vya ukosefu wa kazi kwa vijana na matumizi madogo ya nguvukazi na kwa kuhimiza biashara ndogo ambayo, muhimu kuliko zote katika Afrika, ni mashamba ya familia.

### Mahali salama pa kuwekeza

Watu wanahitaji kuwa na uhakika wa mambo mengi kujiona salama ili wawekeza fedha zao katika nchi – kwamba kutakuwa na utawala wa kisheria, kwamba mikataba itatekelezwa kisheria, kwamba hayatawekwa masharti ya kibiashara yenye lengo la kuleta misururu ya hongo ya maofisa wala rushwa. Wanahitaji pia sera imara za uchumi, mifumo mizuri ya usimamizi wa fedha za umma, utozaji kodi ulio wazi na sheria thabiti za ushindani. Matakwa haya ni yaleyale kwa wawekezaji wa ndani na nje na katika Afrika, kama ilivyo kwa baadhi ya nchi nyingine zinazoendelea, asilimia 80 ya vitegauchumi ni vya ndani na asilimia 20 ni vya nje. Hatua hizi zinatekelezeka. Katika Tanzania, uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji ndiyo chanzo cha kukua uchumi kwa haraka sana katika miaka 15. Huko Msumbiji, uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji umesababisha kuongezeka maradufu kwa uwekezaji katika sekta binafsi.

Kueneza maendeleo haya kwa bara zima, mpango wa NEPAD umependekeza kuundwa mpango wa Fursa za Uwekezaji (ICF). Kuunga mkono wazo hili hakutagharimu fedha nyingi – jumla ya dola 550 milioni kutoka kwa wafadhili na sekta binafsi kwa miaka saba – bali faida kutokana na uwekezaji huu itakuwa kubwa. Mfuko huu utashughulikia matatizo makubwa katika kufanya biashara, ikiwa ni pamoja na yale yaliyogunduliwa na APRM na hatua nyingine. Utasaidia kuleta na kupanga sera kwa maeneo mengi na kuipa sekta binafsi sauti katika kuamua vipaumbele vya miundombinu mipya.

Moja ya vikwazo vikubwa kwa uwekezaji katika Afrika ni kwamba watu wa nje wanaona Afrika kama nchi moja kubwa ya hatari – mawazo ambayo yanaenezwa na vyombo vya habari na yanatokana na ukosefu wa taarifa sahihi. Bali tunaamini, kutokana na maendeleo ambayo tumeona yakitokea Afrika katika miaka michache iliyopita, na kutokana na yale ambayo makampuni makubwa ya kimataifa yametuambia, ni kwamba mawazo haya si sahihi na yamepitwa na wakati. Wale wanaoifahamu Afrika wana imani ya kuwekeza. Kwa hiyo ICF sharti izingatie mawazo hayo pia. Aidha, nchi zilizoendelea hazina budi kusaidia Wakala Dhamini wa Uwekezaji (MIGA) kuwawekea bima wawekezaji

wa nje na wa ndani katika nchi za Afrika ambazo zimetoka katika migogoro. Litakuwa jambo la manufaa kusaidia pia wawekezaji wa ndani katika nchi za kusini mwa jangwa la Sahara, hatua ambayo itainua uwekezaji kwa kiwango kikubwa.

### Uendelezaji wa miundombinu

Matatizo ya barabara, reli, bandari, nishati, mawasiliano na miundombinu mingine yametajwa na jumuiya za kibiashara na Mawaziri wa Fedha wa Afrika kuwa ni moja ya vikwazo vikubwa kwa ukuaji wa uchumi wa Afrika. Na umwagiliaji mashamba, nishati, ugavi wa maji na usafi ni miongoni mwa vipaumbele kwa watu masikini wa Afrika. Afrika inahitaji kutumia kiasi cha nyongeza cha dola 20 bilioni kwa mwaka kwa uwekezaji na ukarabati wa miundombinu kati ya sasa na mwaka 2015 ili kuendeleza kiwango cha uakuaji cha asilimia saba.

Kama hatua ya kwanza nchi zilizoendelea hazina budi kutoa nyongeza ya dola 10 bilioni kwa mwaka kuinua miundombinu ya Afrika. Na kwa kutegemea matokeo ya matumizi, kiwango hiki sharti kiongezwe tena hadi dola 20 bilioni baada ya mwaka 2010. Fedha hizi zisigharimie miradi ya kifahari ambayo mara nyingi huko nyuma iligeuka kuwa isiyo ya maana bali zitumike katika miundombinu – kuanzia barabara za vijijini na umwagiliaji wa maeneo madogo hadi miradi mikubwa ya nishati ya umeme, bandari na miundombinu ya kikanda. Fedha hizi pia zinapasa kugharimia miundombinu iliyopo. Miradi mikubwa inaweza kuanzishwa na kuwekwa katika ubia na sekta binafsi. Yanahitajika maamuzi sasa kwamba viwango hivi vitimizwe ifikapo mwisho wa mwongo huu.

### Nafasi ya kilimo

Kilimo kinaendelea kuwa sehemu muhimu ya uchumi katika kila nchi ya Afrika. Ni muhimu pia kwa njia nyingine. Kwa kuwa asilimia 80 ya watu wanategemea kilimo kwa mapato yao, ukuaji katika eneo hili utakuwa na athari ya kipekee katika kupunguza umaskini. Na kwa kuwa wanawake huwa na jukumu kubwa katika kilimo, hii itasaidia kukabili hali ya kutokuwa na usawa ambayo inawakabili wanawake na ambayo imekuwa nguvu kubwa ya kuongeza umaskini.

Kilimo ni sekta muhimu kwa Afrika. Ushahidi kutoka duniani kote umeonyesha kwamba ujenzi wa viwanda hufuata kipindi cha kukua kwa kilimo. Lakini kilimo pekee kinaweza kuleta ukuaji halisi na wa muda mrefu kama inavyodhihirishwa na kilimo cha maua na mazao mengine yasiyo ya asili katika Kenya, Uganda na Ethiopia. Bali hivi sasa kilimo kimelenga katika maeneo mawili: kilimo cha mazao ya kujikimu na yale ya kuuza kwa nchi zilizoendelea. Iwapo eneo la tatu litaongezwa – kuzalisha chakula kwa ajili ya sehemu za Afrika ambazo zina upungufu wa chakula wa mara kwa mara – basi kilimo kinaweza kuleta ukuaji katika maeneo ambayo yanatoa chakula kwa ajili hiyo. Hili linaweza kurekebisha hali katika maeneo mawili – pale ambako asilimia 25 ya watu hawapati chakula cha kutosha, na pale ambapo karibu nusu ya nchi za Afrika zenye mazoea ya kukumbwa na upungufu wa chakula. Hii pia inaweza kupunguza haja ya kupata vyakula kutoka nje kwa kiwango cha sasa – chakula cha kununua cha dola 22 bilioni na chakula cha msaada wa dola 1.7 bilioni kwa mwaka 2002. Kutokana na kukua kwa idadi ya watu, masoko ya mazao ya chakula yatakua kwa kasi kubwa zaidi kuliko mazao mengine ya kilimo katika Afrika katika kipindi cha miaka 20 ijayo. Kwa kuzingatia mfumo wa sasa wa matumizi, mahitaji ya ndani ya chakula yatazidi ukuaji wa masoko ya nje.

Kile ambacho mafanikio ya kilimo cha Afrika yanaonyesha ni kwamba hakuna njia moja ya kufungulia ukuaji wa kilimo. Kama ilivyo katika nchi nyingi za Afrika, misaada sharti ije wakati mmoja katika maeneo mengi. Uongezekaji wa uzalishaji hautakuwa wa maana bila kukuza masoko ya kuuza mazao au miundombinu ya kuyasafirisha. Sharti maeneo yanayoingiliana yashughulikiwe hapa, na siyo moja baada ya jingine, bali yote kwa pamoja.

**Umwagiliaji:** Ardhi ambayo inamwagiliwa inazalisha zaidi kuliko ile inayotegemea kilimo cha mvua. Mazao yanayoweza kuzalishwa kwa umwagiliaji ni ya ubora zaidi na mavuno yake hayabadilikibadiliki. Yapo kwa kipindi chote cha mwaka na hayaathiriki kwa urahisi kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa. Na umwagiliaji unaweza kuongezwa bila kuleta hitilafu kwa watumiaji wengine wa maji. Jumuiya ya kimataifa haina budi kuongeza ugharimiaji wa umwagiliaji katika kuunga mkono ongezeko la eneo la umwagiliaji kuwa maradufu ifikapo 2015 kwa kujielekeza kwanza kwenye ugharimiaji wa asilimia 50 ifikapo 2010 na mkazo ukiwa kwenye umwagiliaji wa mashamba madogo.

**Ufikishaji mazao kwenye masoko:** Kiasi cha asimilia 50 ya mavuno hupotea katika sehemu nyingi za Afrika kutokana na wakulima kushindwa kufikisha mazao yao kwenye masoko. Kiwango hiki ni zaidi ya mara mbili ya wastani wa chakula kinachopotea katika nchi nyingine zinazoendelea. Nchi zilizoendelea hazina budi kugharimia ujenzi wa maghala, barabara na miundombinu ya nishati katika sehemu za vijijini katika Afrika. Uwekezaji wa dola 30 hadi 50 milioni kwa kaipindi cha miaka 10 unaweza kuokoa dola 480 milioni kila mwaka kwa zao wa mahindi peke yake.

**Utafiti na uvumbuzi:** Utafiti zaidi ni muhimu sana. Bali sharti ulenge kwa karibu matatizo na mahitaji ya wakulima katika maeneo yao. Tayari kuna njia nyingi na bora na mazao, kama vile mazao chotara, tayari yapo lakini kuna haja ya kufanya kazi zaidi. Katika hili Afrika haina budi kuchagua vipaumbele vyake. Jumuiya ya kimataifa sharti isaidie juhudi za Afrika za kuongeza uchambuzi katika kilimo katika miaka 10 ijayo. Misaada hii haina budi kupitia kwenye mashirika ya utafiti na vyuo vikuu vya Afrika.

**Uuzaji bidhaa ndani ya Afrika:** Mazao kwa ajili ya biashara ya nje hivi sasa yamelenga soko la kimataifa. Haya yanaingiza mapato muhimu ya dola 17 bilioni kila mwaka, wakati soko la ndani la Afrika linaweza kuwa dola 50 bilioni kwa mwaka. Uendelezaji wa masoko ya ndani na yale ya kanda kutaweza kuwapa wazalishaji wadogo na wazalishaji wengine nafasi kubwa ya kuuza vyakula vyao na kuwapa pia nafasi ya kupanuka na kuingia katika kilimo na bishara ya mazao mengine. Hali hii itahitaji usafiri bora wa ndani na taasisi za ndani za kifedha kutoa mikopo kwa wakulima wadogo na watu maskini.

**Hakimiliki ya ardhi na ukodishaji salama:** Kugawa ardhi kwa watu maskini na kuwahakikishia usalama wa miliki kwenye ardhi yao katika sehemu za vijijini na mijini ni muhimu pia katika kuchochea uwekezaji. Urekebishaji wa milki za ardhi katika Afrika ni suala nyeti la kisiasa na, wafadhili wengi wamejitoa kulishughulikia katika miongo ya hivi karibuni. Lakini serikali za Afrika sharti zichukue hatua kuwapa watu maskini, hasa wanawake, ardhi na ulinzi wa hakimiliki zake. Watu wanapokuwa na hati za kumiliki ardhi yao huwa na uhakika wa kuwekeza na wanaweza pia kutumia hatimiliki kama dhamana ya kupatia mikopo.

## Changamoto ya ongezeko la watu mijini

Mbinu yoyote ile ya ukuaji wa uchumi na upunguzaji wa umasikini sharti izingatie kwa makini suala la ukuaji wa miji. Afrika ndilo bara linalokuza miji kuliko yote duniani – karibu mara mbili zaidi ya Amerika ya Kusini na Asia. Katika miaka 25 ijayo, nusu ya idadi ya watu wote wa Afrika watakuwa wanaishi mijini. Afrika inaelekea kwenye viwango vya ukuaji wa miji vya Ulaya – bali haina msingi wa uchumi wa kuiendeleza. Miji haina uwezo wa kujihimili, kwa kuwa ni ukuaji uliokuja kabla ya wakati wake. Hakuna viwanda vya kutoa ajira na watu wengi – karibu asilimia 72 wanaoishi mijini Afrika, wanaishi katika makazi yasipopimwa. Zikiwa wakati wote zinakabiliwa na tishio la kuhamishwa, hali za maisha za kaya kama hizo hufanywa kuwa mbaya zaidi kutokana na ukosefu wa maji na mifumo ya maji taka na huduma nyingine. Karibu wakazi wote wa mjini katika Chad na Ethiopia wanaishi katika makazi yasiopimwa. Miji mikubwa kama Nairobi – ambako karibu watu milioni moja huishi Kibera, kitongoji kikubwa kuliko vyote chenye kusambaza makazi yasiyopimwa – haina maendeleo endelevu kijamii.

Duniani kote, usimamizi wa miji ni jukumu la moja kwa moja la serikali za mitaa. Lakini serikali za mitaa zinashindwa kutokana na utawala dhaifu na ukosefu wa uwezo na raslimali. Mamlaka za miji hazina fedha wala watumishi wenye taaluma kusimamia ukuaji haraka ambao umeleta upungufu wa mamilioni ya nyumba. Viongozi wa Afrika walifanya suala hili kuwa la kipaumbele katika mkutano wa AU uliofanyika Maputo mwaka 2003. Nchi kama Nigeria, Burkina Faso, Uganda na Afrika Kusini zimeanzisha kampeni za kitaifa za utawala mijini. Makubaliano chini ya mpango wa NEPAD kuhusu miji ni kwamba utawala thabiti wa serikali za mitaa, utoaji madaraka kwa watu wengi na idara nyingi kuliko kuwa mikononi mwa mtu mmoja, na mifumo ya ushirikishwaji wa jamii, sasa ni muhimu. Jumuiya ya kimataifa haina budi kuwezesha serikali za Afrika kuweka mipango ya kukabili ukuaji haraka wa miji. Ukuzaji wa uwezo ni muhimu kwa ngazi ya serikali za mitaa ili kuhimiza ugunduzi kama ule wa mpango wa Fursa za Kuboresha Makazi Yasiyopimwa Mijini (SUF) wa shirika la UN la Makazi (UN-HABITAT), ambao utatoa mifumo ya udhamini wa madeni kwa ajili ya uwekezaji katika ujenzi wa nyumba kwa watu maskini wa mijini.

### Mabadiliko ya mazingira na hali ya hewa

Kuna kipengele cha mwisho ambacho ni dhahiri kitakuwa na athari kubwa kwa ukuaji wa uchumi wa Afrika katika siku zijazo. Watu maskini wa Afrika husisitiza kwa makini umuhimu wa mazingira kwa maisha yao. Bali umaskini unaingiliana na matatizo ya mazingira kama vile kuwepo kwa jangwa, uteketezaji wa misitu, upotevu wa bioanuwai, uharibifu wa ardhi na vyanzo vya maji. Usimamizi bora ya mazingira ni muhimu kwa kukabiliana na changamoto hizi. Serikali za Afrika hazina budi kuweka suala la mazingira endelevu katika mikakati yao ya kupunguza umaskini. Na wafadhili hawana budi kuimarisha suala la mazingira katika kazi zao zote katika Afrika, kwa shabaha ya kuunga mkono mpango wa mazingira wa NEPAD.

Mabadiliko ya hali ya hewa ni chanzo cha wasiwasi mkubwa. Hali ya hewa inaendelea kuwa ya kubadilikabadilika katika Afrika. Mvua zinaonekana kunyesha mara nyingi zaidi. Ndiyo maana tumesisitiza sana umwagiliaji. Utabiri wa sasa unaonyesha kuwa huko mbele Afrika itakuwa na ongezeko la joto la nyuzi 0.2 hadi 0.5 centigrade kwa muongo. Afrika inawezekana kuwa kavu katika latitudo za kaskazini na kusini na kuwa na unyevu katika sehemu za tropiki, kukiwa na mabadiliko ya hapa na pale katika kanda na nchi. Mabadiliko ya hali ya hewa na kurudiarudia na kuongezeka kwa hali mbaya ya hewa. Kuongezeka kwa kima cha maji baharini, kumomonyoka kwa fukwe, utapakaaji wa maji ya chumvi nchi kavu na mafuriko vitaleta athari kwa jamii za mwambao na uchumi wao. Huko Tanzania kupanda kwa kima cha maji ya bahari kwa mita 0.5 kutameza zaidi ya kilometa 2,000 za mraba za ardhi. Vitisho kwa uzalishaji katika kilimo, uhakika wa chakula, usalama wa maji na nishati na afya, ambao unatokana na hali ya hewa, vitadhoofisha uwezo wa Afrika wa kuendelea.

Gharama za kutochukua hatua ni kubwa. Gharama za uharibifu wa mazingira katika Ghana zinakadiriwa kuwa asilimia mbili ya mapato ya taifa. Katika mwaka 2000, mafuriko makubwa nchini Msumbiji yaliua watu 700 na kuacha wengine wapatao milioni moja bila makazi – na kufanya ukuaji wa uchumi kushuka kutoka asilimia nane hadi asilimia mbili mwaka huo. Kuja mara kwa mara kwa matukio haya kunaweza kuongezeka sambamba na kukua kwa athari za mabadiliko ya hewa ambavyo kwa pamoja vinaweza kuvuruga Afrika kisiasa. Bila kupunguza joto duniani kwa kiwango kikubwa, ni wazi kwamba maisha ya mamilioni ya Waafrika yatadhoofishwa. Nchi zilizoendelea hazina budi kuweka malengo ya kutumia kikamilifu teknolojia mpya ya nguvu za nyuklia ili kupunguza moshi wa viwanda. Wafadhili hawana budi kutoa kiwango cha dola 100 milioni katika kipindi cha miaka 10 ijayo, kuboresha uchunguzi wa hali ya hewa kupitia Mfumo wa Uchunguzi wa hali ya Hewa Duniani (GCOS) na kujenga uwezo katika taasisi za uchunguzi za Afrika. Wafadhili hawana budi pia kufanya kipengele cha hatari ya ugeugeu na mabadiliko ya hewa kuwa sehemu ya mipango na upimaji utekelezaji wa miradi yao ifikapo 2008 na kutekeleza ahadi zao za kutoa fedha ili kuwezesha nchi za Afrika kujiandaa kukabili hatari za mabadiliko ya hali ya hewa.

### Ushirikishaji watu maskini katika ukuaji

Katika yote haya ukuaji peke yake hautoshi. Mahali ambako hakuna usawa katika mapato, faida kutoka kwenye ukuaji huenda kwa wenye mali. Ukuaji hautaweza kupunguza umaskini hadi hapo watu maskini watakapoweza kushiriki katika ukuaji huo. Na sera za ukuaji sharti zihusishe, na zichukue tahadhari kwamba hazistahili kutenga, watu maskini sana katika fursa za afya, elimu na kazi. Hatua maalum zinaweza kuchukuliwa katika maeneo yafuatayo.

Chanzo kikuu cha ajira katika Afrika ni shughuli ndogo za biashara, mfano mkubwa ukiwa mashamba ya familia. Nyingi ya shughuli hizi huendeshwa nje ya mfumo rasmi wa uchumi. Katika Afrika, uchumi usio rasmi huhusisha shughuli nyingi za kilimo na sehemu kubwa ya shughuli za mijini kama vile usafiri, huduma, stadi mbalimbali hata viwanda vidogo vya uzalishaji.

Mkulima mdogo, mchuuzi wa mitaani, dreva wa teksi, mpiga rangi viatu – watu walio wengi wote huachwa nje ya duara la taarifa, huduma za biashara na hawapewi mikopo. Ni kwa njia hii pia wanawake huwekwa pembeni kwa kuwa wanawake mara nyingi huwa na jukumu kubwa katika biashara isiyo rasmi. Huko Benin wanawake wachuuzi wanafikia asilimia 90 ya watu wote waliomo katika ajira isiyo rasmi.

Biashara nyingi ndogo – nyingi zikihusisha mtu mmoja – mara nyingi hutegemea mifumo ya kifamilia na kijamii kupata mitaji ya kuanzia na kuendelezwa. Katika muongo uliopita, kukua kwa taasisi za kukopesha wafanyabiashara wadogo – Asasi za Mitaji Midogo (MFI) – zikiitwa hivyo kwa kuwa zinajishughulisha na viwango vidogo mno vya fedha visivyovutia mabenki ya biashara – kumesaidia kuhamasisha uwekezaji wa amana na kutoa mikopo ya muda mfupi kwa idadi kubwa ya watu maskini. Taasisi hizi zimeanzishwa kwa wingi na mashirika ya hisani, mashirika ya misaada na mengine yasiyo ya kiserikali. Kukuza mafanikio ya MFI kunahitaji kuhusisha mabenki kwa kuwa yana raslimali kubwa. Bali hivi sasa mabenki mengi yana tabia ya kuogopa hasara na karaha inayoweza kuletwa na biashara hizi ndogo, hivyo yanaacha kutoa misaada kwa kuwa pia viwango vyake vya faida itokanayo na mikopo hiyo ni vidogo mno.

Wafanyabiashara wa nje pia wanaweza kusaidia kwa kutumia vizuri fursa hii. Makampuni ya kimataifa na maduka makubwa katika nchi zilizoendelea hayana budi kutambua kwamba uwajibikaji kijamii wa makampuni hayo siyo kwa ajili ya huruma. Aidha, yachunguze athari za shughuli za biashara yao kwa watu maskini. Kwa kuanzia, sharti wafanyabiashara waweke saini makubaliano ya kanuni kuu za tabia nzuri ya kijamii na kimazingira, ikiwa ni pamoja na yale yanayohusu kuwa na uwazi na kupambana na rushwa. Bali hatua hizi sharti ziwe zaidi ya maneno matupu. Sharti wahakikishe kwamba mifumo yao imerekebishwa ili iendane na matakwa ya wafanyabiashara wa Afrika – ikiwa ni pamoja na kuwalipa mara moja.

Makampuni makubwa ya nje na ndani yanaweza kulea ujuzi wa biashara wa Afrika kwa kulenga wafanyakazi wa ndani ya Afrika na kuwapa nafasi za umeneja, kunasihi mameneja wa biashara ndogo, kuwapa nafasi ya kujifunza biashara na kuwasaida kupata fedha. Serikali wafadhili hazina budi kugharimia juhudi hizi na kukuza ushirikikiano wa aina hii.

Kusaidia katika yote haya nchi zilizoendelea zinahitaji kuanzisha Mfuko wa Kukuza Biashara Afrika (AECF) – wa dola 100 milioni ili kukuza uwezo wa wenye biashara ndogo kupata mikopo na kuwa na kiungo na wenye biashara wengine. Mfuko huu mpya sharti uweke mkazo maalum kwenye kukabili ukosefu wa kazi kwa vijana na matatizo ya kiuchumi ambayo wanawake wanakabiliana nayo. Kukamilisha hili, nchi zilizoendelea hazina budi kutoa dola 20 milioni kwa mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Juhudi Endelevu za Kibiashara (GSB) ili kusaidia makampuni ya nje na ndani kuendeleza miradi ya uwekezaji ambayo ina uwezekano wa kujiendesha na kunufaisha watu maskini.

Hatua hizi juu ya ukuaji na upunguzaji wa umaskini, kama hatua nyingine ambazo tumezijadili, ni sehemu ya mpango thabiti wa mikakati juu ya ukuaji na utawala. Kosa la huko nyuma lilikuwa kufikiri kwamba moja linaweza kutekelezwa bila jingine.

## Biashara zaidi

Biashara imekuwa kiongozi wa ukuaji wa uchumi kwa zaidi ya miaka 50 iliyopita, kwanza katika dunia ya Magharibi na Japan, na baadaye, hivi karibuni huko China na India. Nchi zinazoendelea, hasa za Asia, zimetumia biashara kuingia katika masoko mapya na kubadili sura za uchumi wao; miongo miwili iliyopitta asilimia 70 ya biashara yao ilikuwa katika uuzaji wa malighafi lakini leo asilimia 80 imo katika bidhaa za viwanda.

Bahati mbaya, hali haiko hivyo Afrika. Kwa kulinganisha, miongo mitatu iliyopita imeshuhudia kudorora katika nchi za Afrika, kuanguka katika mgawo wake wa biashara na nchi za nje, ambayo ilishuka kutoka asilimia sita mwaka 1980 hadi asilimia mbili mwaka 2002. Hii imesababishwa, kwa kiwango fulani, na ukweli kwamba idadi na aina ya bidhaa za Afrika kwenda masoko ya nje imeendelea kuwa ileile. Jinsi kanda nyingine zenye ukakamavu na ushindani wa biashara zilivyofanya mabadiliko na kuingia katika utengenezaji wa bidhaa za viwandani, Afrika imeachwa nyuma. Jukumu la kufikia viwango vipya linakuwa gumu kila kukicha.

Uchambuzi wa hili unatueleza kitu cha kufurahisha. Watu wengi hufikiri kwamba matatizo ya Afrika katika biashara hutokana hasa na vikwazo vya kiuchumi vilivyowekwa na nchi tajiri. Ni kweli kwamba vikwazo hivyo havikubaliki hata kidogo. Kisiasa vimepitwa na wakati, kiuchumi ni vya kijinga, kimazingira ni vya kiharibifu na kimaadili havitetewi. Kama tutakavyoonyesha baadaye, sharti vikwazo hivi viondolewe. Lakini – kinyume na kile ambacho kinadhaniwa – kuna sababu nyingine pia, nayo ni hii: Afrika haizalishi bidhaa za kutosha kwa ajili ya biashara, angalau siyo bidhaa sahihi au bora, au za bei sahihi. Iwapo Afrika inahitaji kuendelea, sharti ijishughulishe na masuala haya pamoja na vikwazo vya kiuchumi vinavyoikabili.

Ili biashara iweze kukua, sharti iwe na mazingira kama yale ya uchumi. Bali kuna maeneo mengine matatu ambamo Afrika, kwa kupata msaada kutoka nchi tajiri, haina budi kufanya mabadiliko: uboreshaji miundombinu ya uchukuzi, upunguzaji wa vikwazo vya biashara ndani ya Afrika, na upanuzi wa uchumi wa Afrika kwa kuachana na viwango vya sasa vya kutegemea bidhaa zisizosindikwa.

### Uboreshaji wamiundombinu ya uchukuzi

Afrika inahitaji mfumo wa uchukuzi na mawasiliano ili kufikisha bidhaa zake kwenye masoko. Hili ni eneo muhimu ambalo nchi tajiri zinaweza kusaidia. Kwa sasa gharama na ugumu wa kusafirisha bidhaa Afrika uko juu kuliko ilivyo katika nchi zinazoendelea – ni maradufu. Katika nchi zisizo kwenye mwambao wa bahari gharama za usafirishaji zinaweza kuwa robo tatu ya thamani ya bidhaa zinazosafirishwa; nchini Uganda gharama za usafirishaji zinalingana na asilimia 80 ya kodi kwenye kodi ya nguo zinazosafirishwa nje. Gharama za aina hii hufanya iwe vigumu kupindukia kufikisha bidhaa sokoni kwa bei za ushindani. Na tatizo halipo tu kwenye usafiri wa ardhini. Inagharimu karibu kiasi hichohicho kusafirisha kontena la futi 20 kupitia bandari ya Dakar kama inavyogharimu kusafirisha kontena hilohilo kwa meli kutoka Dakar hadi bandari yoyote Ulaya kaskazini. Hii ndiyo maana uchukuzi ni sehemu muhimu katika fungu la miundombinu ambayo tayari tumependekeza hapo juu.

### Uondoaji vikwazo

Afrika ina vikwazo vingi vya ndani vya biashara ambavyo vinadhuru uwezo wake wa kukua kutoka kwenye umaskini. Hivi ni pamoja na ukiritimba uliopindukia, taratibu za kuchosha za forodha na rushwa inayoendeshwa na watumishi wa serikali kujazia kwenye ujira wao mdogo. Kizuizi cha barabarani katika Afrika ni ishara ya yote haya. Vizuizi, rasmi na visio rasmi, vimejaa katika kila barabara kuu Afrika. Safari ya kutoka Lagos kwenda Abijan ina kizuizi kila baada ya kilometa 14. Huko Cote d'Ivoire, kutoa lori moja upande mmoja wa nchi kwenda upande mwingine hugharimu dola 400 zaidi kwa njia ya kodi na hongo.

Maeneo ya forodha yanahitaji mabadiliko haraka. Afrika ina ucheleweshaji mkubwa wa shughuli ikilinganishwa na wastani wa dunia – wastani wa siku 12. Estonia na Lithuania zinahitaji siku moja kwa ajili ya shughuli za forodha na Ethiopia inahitaji wastani wa siku 30. Taratibu za forodha mara nyingi huwa za kale. Ushughulikiaji wa kawaida huhusisha watu kati ya 20 na 30, hati 40; vipande 200 vya taarifa, ambavyo 30 kati ya hivyo sharti virudiwe angalau mara 30. Ucheleweshaji katika shughuli za forodha za Afrika unaongeza kwa asilimia 10 gharama za usafirishaji bidhaa kwenda nje. Hilo pekee linaleta madhara zaidi kuliko vikwazo vya uchumi vya nchi nyingi tajiri.

Eneo jingine la matatizo ni ukosefu wa biashara kati ya taifa moja na jingine katika Afrika. Asilimia 12 tu ya bidhaa zote za Afrika ndiyo huenda kwa nchi za Afrika. Kuboresha hili, Afrika inahitaji kupunguza vikwazo vya ndani vya uchumi. Hii ina maana ya kupunguza na kurahisisha mifumo ya kodi ya Afrika na hatimaye kuunda maeneo ya biashara huru. Hii ina maana pia ya kupunguza udhibiti na vikwazo vingine kwenye mipaka. Ukubwa wa ekseli za magari makubwa ya mizigo na sheria za uzito wa mizigo kufuatana na ekseli hutofautiana kati ya Botswana, Namibia na Zambia. Na kuna aina tatu za geji za reli katika Afrika.

Serikali nyingi za Afrika zinaogopa kwamba kuondoa vikwazo hivi kutapunguza mapato. Ushuru wa forodha huingiza karibu robo ya mapato ya serikali katika Afrika. Bali uzoefu unaonyesha kwamba inawezekana kupunguza kodi na bado zikaendelea kuwa na mapato. Lesotho iliongeza mapato yake mara tatu zaidi pale ilipoweka viwango vya VAT kuwa sawa na vile vya Afrika Kusini na kuweka taratibu nyingine ambazo zilipunguza magendo na kurahisisha ukusanyi ushuru mpakani.

Serikali za Afrika, kwa miongo kadhaa, zimekuwa zikishinikiza nchi tajiri kuondoa vikwazo vya kiuchumi lakini zenyewe zingefanya vizuri zaidi kwa kupunguza vizuizi vya ndani vya uchumi. Kwani vikwazo vingi ni rahisi kuviondoa; inaweza kufanywa na nchi mojamoja. Hiki kinapaswa kuwa kipaumbele kisichobishaniwa katika Afrika. Urekebishaji wa huduma za forodha katika Msumbiji na ugeuzaji wa bandari ya Dar es Salaam kuwa ya viwango vya kimataifa vya ufanisi, unaonyesha kinachowezekana kufanyika. Katika Msumbiji, bidhaa zinapakuliwa kwa kasi ya mara 40 kuliko ilivyokuwa kabla ya mageuzi na mapato ya forodha yameongezeka kwa silimia 38 katika miaka miwili ya kwanza. Serikali za Afrika sharti zifanye mageuzi katika eneo hili kuwa ya kipaumbele cha juu mno.

Wafadhili hawana budi kugharimia hatua za serikali za Afrika za kuondoa kodi za ndani katika bidhaa na vikwazo vingine vya kisheria. Hawana budi kusaidia mageuzi katika maeneo ya forodha na uendeshaji wa bandari. Hili halitahitaji msaada mkubwa wa wafadhili, bali litakuwa na matokeo kubwa kiuchumi.

### Upunguzaji wa utegemezi kwenye bidhaa ambazo hazijasindikwa

Hatua kubwa na pekee ambayo Afrika inaweza kuchukua kupunguza utegemezi wake kwa malighafi, ni kusaidia makampuni makubwa na mashamba ya kifamilia kuingia katika utengenezaji wa bidhaa mpya na katika shughuli nyingine mpya. Msaada mkubwa kutoka nchi za G8 na zile za EU katika kujenga miundombinu, kama ilivyoelezwa mapema, ni muhimu katika kujenga uwezo kibiashara, bali sharti zisaidie pia Afrika kukuza uwezo wa

kusindika mazao yao ya kilimo na kuongeza tija na ubora wa malighafi. Hawana budi kugharimia ukuzaji wa taasisi na asasi za kusaidia wakulima wadogo kuuza mazao yao. Supamaketi zinaweza kufanya iwe rahisi kwa wakulima kuuza bidhaa zao katika maduka hayo ya vyakula.

## Biashara ya haki zaidi

Sehemu muhimu ya kiapo cha uaminifu cha madaktari wanapokuwa wanahitimu inasema, "Kwanza usidhuru mtu." Kanuni hii haina budi kutumika pia katika jukumu ambalo nchi tajiri zinalo kwa Afrika.Uhusiano wa kibiashara kati ya nchi zinazoendelea na dunia iliyoendelea umetawaliwa zaidi na mfumo changamani wa sheria, kodi, ushuru na viwango vya mauzo – vyote vikipendelea, kwa kiwango kikubwa, biashara ya kimataifa kwa manufaa ya nchi tajiri. Pamoja na kusaidia kukuza uwezo wa Afrika wa kushindana kibiashara, nchi za G8 na EU hazina budi kushindana kwa njia za haki zaidi. Kuna maeneo makuu matatu ambako nchi zilizoendelea zinaweza kufanya bora zaidi. Wafikie makubaliano kwenye mazungumzo ya Doha ambayo hakika yatasaidia maendeleo. Wanapaswa kufanya 'upendeleo wao kibiashara' wa sasa uwe bora zaidi. Na hawana budi kutoa fedha taslimu kusaidia nchi za Afrika kujirekebisha kwa ajili ya fursa mpya za kiuchumi.

Kilimo ndiyo shughuli ambayo Waafrika wengi maskini wanategemea kwa uhai wao. Kwa kulinganisha, kilimo hakina umuhimu mkubwa kiuchumi katika nchi zilizoendelea sana ambako kinaingiza asilimia kidogo ya mapato ya taifa au chini zaidi. Lakini sekta za kilimo za nchi nyingi za G8 na EU ndizo zinalundikiwa ruzuku na kulindwa katika uchumi wa nchi tajiri zenye viwanda. Nchi tajiri hutumia dola 350 bilioni kwa mwaka katika kulinda kilimo na ruzuku – ambayo ni mara 16 ya misaada wanayotoa kwa Afrika. EU hutoa asilimia 35, Marekani asilimia 27 na Japan asilimia 22.

Sera hizi zina madhara kwa nchi masikini na nchi tajiri. Walipa kodi na walaji hulipa pesa nyingi kusaidia wakulima wao – ingawa, kusema kweli, si wakulima wadogo wa EU na Marekani ambao wananufaika: wao hupata asilimia nne tu ya ruzuku na zaidi ya asilimia 70 zikienda kwa asilimia 25 ya wakulima matajiri, wanaomiliki ardhi na makampuni makubwa ya kilimo. Matokeo yake ni kwamba EU inatoa ruzuku ya viwango vikubwa kwa ajili ya kuzalisha viazisukari, kiasi kwamba vinazalishwa katika maeneo ya Ulaya ambayo hayafai kiuchumi wa kiufanisi. Na huko Marekani, ruzuku kwa wakulima 25,000 tu wa pamba, ambao wanalipwa mara mbili ya bei ya soko la dunia, wanatishia uhai wa watu zaidi ya milioni 10 wa Afrika Magharibi ambao huzalisha zao hilo kwa theluthi moja ya bei hiyo.

Marekebisho ya sera ya kilimo ya EU ni muhimu, kama ilivyo kwa sera za Marekani na Japan za kujihami na kutoa ruzuku. Kuna njia nyingi nyingine kwa nchi tajiri kutumia haki zao kusaidia maeneo ya mashambani, kama vile msaada wa moja kwa moja wa mapato kwa wakulima na uwekezaji katika maendeleo ya shamba na katika mazingira. Ulinzi wa shughuli za mashambani unaoangamiza uhai wa mamilioni ya watu maskini wa Afrika, ni kosa ambalo kimaadili halisameheki.

Hatua ya kurekebisha hali hizi zisizo na urari kibiashara sharti ichukuliwe katika maeneo yafuatayo:

### Kuondoa ushuru

Nchi zinazoendelea zinakabiliwa na vikwazo vya fedha katika masoko ya nchi zilizoendelea. Kilimo ndio sekta muhimu kwa bidhaa za kuuza nje, kwa kiwango kikubwa, kwa watu maskini wa Afrika. Bali pamoja na kujua hivyo, Ulaya inaweka kodi kwenye mazao ya kilimo ambayo ni mara tatu au nne zaidi ya ushuru wa bidhaa zake za viwandani, na hata juu zaidi katika bidhaa ambazo Afrika inazihitaji zaidi. Ni muhimu kwamba nchi tajiri ziache ubaguzi dhidi ya bidhaa ambazo Afrika inajisikia kuwa na faida zaidi. Nchi za G8 na EU

sharti ziongeze kasi katika kuvunja vikwazo vya kiuchumi ili kuipa Afrika fursa ya kupanua uuzaji wa bidhaa zake nje – kwa kupunguza hatua kwa hatua ushuru kwa bidhaa hadi utakapotokomezwa kabisa ifikapo 2015. Hiki ndicho kinapaswa kuwa kipaumbele cha kwanza kwenye mazungumzo ya WTO huko Doha.

Na kuna vikwazo vipya pia, kwa mfano viwango vya afya na usalama, ambako misaada inahitajika vilevile. Kama EU ingetumia viwango vya kimataifa vya dawa za kuua wadudu kwenye migomba, badala ya kutumia viwango vyake, biashara ya nje ya Afrika ingekua kwa dola 410 milioni. Nchi za G8 na EU zinapotengeneza na kuweka viwango sharti zitumie vigezo vya kimaendeleo ili kuzuia kuleta uharibifu kimaendeleo kwa ajili ya mapato kidogo. Nchi tajiri hazina budi kuiwezesha Afrika kifedha ili iweze kufikia viwango hivi.

### Uondoaji wa ruzuku

Nchi tajiri sharti pia ziache kutoa ruzuku kwa wakulima wao ili wazalishe hata chakula kisichohitajika na kwa kufanya hivyo kudhoofisha bei za dunia, na hatimaye kutupa ziada zao kwenye masoko ya Afrika. Wakati Mawaziri wa Biashara watakapokutana, Hong Kong, Desemba mwaka huu, nchi za G8 na aaeu sharti zifungamane pamoja katika suala la kumaliza ruzuku kwa bidhaa za kuuza nje na kuondosha misaada inayovuruga biashara ifikapo 2010. Kwa kuanzia, misaada inayovuruga biashara ya pamba na sukari sharti iondolewe mara moja. Kwa kufanya hivi na kwa kuondoa ushuru, watapunguza matumizi makubwa yasiyo ya lazima na kutoa faida kubwa kwa watu wao na kwa Afrika na nchi nyingine zinazoendelea. Mageuzi haya yanaweza kuleta ushindi kwa kila mmoja. Fedha zinazookolewa zinaweza kupelekwa kwenye mahitaji ya maendeleo na mazingira katika nchi tajiri na kuongeza misaada kwa Afrika.

### Maendeleo kwenye Upendeleo

Kinyume na imani iliyoenea kwamba Afrika imefungiwa kabisa masoko ya nchi tajiri, bara lina njia za kufikia masoko ya nchi zilizoendelea kupitia mifumo kadhaa ya 'upendeleo' – mifumo ambayo inafanya nchi zenye mapato ya juu kutoa nafasi ya masoko yao kwa bidhaa za nchi zinazoendelea.

Bali upendeleo huu hauleti manufaa yaliyotarajiwa. Mara nyingi ni ya muda tu na yenye ugumu usio wa lazima (kwani kutekeleza matakwa yao kunaweza kugharimu hadi asilimia 10 ya thamani ya bidhaa zinazoingia katika mpango huu). Wengine wana masharti ambayo yanatumika kwa makusudi ya kuzuia biashara: 'Masharti ya mahali zitokako bidhaa,' yakilenga kuthibitisha iwapo kweli bidhaa kutoka nchi maskini sana za Afrika zilitengenezwa huko, yanatumiwa kipuuzi mno hadi kufikia kiwango cha kuamua, kwa mfano, kwamba samaki hawa hawafai iwapo walivuliwa na mtumbwi uliotengenezwa Ghana lakini mwenye chombo hicho ni wa Afrika Kusini. Mfumo wa Marekani umekuwa wa manufaa zaidi kwa baadhi ya nchi za Afrika katika sekta ya nguo. Inaruhusu nchi maskini sana za Afrika kuingiza nguo hata kama zimetengenezwa kutokana na vitambaa vilivyotengenezwa nchi nyingine. Hadhi ya 'mahali' bidhaa inakotoka inatumika tu kwenye bidhaa za kuunda. Hatua hii imeleta nafasi 40,000 za kazi katika viwanda vya nguo nchini Lesotho.

Nchi za G8 na EU, kama hatua ya kwanza, sharti zipanue mpango wake ili uzifikie nchi zenye mapato ya chini katika Afrika ili nchi maskini kama Ghana, Cote d'Ivoire na Kenya zihusishwe. Zinapaswa kutumia masharti ya mahali zitokako bidhaa kuruhusu nchi kutafuta pembejeo kwa ushindani kutoka kokote kule duniani na kuzitaka nchi ziongeze asilimia 10 ya thamani katika viwanda vyao vya utengenezaji na usindikaji.

Kuwezesha mipango hii kufanikiwa kunaweza kukuza mapato ya Afrika kwa dola 5 bilioni kwa mwaka na kuongeza kiwango cha ukuaji kwa bara zima cha asilimia moja.

## Jinsi ya kusaidia kuleta mabadiliko

Upendeleo hauwezi kuwa mfumo wa kudumu. Hatimaye sharti Afrika ijiandae kwa ajili ya mashindano na nchi nyingine duniani. Kufanya maandalizi hayo ni suala la polepole ambalo linahusu mazungumzo ya Doha ya WTO. Lakini mabadilko hayo yanahusisha gharama. Nchi tajiri hazina budi kugharimia mabadiliko haya na taratibu za marekebisho. Hii ina maana kwamba kusaidia watu maskini kunufaika na fursa mpya zilizopatikana, na kusaidia wale ambao mapato yao yanaweza kupungua; kuunga mkono serikali kukabili hasara katika biashara na mapato ya kodi; kukabili makali ya bei za juu za vyakula kwa nchi zinazoagiza chakula kutoka nje; na kusaidia nchi kukabiliana na hasara zitokanazo na upendeleo ambao thamani yake inapungua wakati vikwazo vya kibiashara vya nchi tajiri vinapoondolewa.

## Kinachotegemewa kutoka Doha

Mwisho – na labda muhimu zaidi – kile ambacho Afrika inahitaji ni makubaliano makuu yatokanayo na mazumgumzo ya WTO ya Doha kabla ya mwisho wa mwaka 2006. Hayo hayawezi kuwepo mpaka nchi tajiri zikubaliane kupunguza kwa kiwango kikubwa ruzuku wanayotoa kwa kilimo. Hilo haliwezi kutokea bila kuondolewa kwa vikwazo vya kiuchumi vya nchi tajiri. Haliwezi kutokea bila kutupilia mbali mawazo kwamba nchi maskini nazo sharti zitekeleze yale ambayo nazo zinadai kutoka kwa nchi tajiri: huu sio uwanja linganifu kwa washiriki wote. Aidha, urekebishaji uchumi haupaswi kufanywa kuwa sharti la kibiashara au mazungumzo ya kupata misaada. Nchi binafsi za Afrika sharti ziruhusiwe kuweka mipangilio yao ya kiuchumi kulingana na mipango yao ya upunguzaji umaskini na maendeleo, na siyo kulazimishwa kufungua masoko yao kwa bidhaa kutoka nje kwa njia ambayo inahujumu viwanda vyao vichanga. WTO hutoa 'upendeleo maalum' kwa nchi zinazoendelea lakini huu sharti utumiwe vizuri ili kufikia malengo tuliyoeleza hapo juu. Na nchi tajiri sharti zitoe misaada zaidi yenye kusaidia Afrika kujirekebisha kwa masoko yaliyo wazi zaidi.

Makubaliano yoyote yatakayopatikana Doha sharti yaruhusu kuendelea kwa mabadiliko kwa kasi ambayo imekubaliwa na Afrika, na siyo inayong'ang'anizwa kwake. Mijadala sharti ichukue sura ya uwazi zaidi na mfumo shirikishi wa maamuzi kuliko tabia ya kawaida ya mazungumzo ya WTO. Aidha, sharti ihakikishwe kwamba serikali za Afrika zenye wafanyakazi wachache zinaweza kupata haki pale zinapohusishwa katika majadiliano ya biashara yenye kanuni ngumu na changamani ambapo nchi tajiri kuwa na wawakilishi wengi na wanasheria wanaolipwa viwango vikubwa.

Wakati Doha ni mchakato wa kimataifa, hatua za kati ya nchi na nchi – kwa mfano makubaliano ya biashara huru kati ya Marekani au EU, na Afrika – zinaweza kuleta madhara kwa kuingiza masharti zaidi. EU inapaswa kuhakikisha kwamba Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi (EPA) ambao inajadiliana na Afrika hivi sasa umeelekezwa kwenye maendeleo, ukiongozwa na misingi ambayo tunatoa wito itumike katika mazungumzo ya Doha – na kuzipa bidhaa za Afrika nafasi kwenye masoko ya EU bila umoja huo kudai kupata fursa kama hiyo kutoka Afrika; na kutoa misaada ambayo ni muhimu katika kuongeza uwezo wa Afrika wa kufanya biashara. Majadiliano kama hayo sharti yazingatie kikamilifu athari za umaskini.

Sera zote hizi – kukuza fursa ya kufanya biashara, na kuondolewa kwa vikwazo kwa biashara – sharti zitekelezwe kwa pamoja. Tunaelewa hii ni ajenda ya malengo makuu bali tunaamini kuwa inawezekana kutekelezeka. Chochote pungufu ya haya hakitaipa Afrika fursa inayohitaji kukuza biashara katika bidhaa za asili na bidhaa mpya. Hili pia halistahili kutengwa na mapendekezo mengine ya Tume hii. Afrika haitaweza kutoka nje ya duara hili la maangamizi kwa ufumbuzi nusunusu wa jambo mojamoja na sera zisizoshikamana.

## Fedha zitatoka wapi?

Unapokabiliwa na tatizo kubwa, Albert Einstein aliwahi kusema, sharti ubadili kabisa mtizamo wako kiakili. Mambo yaleyale kila wakati hayawezi kukufikisha popote. Inabidi uelekeze fikra zako katika ngazi tofauti.

Hivyo ni kweli pia kuhusu Afrika na swala la jinsi dunia inavyoweza kugharimia mabadiliko yanayohitajika. Matatizo tunayoyashughulikia ni makubwa. Ni matokeo ya miongo mitatu ya kukwama. Kukubaliana juu ya hatua nyingine zaidi za nyongeza kwenye yale tuliyokwishayafanya hakutatupeleka kokote. Mabadiliko yanahitaji upigaji wa hatua kubwa. Hii ndiyo sababu tunapendekeza uongezaji mara mbili wa misaada kwa Afrika katika kipindi cha miaka mitatu hadi mitano ijayo.

Hizo ni fedha nyingi. Lakini huu siyo wakati wa kuwa na woga. Tekeleza mipango hii kikamilifu, na katika miongo miwili, tutakuwa na Afrika yenye nguvu na inayokua, ambapo misaada inayohitajika itaendelea kupungua kama ilivyotokea huko Asia. Ila tukifanya makosa katika hili, watoto wengi wa Afrika watakumbwa na maisha dhalili kama walivyo mama na baba zao – na mambo kwa kweli yatazidi kuwa mabaya.

Mabadiliko matatu ni ya lazima sasa: kuendelea kuboresha utawala katika Afrika, ongezeko kubwa la misaada kutika jumuiya ya kimataifa, na mabadiliko muhimu katika jinsi wafadhili wanavyofanya shughuli zao barani Afrika.

Tunakadiria kwamba programu kubwa ya mabadiliko ambayo tumefafanua – katika utawala, uwekezaji na matumizi ya jamii – itagharimu nyongeza ya dola 75 bilioni kwa mwaka. Hakuna uwezekano wa Afrika kugharimia hili peke yake. Kwa sasa Waafrika wanalipa kodi zinazolingana au kuzidi mapato yao kama raia wa nchi nyingine zenye mapato ya chini. Lakini hii haiwezi ikatosha kuiondoa Afrika kwenye mkwamo huu. Hivyo ni vipi tutagharimia uwekezaji na matumizi zaidi yanayohitajika?

Tunachopendekeza ni njia yenye hatua mbili: Kwanza tunapendekeza kwamba serikali za Afrika na wafadhili, katika kipindi cha miaka mitatu hadi mitano ijayo, wafikie nusu ya kile kinachopendekezwa. Hiyo itakuwa na maana kwamba theluthi ya raslimali zinazohitajika (kiasi cha dola 12.5 bilioni) zitakuwa zimetolewa na Afrika kwa njia ya ongezeko la kodi inayotokana na ukuaji wa ziada. Theluthi mbili za raslimali (dola 25 bilioni) zitatokana na ongezeko la misaada. Kisha maendeleo yapitiwe. Kutegemea maboresho katika uwezo wa usimamizi na uendeshaji wa serikali za Afrika, na maboresho katika namna misaada inavyotolewa, tutapendekeza ongezeko jingine la misaada la dola 25 billioni kwa mwaka. Afrika inaweza kutafuta mchango wa nyongeza kwa kushawishi vyanzo vingine vya fedha ikiwa ni pamoja na amana za ndani, uwekezaji wa ndani na nje na kwa njia ya matumizi ya fedha za umma kwa makini na kwa uwazi.

Halitakuwa jambo la busara kujaribu kutoa fedha za nyongeza za msaada kwa kasi zaidi ya hii, kwa sababu, kama tutakavyoeleza hivi karibuni, hivi sasa Afrika haina uwezo wa kusimamia misaada kwa uthabiti – ingawa ni muhimu kutosisitiza sana suala hili. Njia hii ya hatua mbili ni halisi lakini pia inatekelezeka. Chochote chini ya hapo hakitaupa uchumi wa Afrika msukumo unaohitajika.

Wanaweza kuwepo wale wanaouliza iwapo misaada ni ufumbuzi sahihi. Kwa hakika Afrika inaweza na ingefaa ilipe sehemu ya nyongeza inayohitajika katika matumizi. Lakini viwango vinavyohitajika ili kufanikisha hatua za lazima za kuleta mabadiliko ni vya hamna kwamba sehemu kubwa itabidi itoke kwa nchi tajiri. Misaada ndiyo chanzo kinachoaminika cha fedha hizi. Na kiasi cha dola 25 bilioni zinazohitajika katika hatua ya kwanza, cha fedha hizi kwa vyovyote vile ni ziada kwa ya asilimia 0.1 ya mapato ya nchi tajiri; – yaani senti 10 kwa kila dola za Kimarekani 100.

**Je, misaada inaweza kukidhi haja?**

maafa ya asili – ukame na mafuriko, kushuka ghafla kwa bei za bidhaa zinazouzwa nje ambako kunaweza kuletwa, kwa kiwango fulani, na mfumo wa biashara duniani usio linganifu; mambo ambavyo yanaweza kuvuruga uchumi na kupunguza mapato ya taifa kwa hadi viwango vya asilimia 3.

### Ni kiasi gani cha misaada ambacho Afrika inaweza kutumia vizuri?

Kuna suala jingine muhimu sana. Licha ya mahitaji makubwa ya Afrika, kuna kikomo kwa idadi ya barabara, mabwawa, shule na kliniki zinazoweza kujengwa na kuhudumiwa ipasavyo katika mwaka mmoja wowote. Afrika inao tu wataalamu wengi wa kiufundi na mameneja wa kupanga, kutengeneza bajeti na kujenga. Kuna vipengele vingine vya kiuchumi mtandao/jumla, kitaasisi, kimaumbile, kibinadamu, kijamii, kiutamaduni na kisiasa – ambavyo huweka ukomo wa kiwango cha misaada ambacho Afrika inaweza kuchukua na kutumia kikamilifu na kwa mara moja. Njia fupi ambayo wanauchumi hutumia kuelezea hili ni 'uwezo wa kuhimili.' Hakuna uchambuzi wowote wa misaada unaweza kupuuza tatizo hili na Tume imelichunguza kwa makini sana.

Uwezo wa kuhimili hutegemea mambo mawili makuu: Utawala katika Afrika na ubora wa misaada kutoka nchi tajiri. Nchi wafadhili hazina budi, kama tulivyosema, kuunga mkono mabadiliko katika utawala na kwenda haraka katika kukuza ubora wa misaada. Ushahidi tulio nao unaonyesha kwamba utawala katika Afrika umeboreshwa, kama ilivyo kwa misaada, kwa kiwango kwamba dola 25 milioni za nyongeza zinaweza kutumiwa ipasavyo. Na iwapo mkondo huu utaendelea na msaada kutoka nje ukatimilika, miaka mitano kutoka sasa Afrika itakuwa na uwezo wa kupokea na kutumia nyongeza nyingine ya kiwango hicho.

### Je, nyongeza ya misaada ni ya kudumu?

Kuna wale wanaofikiri kwamba misaada siku zote husababisha utegemezi. Hili huwa pale tu ambako ukuaji wa uchumi hautokei. Ukuaji unapokuja, misaada inatoweka. Hii imetokea duniani kote. Kwa mfano, Korea imetoka kwenye kuwa mpokeaji wa misaada katika miaka ya 1960 na kuwa mmoja wa watoa misaada katika miaka ya 1990.

Hii imetokea Afrika pia ambako, kama tulivyoona, Botswana imebadilishwa kutoka moja ya nchi zinazotegemea zaidi misaada na kuwa nchi ya mapato ya kati na isiyohitaji viwango vikubwa vya misaada kutoka nje. Wafadhili wameanza kuondoa ugharimiaji hatua kwa hatua. Botswana imefanya haya kupitia uongozi imara wa kisiasa na menejimenti thabiti (ikiwa ni pamoja na katika sekta ya misaada ambako serikali iliweza kukataa misaada ambayo haikulingana na sera na aula zake). Idadi ya watu ambao wanaishi katika umasikini uliokithiri imepungua kwa kiwango kikubwa. Kwa kiwango cha juu cha ukuaji wa uchumi, Botswana inathibitisha kwamba haja ya misaada inatoweka taratibu.

### Madeni, je?

Kile ambacho Afrika haitaki ni misaada hasi – ambayo ndiyo hasa mikopo inayoikamua kwa njia ya riba. Jumla ya deni la nje la nchi za Afrika kusini mwa Sahara lilifikia dola 185 bilioni mwaka 2003. Mzigo huo unaning'inia kama kirukizi kwenye mwili wa kila mwanamme anayelima shambani kwake; kila mwanamke aliyebeba mtungi wa maji akitoka kisimani; na kila mtoto ambaye hawezi kwenda shule. Kwa mzigo huu wa madeni, maendeleo yanazunguka kasi. Nchi zenye viwango vya juu vya madeni mara nyingi zina viwango vya chini vya ukuaji wa uchumi.

Sehemu kubwa ya deni la Afrika, kwa kuzingatia hali ya sasa ya uchumi wake, haiwezi kulipwa. Jumuiya ya kimataifa imewahi kukubaliana na hili katika miaka ya nyuma na kuweka programu za kupunguza madeni. Wakati umefika kwa nchi zilizoendelea

kukubaliana na ukweli huu kwamba pale ambapo madeni hayawezi kulipwa, "unafuu wa madeni" unamwondolea mdau njozi katika mizania. Na madeni yanaendeleza hali yanawa katisha tamaa, wawekezaji binafsi na kuongeza viwango vya uhamishwaji wa mtaji kutoka nchi za Afrika.

Zaidi ya hayo, maamuzi juu ya upunguzaji madeni yamefanywa kwa kuzingatia uwezo wa nchi wa kulipa madeni na bado ikaendelea kuwa na uchumi endelevu. Hili halikuwa na uhusiano na hali halisi: kwani ni nchi nne tu zilizofaulu kufikia viwango vya ulipaji madeni kwa mujibu wa vigezo finyu vya mpango kwa ajili ya Nchi Zenye Madeni Makubwa (HIPC). Maamuzi juu ya unafuu wa madeni sharti yafanywe kwa mujibu wa vigezo vya upunguzaji umasikini ambavyo vinatumika kufanya maamuzi ya kutoa misaada – hivi ni iwapo misaada itatumika vizuri kuinua mambo mawili ambayo ni ukuaji wa uchumi na ushirikishwaji wa watu masikini katika kukua huko – mambo ambayo yanapunguza umasikini.

Kwa nchi masikini zilizo kusini mwa jangwa la Sahara ambazo zinahitaji kufutiwa madeni, sharti shabaha iwe kuyafuta kwa asilimia 100 na mapema iwezekanavyo. Hii sharti iwe sehemu ya mpango wa jumla kwa nchi hizi ili kufikia Lengo la Maendeleo la Milenia kama ilivyoahidiwa huko Monterrey na Kananaskis. Kigezo kikubwa kinastahili kuwa, kwamba fedha zitumike kuleta maendeleo, kukuza uchumi na kupunguza umasikini katika nchi ambazo zina juhudi ya kuendeleza utawala bora. Vilevile kazi ianze mara moja ya kuunda mfuko wa wazi wa madeni yakiwemo yale ya nchi zote zenye mapato madogo za kusini mwa jangwa la Sahara, na zote ambazo hazimo kwenye mipango ya sasa. Mfuko sharti ufute malimbikizo ya madeni na riba kwa asilimia 100, na kuhusisha madeni kutoka mashirika ya fedha ya kimataifa na yale ya kati ya nchi na nchi. Kama hatua ya haraka, sharti fedha zitolewe mara moja ili kuwezesha kufuta kwa asilimia 100 ya riba ya madeni ya kimataifa, pale ambapo hili ni sharti la kufikia Lengo la Maendeleo la Milenia.

Mwisho, masharti nafuu ya madeni sharti yakome mwaka 2015 ili kuondoa matumaini kwamba mikopo mipya inayochukuliwa sasa nayo itafutwa.

### Jinsi ya kupata fedha

Kuna njia mbalimbali ambamo nyongeza za misaada zinaweza kupatikana. Nchi kadhaa zimeahidi kufikia kiwango cha UN cha kutoa asilimia 0.7 ya mapato yao ya taifa katika misaada. Nchi nyingine za G8 na EU hazina budi sasa kufuata mfano huu na kutangaza ratiba ya kufikia lengo la asilimia 0.7. Katika bajeti hizi za misaada, hasa katika muktadha wa uwezekano wa ongezeko la dola 50 bilioni katika misaada, kuna hoja muhimu ya kugawa fedha upya ili kidogo ziende kwa nchi zenye "mapato ya kati" na nyingi ziende kwa nchi masikini, hasa Afrika, ambalo ndilo eneo duniani ambalo halikui.

Lakini hii haitatosha. Kutoa viwango muhimu ambavyo vitaipa Afrika msukumo inaotaka, kutahitaji misaada mingi. Uwekezaji katika elimu ya watoto, katika kukuza viwango vya afya, katika miundombinu, katika kuboresha utawala na katika kujenga mazingira yanayoshawishi watu kuwekeza katika uzalishaji wa ajira mpya, hakika ni mzuri kwa watu masikini wa Afrika leo. Lakini uwekezaji wa aina hiyo pia unajenga misingi imara kwa ukuaji wa uchumi katika siku za mbele. Na hatua zote hizi zinakuza matumaini ya mafanikio ya kila mmoja. Yakitekelezwa kwa pamoja yanaweza kuleta hali iliyo kinyume kabisa cha duara la maangamizi – ubora wa maisha. Lakini yakifanywa kuwa matengano na kwa juhudi ndogondogo, kwa kipindi kirefu, yatakosa athari za kuimarishana kwa hatua zinazochukuliwa pamoja. Hii ndiyo maana ni muhimu kuchukua fedha za misaada zinazoahidiwa kwa ajili ya muongo ujao na kutumia sehemu yake kubwa mapema. Bila kufanya hivyo itakuwa ni kushindwa kujifunza kutokana na yaliyopita.

Utumiaji wa misaada mapema siyo tu kwamba ni sahihi katika misingi ya kibinadamu – unakabiliana na umasikini wa leo – na unaleta maana kiuchumi. Uwekezaji wa misaada

zaidi sasa utaleta mafao makubwa kwenye uwekezaji wa jumla. Nchi za G8 na EU hazina budi kutekeleza ahadi zao za misaada sasa ili kiasi muhimu/kikubwa cha fedha hizo kiweze kutumika hivi punde. Hazina budi sasa kuweka awamu za kuongeza maradufu misaada kwa Afrika. Hii sharti igharimiwe kupitia uanzishwaji haraka wa mfuko wa Fursa za Fedha Kimataifa (IFF). Chini ya mfuko huu, wafadhili watatoa ahadi za kutoa misaada ya muda mrefu na zenye kuwabana kisheria; na kwa kutumia ahadi hizo kama dhamana, IFF itatafuta fedha kutoka masoko ya mitaji ya kimataifa kwa kutoa dhamana ambazo zitalipwa kutokana na fedha ambazo wafadhili watalipa hapo baadaye. IFF haitahitaji nyongeza kwenye bajeti za misaada kutoka serikali wafadhili; huwa wamekitwa kwenye ahadi za misaada ya nyongeza kwa siku za baadaye ambazo nchi hizo zimetoa, hasa zile

ajetna abu. Mfanofuidushurefwika ghadi kwenytatajeti zndegaye amsokahiowenzishwe kuzo

Njia bora ya kutoa misaada hiyo ni kuiweka katika bajeti za serikali za Afrika na kuziacha serikali ziweke vipaumbele ambako itatumika. Msaada huu wa moja kwa moja kwenye bajeti unahakikisha kwamba misaada inaingia kwenye aula za maendeleo ambazo zimekubaliwa kiserikali. Aidha, hufanya gharama za nyongeza za uhakiki na utoaji taarifa kubaki mdogo. Misaada haina budi kuwa ya kutabirika na ya muda mrefu, ingawa sharti pawepo maelezo ya kipi kifanyike pale hali ya ndani itakapobadilika ghafla.

Bali hili linaweza kufanyika pale ambapo serikali ina mkakati wazi wa maendeleo na ambapo mfumo wa bajeti ni wazi na unaohakikika. Pale ambako hali ni tofauti na hapa, njia ya kutumia sekta kwa eneo maalumu kama elimu na afya inaweza kuwa ya manufaa. Na pale ambapo utawala unalegalega kiasi kwamba wafadhili hawana imani katika mfumo wa sekta, basi misaada inaweza kupelekwa kwenye miradi mahsusi inayoendeshwa na mashirika au asasi zisizokuwa za kiserikali. Utoaji misaada kwa miradi kwa njia hii kunaweza kuleta mabadiliko kwa ngazi ya chini/msingi, lakini kwa ufafanuzi hakuwezi kusaidia kujenga uwezo ndani ya serikali ambao ni muhimu kwa maendeleo ya muda mrefu. Hii ndiyo maana tunahimiza wafadhili kwenda kwa mkondo wa kusaidia njia za miradi na sekta, na kutoka hapa moja kwa moja hadi katika kusaidia bajeti. Wafadhili hawana budi kuhakikisha kwamba miradi haiendi kinyume na maendeleo ya serikali za Afrika na vipaumbele vya bajeti. Aidha, hawapaswi kudhoofisha juhudi za Afrika za kukuza uwezo wa wizara za serikali zao.

Mashirika yanayoendesha shughuli katika nchi za Afrika yanahitaji misaada pia. Jumuiya zake za kanda za kiuchumi zina uwezekano mkubwa wa kukua zikiwa mihimili ya UA – bali bado ni dhaifu na mara nyingi zinavurugika kuzingatia maendeleo ya muda mrefu kutoka kwenye kashifa au migogoro. Nayo yanahitaji misaada ya jumuiya ya kimataifa kama ilivyo kwa UA na mpango wake wa NEPAD, Tume ya Uchumi ya Afrika (ECA) na ADB ambavyo wanahisa wake hawana budi kuhakikisha kwamba inajenga dira na inachukua hatua ya kuwa asasi kubwa inayotoa fedha Afrika. Ni mashirika kama haya hujenga “ajenda ya mabadiliko” ndiyo tumaini jipya la Afrika.

Benki ya dunia haina budi kuhamishia raslimali zake nyingi, ikiwa ni pamoja na wafanyakazi, katika Afrika na kutoa misaada yake mingi kama misaada na siyo mikopo katika nchi masikini. Sharti ielekeze wafanyakazi wake wengi katika mataifa yenye asasi dhaifu na zisizo thabiti. Sharti ifanye ahadi za misaada ya muda mrefu na iwe na ratiba isiyobadilikabadilika ya jinsi, lini na kiasi cha fedha kitakacholipwa. Aidha, ikuze uratibu na wafadhili wengine, ikiwa ni pamoja na mashirika ya UN ambayo yanapaswa kukuza uratibu wao kwa ngazi ya taifa.

Shirika la Fedha Duniani (IMF) linaweza kusaidia nchi zinazoendelea katika kutathmini kutangaza taarifa juu ya bajeti na hesabu zao, na kwa hiyo kuwezesha raia wa nchi husika kudai serikali zao ziwajibike. IMF inaweza pia kusaidia ukadiriaji wa nje, kama vile mazungumzo kuhusu madeni. Sharti IMF ijizuie kuziwekea nchi viwango vya matumizi na inapaswa kukuza ugawanyaji sahihi/bora wa misaada kwa nchi masikini. Sharti ibadilishe utamaduni wake wa “mtoza kodi” na “mlipa madeni” na ionyeshe mnyambuliko mkubwa.

Vyote viwili – Benki ya Dunia na IMF – havina budi kujiondoa kwa kiwango kikubwa katika kujihusisha na uchumi wa taifa mojamoja na kupunguza masharti wanayoweka kwa nchi masikini. Masharti pekee ambayo yanapaswa kuwekwa ni kwamba sera za serikali za Afrika sharti zijielekeze kwenye maendeleo, ukuaji wa uchumi na upunguzaji wa umasikini, na kwamba katika kushughulikia bajeti zao, sharti wawe wazi na wawajibike kwa wapiga kura wao. Iwapo serikali za Afrika zitaachwa kufanya maamuzi mazito zenyewe, kama nyingine nyingi zinavyoonyesha hiari ya kufanya hivyo, mageuzi yana uwezekano mkubwa wa kuendelea. Methali moja ya Tanzania inasema hivi, “Yule ambaye kwa makusudi anaoga maji baridi hasikii baridi.”

Katika mazungumzo ya Shirika la Biashara Duniani (WTO), nchi tajiri sharti zitafute tu upendeleo mdogo kutoka kwa nchi masikini na siyo kubwa kama zile ambazo nchi masikini zinataka kutoka kwa nchi tajiri. Utamaduni wa kutendeana kiulinganifu katika mazungumzo ya biashara hautaisaidia Afrika kuondoa vikwazo vinavyoikabili. Wala nchi masikini zisitishwe na kukubali mipango mingi kupita kiasi na isiyoeleweka eti ikiwa ndiyo gharama ya kuingizwa kwenye WTO. Maazimio ya aina hii sharti yafanywe na mawaziri wa nchi tajiri kwenye mkutano ujao wa WTO.

Menejimenti za Benki ya Dunia, IMF na WTO sharti ziandae mikakati kwa Afrika inayozingatia masuala haya, hasa kwa mikutano yake ya mwaka ya 2005. Mkakati wa WTO sharti ukubaliwe kwenye mkutano wa mawaziri wa shirika hilo wa mwaka 2005. Kilicho muhimu zaidi hapa ni kutafuta njia za kuongeza uwajibikaji wa mashirika haya kwa wanahisa na wateja wake. Moja ya hatua za hiari ni kuunda kikundi cha kufuatilia na kuhakiki ubora wa misaada ya wafadhili katika kila nchi; hiki kinaweza kuwa kinajitegemea au kinaweza kuwa na wajumbe kutoka nchi zinazopokea misaada na nchi wafadhili. Lakini kilicho muhimu ni kwamba Afrika ipewe nafasi kubwa ya kufanya maamuzi katika mashirika haya ya kimataifa. Uwakilishi wa Afrika sharti uongezwe pia kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Sharti Afrika ipewe sauti yenye nguvu kwenye Bodi za Utendaji za Benki ya Dunia na IMF. Aidha, mwelekeo wa kimikakati wa mashirika haya sharti uwe mikononi mwa mabaraza yanayofanya maamuzi ambayo wajumbe wake watawajibika kwa viongozi wa kisiasa wenye uwezo wa kusema kwa niaba ya nchi wanachama.

Jukumu la mageuzi haya limo mikononi mwa viongozi wa kisiasa wa nchi wanachama ambao sharti wafanye mashirika haya ya kimataifa kuwa wazi zaidi na kuwajibika kwa umma. Kama ishara ya mabadiliko haya, nafasi za kazi za juu katika IMF na Benki ya Dunia zisiwe tena haki pekee ya watu kutoka Ulaya na Marekani bali zijazwe kwa njia ya ushindani ulio wazi. Iwapo hakutakuwa na mageuzi, jumuia ya kimataifa italazimika kufikia hitimisho kwamba mashirika haya yaliyoanzishwa baada ya Vita Vya Pili vya Dunia, sasa hayana maana katika dunia baada ya Vita Baridi, baada ya ubaguzi wa rangi na baada ya Septemba 11.

Mapendekezo yetu ni mpango makini wenye maelezo kinaganaga, lakini hautaweza kuwa wa mafao zaidi iwapo hakutakuwa na taratibu za kuyasimamia na kuyafuatilia. Kuna baadhi ya vyombo vilivyopo ambavyo vinaweza kupewa jukumu hili, lakini ama vina uwezo mdogo au havina madaraka ya kusimamia utekelezaji. Kwa hiyo, kuongeza nguvu ya ziada kwenye mapendekezo, Tume inapendekeza utaratibu unaojitegemea wa kuhakiki mwenendo wa yale ambayo tumependekeza. Utaratibu huu unaweza, kwa mfano, kuongozwa na watu wawili mashuhuri, wenye uzito katika jumuia ya kimataifa, mmoja Mwafrika na mmoja kutoka jumuiya ya wafadhili, ambao wanaweza kutoa taarifa ya mwaka ambayo ni fupi, wazi na timilifu. Hawa hawana budi kusaidiwa na kitengo kidogo kilichopo katika moja ya asasi za kimataifa au za Afrika.

Lakini hata kama mapendekezo yako wazi kiasi gani, au hatua za ufuatiliaji kuwaza juhudi gani, hakuna moja kati ya haya ambalo litafanikiwa bila utashi wa kisiasa. Ni utashi wa kisiasa pekee unaoweza kuziba mianya ya zamani kati ya ahadi na utekelezaji. Kujenga utashi huo wa kisiasa kunahitaji Afrika kuwa suala ambalo haliwezi kupuuzwa katika siasa za ndani za nchi za G8.

Tunajua kwamba – kwa msaada wa wabunge, vyombo vya habari, mashirika ya misaada, makanisa na makundi mengine ya dini, vyama vya wafanyakazi, Waafrika waishio nje ya bara lao na jumuiya ya kimataifa – hili linaweza kufanyika. Sauti za watu binafsi na vikundi vya ngazi ya chini katika jamii vinaweza kuleta mabadiliko makubwa. Kampeni ya Jubilei 2000 ilithibitisha hilo. Ilianzishwa na watu wawili lakini ilikamilishwa na watu milioni moja katika mitaa duniani kote, wakidai kwamba madeni ambayo nchi masikini zinadaiwa yafutwe. Serikali za nchi tajiri duniani zililazimika kusikiliza na deni la dola 100 bilioni lilifutwa.

Hii ndiyo maana kampeni ya kimataifa ya mwaka huu – Wito kwa Dunia Kuchukua Hatua (Fanya Umasikini kuwa Historia) ni muhimu sana. Tunategemea mwaka 2005 utakuwa mwaka ambamo asilimia 100 ya madeni yote yanayokabili nchi masikini yatafutwa. Kwenye uzinduzi wa kampeni hiyo mjini London, Februari mwaka huu, Nelson Mandela aliuambia umati uliofurika Trafalgar Square: "Katika karne hii mpya, mamilioni ya watu katika nchi masikini sana duniani wanaendelea kuwa wafungwa, watumwa na walioko kwenye minyororo. Wamenaswa kwenye magereza ya umasikini. Huu ndio wakati wa kuwaweka huru." Ni msononeko pekee na wa wazi unaoletwa na hali hii ambao utafanya wanasiasa wetu kutoa ahadi ya kuchukua hatua za kufanya hivyo. Na wakati huo kuwa thabiti katika kuziendeleza.

## Ahadi zilizovunjika na fursa zilizopotea

Yeyote anayeandaa mpango wa programu kubwa ya utekelezaji kama inayopendekezwa na Tume hii huwa makini kabisa na jambo moja. Uhusiano kati ya Afrika na nchi zilizoendelea ni juu ya mategemeo yaliyoibuliwa na yaliyotupwa daima ya ahadi zilizovunjwa na fursa zilizopotea. Hakika, viongozi wa Afrika wenyewe hawawezi kuachwa bila kutiwa hatiani. Afrika imeshindwa kutekeleza ahadi zake pia. Ahadi za kutumia asilimia 15 ya bajeti zao kwa afya hazikutekelezwa. Ahadi za jumla tu juu ya usawa wa jinsia hazijatekelezwa. Lakini orodha ya mipango ambayo haikukamilishwa na viongozi wa nchi tajiri duniani ni jambo lisilotia aibu kwa kiasi fulani.

Ahadi za "elimu kwa wote" zimepita bila kugharimiwa. Ndivyo ilivyo pia kwa VVU na Ukimwi. Juhudi za kuzuia rushwa hazijaidhinishwa na hazijatekelezwa. Kila baada ya ukatili mkubwa, dunia inasema "lisitokee tena," lakini inafumbia macho biashara katika silaha ndogo. Kanuni za maadili ya makampuni ya kimataifa zimebaki kuwa mazoezi tu katika nyanja ya mahusiano kibiashara. Kanuni za biashara zinatumika kwa namna inayokera. Ahadi za misaada zinaonekana kama malengo yasiyowezekana. Taratibu za kusamehe madeni zinapigwa chenga kwa vizuizi visiigwe. Mataifa tajiri hutoa ahadi zenye makusudi mazuri kwenye mikutano ya kimataifa tu na baadaye kuamua kwamba ahadi hizo, au ratiba yake, havikuwa halisi. Malengo yanawekwa na kuwekwa tena na kukadiriwa tena na tena, lakini hatima yake ni kwamba nchi tajiri huishia kiwango ambacho zimeshindwa kutekeleza. Ufa kati ya ahadi na utekelezaji hauzibiki kamwe.

Leo hii jumuiya ya kimataifa ina ahadi nyingine kubwa mbele yake. Miaka mitano iliyopita katika jiji la New York kila kiongozi wa dunia, kila chombo cha kimataifa, karibu kila nchi, waliweka saini azimio la kihistoria. Azimio la Milenia lilionyesha msimamo wa pamoja wa kusahihisha makosa mengi ya kizazi chetu. Lengo la Maendeleo la Milenia lilikuwa mpango wa kipekee ambao uliahidi ifikapo mwaka 2015 kila mtoto awe shuleni. Kwamba ifikapo 2015 vifo vya watoto ambavyo vinaweza kuzuilika vimezuilike. Kwamba ifikapo 2015 umasikini uwe umepunguzwa kwa nusu.

Kwa makadirio ya sasa, upunguzaji umasikini kwa nusu hautakuja ifikapo mwaka 2015 bali ifikapo mwaka 2150 – huko ni kuchelewa kwa miaka 135. Waafrika wanajua kwamba mara nyingine ni muhimu kuwa wavumilivu lakini miaka 135 ni mingi sana kuwaambia watu kusubiri, wakati watoto wao wanakufa na wakati sehemu nyingine duniani zina dawa za kuwaponyesha. Haistahili kusubiri haki kwa muda mrefu kiasi hicho.

Lengo la Maendeleo la Milenia ulikuwa mkataba wa uaminifu, labda kumnukuu Kamishna mwingine wa Tume, Waziri wa Fedha wa Uingereza Gordon Bropwn, "mkataba mkubwa wa uaminifu kuliko yote uliowahi kuahidiwa kati ya tajiri na masikini." Ahadi zinazotolewa kwa watu masikini hazina budi kuchukuliwa kuwa zinawafunga hasa kiutekelezaji wale wanaozitoa. Hundi inayolipa haki ya kimataifa haipaswi kurejeshwa, ama kwa kutumia msemo wazi wa Martin Luther King, ikiwa imeandikwa maneno "hakuna fedha za kutosha." Hatari tunayokabili leo ni kwamba kilichoanza kama mkataba mkubwa kuliko

yote kati ya tajiri na masikini, sasa kinageuka kuwa usaliti mkubwa kuliko yote uliofanywa na nchi tajiri kwa nchi masikini.

Tatizo siyo kwamba ahadi za Maendeleo ya Milenia hazikuwa sahihi na halisi au msimamo haukuwa muhimu. Ni kwamba dunia imekuwa na msukumo mdogo sana katika kukuza njia za kuutekeleza. Ukamilishaji wa ahadi unahitaji hatua thabiti na za haraka. Mpango wa utekelezaji wa Tume ya Afrika – ukuzaji utawala na miundombinu katika Afrika, kulipa zaidi bara la Afrika punguzo kubwa la madeni, kuongeza misaada maradufu na kupunguza umasikini kwa nusu na kuleta fursa mpya za biashara – kunaonyesha kuwa kuna njia sahihi/ya kweli ya kufanya haya. Bila programu kama ile. Lengo la Maendeleo la Malenia itapotea kama matakwa mengine mazuri. Na Afrika itabakia, katika maneno ya Mwenyekiti wa Tume hii, kovu kwenye dhamira ya dunia.

## Kwa nini tujihangaishe?

Kutakuwa na wale watakaosema tumekuwa na matumaini makubwa kupindukia au hatukuwa wa kweli. Watasema uchambuzi mwingi umefanywa huko nyuma. Katika miaka ya mwisho ya 1970 Tume ya Brandt ilitumia miaka saba ikichambua suala la umasikini duniani. Ripoti yake (Nchi Tajiri na Masikini au Nchi za Kaskazini na Kusini), ilipendekeza marekebisho mengi katika mfumo wa uchumi duniani ikiwa na shabaha ya kuunganisha uchumi wa nchi masikini (za Dunia ya Tatu) katika mfumo wa dunia. Mabadiliko yaliyofuata yalikuwa madogo na ya hapa na pale, lakini hii haipaswi daima kuwa mwisho wa juhudi kama hizi. Watu walibeza pia baada ya Vita Vikuu vya Pili wakati mpango ulioitwa Marshal Plan (mpango wa kusaidia kufufua uchumi wa nchi za Ulaya zilizoathirika vibaya wakati wa vita) ulipotangazwa. Mwaka 1948, Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Marekani, Jenerali Marshal, akikabiliwa na Ulaya yenye magofu, alipendekeza mpango mkubwa wa ujenzi mpya. Alianza na wazo finyu la misaada ya dharura lakini haraka akaja kwenye hitimisho kwamba kulikuwa na masuala mazito ya kijamii na kiuchumi ambayo yalistahili kukabiliwa.

Matokeo yake yalikuwa nchi tajiri sana duniani – Marekani – ilikubali kuhamisha asilimia moja (1%) ya mapato yake kitaifa, kila mwaka kwa miaka minne, kugharimia maendeleo ya Ulaya iliyokuwa imeharibiwa na vita. Nchi tajiri hivi sasa ni tajiri zaidi na nyongeza ya dola 25 bilioni kwa mwaka ambazo tunapendekeza kama hatua ya kwanza ni nyongeza tu ya asilimia 0.1 ya mapato yao. Hii sharti itumike kuleta mabadiliko katika maeneo mengi na kwa wakati mmoja kama Marshall Plan ilivyofanya. Hatuna budi kukumbuka hayo.

Kile ambacho Afrika inahitaji ni bayana. Inahitaji utawala mzuri na ujenzi wa uwezo wa mataifa ya Afrika wa kutenda na kuleta mabadiliko. Inahitaji amani. Inahitaji uimara kisiasa na kiuchumi ili kuweka mazingira ya ukuaji – na ukuaji ambamo watu masikini wanaweza kushiriki. Inahitaji uwekezaji katika miundombinu na katika mifumo ya afya na elimu ambayo itatoa nguvukazi yenye ujuzi na watu wenye furaha na waliotimiziwa mahitaji yao. Inahitaji kufanya biashara zaidi na kwa masharti ya haki kuliko nchi tajiri zinavyofanya sasa. Inahitaji nafuu ya madeni. Inahitaji misaada yenye ubora zaidi kuliko ilivyo sasa. Na inahitaji mara mbili ya misaada hiyo kugharimia haya yote.

Bila kufanya kazi ya uratibu wa wakati mmoja kwa eneo lote, ufufuaji wa uchumi wa Afrika utasimama, kama utakuwa umeanza kujongea. Bali ikiwa Afrika itapata msukumo tunaopendekeza – haraka kuliko wengi wanavyotegemea – sharti bara hili liwe katika nafasi nzuri ya kusimama kwa miguu yake lenyewe na hatimaye kufanya misaada kuwa jambo la historia.

Katika yote haya sharti Afrika iwe mbele/iongoze, lakini katika yote haya, Afrika inahitaji misaada mingi kutoka nchi tajiri, ambazo zitapaswa kutoa zaidi na pia kubadili tabia zao – katika biashara ya kimataifa, juu ya nafuu ya madeni na katika kuingiza Afrika katika fikra/ajenda za mashirika yake.

Kwa nini nchi tajiri zihangaike? Kwa kuanzia, kutokana na maslahi binafsi. Afrika iliyo imara na inayokua itakuwa soko la mamia ya mamilioni ya watu ambamo sehemu nyingine ya dunia itauza bidhaa na huduma zake. Afrika ina uwezekano wa kubadilishwa kutoka kuwa nafasi ya ufukara na kuwa nafasi ya fursa. Itaweza pia kuwa chanzo imara cha mahitaji. Afrika ina asilimia saba ya akiba ya mafuta duniani na mwaka 2000 ilitoa asilimia 11 ya mafuta yote duniani. Hadi 2015, Afrika Magharibi itauza asilimia 25 ya mafuta nchini Marekani. Na utajiri wake katika raslimali haukushikizwa kwenye bidhaa za asili. Ni chanzo muhimu cha koltani *(coltan)*,

Sisi ni ulimwengu wa maadili moja. Na maana yetu ya tabia hii ni kutambua jukumu letu kwa wengine. Sisi, tukiwa kundi la mchanganyiko wa Makamishna Waafrika na wasio Waafrika, tunalielewa hili kutokana na uzoefu wetu mkubwa kwani tumefungamana katika maslahi yetu ya pamoja.

Wakati wa mabadiliko ni huu. Hiyo ndiyo imani yetu sote. Kwa kusimama na kutenda kwa pamoja tuna uwezo wa kubadili historia. Kutofanya lolote hakutavumilika. Hata hivyo kufanya lolote tu hakutatosha. Kufanya kila kitu tunachoweza siyo mahitaji pekee, ndilo jukumu letu dhahiri. Huu ndio wakati wa kuchukua hatua.

Afrika imeanza kuleta maendeleo katika vita vya muda mrefu dhidi ya umasikini. Bali kuendeleza vita hivyo kutahitaji ushirikiano wenye nguvu kati ya mataifa ya Afrika na yale ya nchi tajiri. Hii ina maana ya kuchukua hatua na mabadiliko kwa pande zote mbili.

Sharti Afrika iongoze katika ushirikiano huu, ichukue jukumu la matatizo yake na imiliki ufumbuzi ambao utaonekana zaidi kuwa utafaa iwapo utatokana na umaizi na maamuzi ya Kiafrika kuliko ule wa kushinikizwa kutoka nje. Nayo jumuiya ya kimataifa, sharti iache kufanya mambo yanayoumiza au kuleta madhara kwa watu masikini sana duniani. Haina budi kufanya kila linalowezekana kusaidia mageuzi ambayo yanaendelea katika Afrika; na haya sharti yaendelezwe kikamilifu iwapo bara linahitaji kustawi na watu wake masikini kunufaika na (kushiriki katika) ustawi huo. Sharti jumuiya ya kimataifa iunge mkono juhudi za kwanza za Afrika ikiwa ni pamoja na mpango wa NEPAD wa UA, kufanya kazi nao na kukuza mageuzi haya.

Baadhi ya mapendekezo yetu – juu ya miundombinu, afya, elimu – yanahitaji uhamishaji wa kiwango kikubwa cha fedha kutoka nchi zilizoendelea kwenda Afrika. Mengine – yanayoimarishwa na mitizamo mipya inayohusu utamaduni wa Afrika – yanahitaji mabadiliko ya tabia, njia za kufanya kazi na vipaumbele. Mengine yanataka jumuiya ya kimataifa kuacha kufanya yale ambayo yanaleta madhara kwa Afrika. Haya yote hayana budi kuchukuliwa kama mpango mmoja. Washiriki hawana budi kufanya kazi pamoja kutekeleza mpango huu kwa dhamira, uvumilivu na kasi, kila mmoja akilenga jinsi ya ambavyo wanaweza kutoa mchango thabiti.

## A: Mapendekezo kuhusu Utawala na Kujenga Uwezo

- Wanataaluma wenye ujuzi ni muhimu katika kuimarisha uwezo kiutawala na kiufundi ambao unakosakana sana Afrika. Katika mwaka wa 2005, jumuiya ya kimataifa inapaswa iahidi kuchangia kiasi cha dola za kimarekani milioni 500 kila mwaka kwa kipindi cha miaka 10 kwa ajili ya kuimarisha taasisi za elimu ya juu za Afrika na kuchangia hadi dola za kimarekani bilioni 3 kwa zaidi ya miaka 10 kwa ajili ya kujenga vituo bora vya sayansi na teknolojia, ikiwa ni pamoja na Taasisi za Teknolojia za Afrika.

### Kuongeza uwajibikaji na uwazi

- Mabunge katika nchi zilizoendelea na zinazoendelea hayana budi kuanzisha ushirikiano wa kuimarisha mabunge katika Afrika, ikiwa ni pamoja na Bunge la Afrika.
- Vyombo huru vya habari, vyombo vya utangazaji vya umma, vyama vya kiraia na sekta binafsi, kwa kusaidiwa na serikali, havina budi kuunda muungano wa wabia ndani na nje ya Afrika, ili kutoa fedha na utaalam wa kuunda mfuko wa kuendeleza uwezo wa vyombo vya habari vya Afrika.
- Serikali za nchi zilizoendelea, wanahisa katika makampuni na walaji hawana budi kuyashinikiza makampuni yaongeze uwazi katika shughuli zao katika nchi zinazoendelea na yazingatie kanuni na viwango vya tabia za kimataifa.
- Jumuiya ya kimataifa sharti iunge mkono kwa dhati, kisiasa na kifedha, mipango mahususi kama ule wa Juhudi Dhahiri za Viwanda Sindikaji (EITI) ili kuongeza uwazi katika malipo yanayofanywa kwa, na yanayopokelewa na, serikali na ihimize kukubalika kwa mipango hiyo miongoni wa nchi zenye utajiri wa rasilimali katika Afrika. Jumuiya ya kimataifa iunge mkono uandaaji wa vigezo na mbinu kwa ajili ya kuhalalisha utekelezaji wa EITI. Aidha isaidie na kugharimia ujenzi wa uwezo miongoni mwa watumishi wa serikali na vyama vya kiraia, kwa kuchangia Mfuko wa Wafadhili wa Juhudi Dhahiri za Viwanda Sindikaji *(EITI Multi-donor Trust Fund).*
- Misingi ya uwazi kama ile ya EITI haina budi kuenezwa katika sekta za maliasili, ikiwa ni pamoja na misitu na uvuvi.
- Nchi ambazo zinanunua mbao na bidhaa za mbao sharti zihakikishe kwamba hazifanyi biashara ya bidhaa za misitu ambazo zimepatikana kinyume cha sheria, na sharti zinunue mbao na bidhaa zilizopatikana kwa msingi wa kisheria.

### Ufisadi (Rushwa)

Ufisadi ni changamoto ya kimfumo inayowakabili viongozi wengi wa Afrika. Viongozi wa Afrika hawana budi kudhihirisha utashi mpya wa kisiasa wa kupiga vita rushwa katika ngazi zote katika uchumi na jamii. Mataifa mengi ya Afrika yameanza kutekeleza jukumu hili. Kuongezeka kwa uwazi katika Serikali za Afrika kutasaidia katika hili. Hata hivyo kupambana na rushwa ni pamoja na kukabiliana na wale wanaoitoa na wanaoipokea.

- Nchi zilizoendelea hazina budi kuhimiza Mawakala wa Mikopo ya Kuuza Bidhaa Nje (ECAs) wawe wawazi, na waweke viwango vya juu vya uwazi katika misaada yao kwa miradi ya nchi zinazoendelea. Aidha nchi zilizoendelea zitekeleze kikamilifu makubaliano ya nchi wanachama wa kundi la mataifa ya viwanda kuhusu vita Dhidi ya Rushwa na Mikopo ya Kuuza Bidhaa Nje inayotambuliwa rasmi na nchi wanachama wa kundi hilo.
- Nchi na majimbo yenye taasisi nyingi za kifedha, hazina budi, na hili likiwa suala la haraka, kuchukua hatua za kisheria na kiuendeshaji kurejesha fedha na mali ambazo ziliporwa kutoka nchi kwa njia zisizo halali. Tunatoa mwito kwa nchi za G8 kutoa ahadi mahususi katika mwaka 2005 na kutoa taarifa ya maendeleo, ikiwa ni pamoja na fedha zilizorejeshwa mwaka 2006.

- Mataifa yote hayana budi kuridhia na kutekeleza, katika mwaka 2005, Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya rushwa na hayana budi kuhimiza uwazi zaidi katika sera za ununuzi katika Afrika na nchi zilizoendelea, hasa katika maeneo ya ujenzi na uhandisi.

### Kuimarisha mifumo habari

Taarifa nzuri ni muhimu katika kutengeneza sera bora na utekelezaji thabiti. Wafadhili hawana budi kutoa kiasi cha dola za kimarekani milioni 60 kwa mwaka ambacho kinahitajika kusaidia Afrika kukuza mifumo yake ya kukusanya na kuchambua data, ili kufikia vigezo ambavyo, katika hali ya kawaida, huitwa viwango vya chini vinavyokubalika.

## B: Mapendekezo kuhusu Amani na Usalama

Haki ya kuishi na usalama ni haki ya msingi sana miongoni mwa haki za binadamu. Bila kuwa na ongezeko la uwekezaji katika kuzuia migogoro, Afrika haitakuwa na kasi ya maendeleo ambayo watu wake wanatafuta. Jukumu la kutanzua migogoro katika Afrika sharti liwe mikononi mwa Waafrika wenyewe, bali kuna mengi mengine ambayo nchi zilizoendelea zinaweza kufanya kuimarisha uzuiaji wa migogoro. Kule tu kuwekeza katika maendeleo ni kuwekeza katika amani na usalama.

### Kukabiliana na sababu za migogoro na ujenzi wa uwezo wa kuisimamia

- Kufanya misaada kuwa ya maana kwa kupunguza migogoro, wafadhili wote, taasisi za fedha za kimataifa na Umoja wa Mataifa inabidi wahimizwe kutumia tathmini kuhusu jinsi ya kupunguza hatari ya migogoro ya silaha na kukuza usalama wa binadamu katika kuandaa mikakati ya misaada kwa nchi na eneo husika.
- Kama suala la kipaumbele, na isiwe zaidi ya mwaka 2006, jumuiya ya kimataifa iwe imeanzisha mazungumzo kuhusu mkataba ATT.
- Jumuiya ya kimataifa pia ichukue hatua thabiti na zinazobana kisheria za makubaliano kuhusu udalali wa silaha kitaifa na kimataifa na kuweka viwango sawa katika ufuatiliaji na usimamiaji wa utekelezaji. Makubaliano haya yanaweza kuunganishwa katika makubaliano mapana ya ATT.
- Kuongeza kasi ya kuzuia biashara ya maliasili katika kugharimia vita, jumuiya ya kimataifa inapaswa:
  - Kukubaliana kuhusu fasili moja kuhusu 'raslimali za migogoro' ili iweze kukubalika kimataifa kupitia UN.
  - Kuunda jopo la kudumu la wataalamu katika UN la kufuatilia uhusiano kati ya uchimbaji wa raslimali za asili na migogoro ya kivita na utekelezaji wa vikwazo. Jopo hilo sharti lipewe madaraka ya kupendekeza hatua za utekelezaji kwa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.
- Nchi za Shirika la Ushirikiano wa Uchumi na Maendeleo OECD sharti zikuze maendeleo na utekelezaji kikamilifu wa miongozo iliyo wazi kwa makampuni yaliyoko katika maeneo ya hatari ya migogoro ya silaha, ili yaingizwe katika miongozo ya OECD katika mashirika ya kibiashara ya kimataifa.

### Kujenga uwezo kikanda na kimataifa wa kuzuia na kutanzua migogoro

Jumuia ya kimataifa sharti iheshimu ahadi zilizopo za kuimarisha uwezo wa kulinda amani katika Afrika, ikiwa ni pamoja na kusaidia kutoa mafunzo pamoja na gharama nyingine. Hata hivyo iende mbali zaidi kwa kuongeza uwekezaji katika njia maridhawa za kuzuia migogoro na zisizo za kijeshi.

- Ili kuuwezesha Umoja wa Afrika uchukue hatua za haraka na madhubuti kuzuia na kumaliza migogoro ya kijeshi, wafadhili hawana budi kukubali kugharimia angalau asilimia 50 ya Mfuko wa Amani wa Umoja wa Afrika kuanzia mwaka 2005. Kwa kadri itakavyowezekana, na kama motisha kwa UA kwa utekelezaji thabiti wa uwazi katika matumizi, michango hii inapaswa kutengwa na kutolewa kwa pamoja kila mwaka. Pale ambako fedha zitatolewa moja kwa moja kwa jumuia za kiuchumi za kikanda katika Afrika, sharti nazo ziratibiwe.
- Katika mwaka 2005 UN na mashirika ya kanda sharti yachukue hatua za kubainisha nafasi na majukumu yao na vigezo vya kuchukua hatua kuzuia na kutanzua migogoro. Hayana budi pia kuweka mifumo thabiti ya uratibu.

- Katika mwaka 2005 Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa sharti lianzishe Tume ya Kujenga Amani ya Umoja wa Mataifa kama ilivyopendekezwa na Jopo la Mabingwa wa Umoja wa Mataifa la masuala ya Matishio, Changamoto na Mabadiliko (UNHLP).
- Sharti Tume hii iwe na uwezo na raslimali za kutekeleza kazi iliyopewa ya kuzuia migogoro ya kivita na kuratibu ujenzi wa nchi baada ya vita kumalizika.

### Kujenga amani baada ya migogoro

Pamoja na kuunga mkono Tume ya Kujenga Amani ya UN kuboresha uratibu wa kujenga amani katika kipindi cha baada ya migogoro, tunapendekeza hatua zaidi:

- Wafadhili sharti wagharimie ulipaji haraka wa viporo vya madeni ya nchi zilizotoka vitani katika Afrika ili kuziwezesha kupata ridhaa mapema ya kukopeshwa na asasi za fedha za kimataifa. Kufuatana na mapendekezo ya ripoti hii kuhusu ubora wa misaada, sharti wafadhili waweke pia utaratibu wa ruzuku ya muda mrefu na ya kuaminika inayotosheleza mahitaji ya ujenzi mpya wa nchi zilizokuwa kwenye migogoro.

## C: Mapendekezo kuhusu kushirikisha kila mtu: Kuwekeza katika watu

Hakuna mbadala wa nyongeza kubwa ya raslimali zinazohitajika kwa ajili kuondosha uwekezaji duni wa miaka mingi katika elimu, afya na hifadhi ya kijamii.

Matumizi bora ya raslimali hizi kubwa yatahitaji mipango mikubwa inayohusu utoaji na ufuatiliaji wake. Hadi hapo, sharti Serikali za Afrika ziendelee kuimarisha utawala na kuhakikisha kunakuwa na ushiriki wa watu wa kawaida na jumuia za kiraia katika kutoa maamuzi yanayohusu maendeleo. Katika hili, jumuiya ya kimataifa sharti itekeleze kile ilichoahidi. Aidha, Serikali za Afrika na wafadhili wa kimataifa sharti wahakikishe kwamba kunakuwa na fursa kwa wote.

### Elimu

- Wafadhili na Serikali za Afrika hawana budi kutekeleza ahadi zao ili kufikia kupatikana kwa Elimu kwa wote, wakihakikisha kwamba kila mtoto katika Afrika anakwenda shule. Wafadhili hawana budi kutoa nyongeza ya dola za kimarekani bilioni 7 … 8 kwa mwaka wakati Serikali za Afrika zikichukua hatua za kuwa na mipango mikubwa ya kitaifa ya kutoa elimu bora.
  - Katika mipango yao ya kitaifa, Serikali za Afrika sharti zitafute taratibu za kuweka wasichana na wavulana katika shule kwa mgawo mzuri wa raslimali. Wafadhili hawana budi kugharimia nyongeza hii.
  - Serikali za Afrika hazina budi kuondoa ulipaji wa karo kwa elimu ya msingi, na wafadhili hawana budi kugharimia hilo hadi hapo nchi za Afrika zitakapokuwa zimepata uwezo wa kumudu gharama hizi.
  - Kuhakikisha kwamba elimu bora inatolewa, Serikali za Afrika sharti ziwekeze katika ufundishaji wa walimu, kulinda watumishi wasikimbie kazi zao na kuendeleza utaalamu. Kiwango cha wanafunzi kwa mwalimu mmoja kiwe chini ya mwalimu mmoja kwa wanafunzi 40 (1:40) katika shule za msingi. Wafadhili hawana budi kutoa ahadi za muda mrefu na za kuaminika za kuwezesha hili.
  - Elimu sharti itoe stadi muhimu zinazoendana na mazingira ya sasa ya Afrika. Wafadhili hawana budi kugharimia mifumo ya kanda kwa shabaha ya kusaidia Serikali za Afrika katika kuandaa na kukuza mitaala muwafaka kwa ngazi zote.

### Afya

- Serikali za Afrika sharti ziwekeze katika ujenzi mpya wa mifumo ya utoaji huduma ya afya kwa umma. Wafadhili hawana budi kutoa dola za kimarekani bilioni 7 katika kipindi cha miaka mitano kwa ajili ya hili, ikiwa ni kuunga mkono programu ya UA ya NEPAD inayohusu Mikakati ya Awali ya Mpango wa Utekelezaji.
- Wafadhili na Serikali za Afrika sharti wawekeze haraka katika utoaji mafunzo na kuhakikisha waliofunzwa wanabaki kazini ili ifikapo 2015 iwepo nyongeza ya watumishi wa afya wapatao milioni moja.
- Serikali za Afrika sharti zitimize ahadi zake za kutenga asilimia 15 ya bajeti zao kwa afya na kuweka utaratibu wa mikakati ya kutoa huduma za afya kwa ufanisi zaidi. Wafadhili hawana budi kuongeza mchango wao kwa mikakati hii, kwa kukabiliana na upungufu uliopo kwa kutoa mara moja nyongeza ya dola za kimarekani bilioni 10 kwa mwaka na kupanda hadi dola bilioni 20 kwa mwaka ifikapo 2015. Msaada huu hauna budi kupitishwa kwenye bajeti za kitaifa.

- Pale ambapo Serikali za Afrika zitaondoa ulipiaji wa gharama za afya kama njia mojawapo ya kuleta mabadiliko, wafadhili hawana budi kutoa ahadi ya muda mrefu kujaza pengo hilo la kifedha hadi nchi zitakapokuwa na uwezo wa kugharimia.
- Wafadhili sharti watoe kiasi chote kinachohitajika katika Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na UKIMWI na Malaria.
- Wafadhili sharti waahidi kutoa kiasi chote kwa Umoja wa Chanjo Duniani (GAVI) kupitia mpango wa Fursa za Fedha za Chanjo Kimataifa (IFFim). Hawana budi pia kutekeleza ahadi zao kwa mfuko wa Juhudi za Kuteketeza Polio (PEI) ifikapo 2005.
- Mkakati wa Shirika la Afya Duniani wa 'Magonjwa mawili, mgonjwa mmoja,' sharti uungwe mkono ili kupata huduma iliyounganishwa ya kukabiliana na TB na VVU.
- Serikali za Afrika na wafadhili hawana budi kufanya kazi pamoja kuhakikisha kwamba kila mjamzito na kila mtoto ana chandarua kilichowekwa dawa itakayodumu kwa muda mrefu na anapewa dawa sahihi za kuzuia malaria.
- Wafadhili hawana budi kuhakikisha kwamba kuna fedha za kutosha kwa ajili ya matibabu na kinga ya magonjwa ya vimelea na upungufu wa viini muhimu katika lishe. Serikali na washiriki wa kimataifa katika mambo ya afya wahakikishe kwamba hili linaingizwa katika kampeni za afya ya umma ifikapo mwaka 2006.
- Serikali za Afrika sharti zidhihirishe kuongoza katika kukuza haki za wanawake na wanaume katika afya ya uzazi. Wafadhili wafanye kila linalowezekana kuwezesha kupatikana kwa huduma ya afya na uzazi kwa wote.
- Wafadhili hawana budi kuweka motisha za utafiti na maendeleo katika afya ambavyo vinakidhi matakwa ya Afrika. Sharti waweke mikataba mapema ya ununuzi wa madawa. Hawana budi kuongeza ugharimiaji wa moja kwa moja wa utafiti unaoongozwa na Afrika, kuratibiwa na jumuia za kiuchumi za kanda na kwa ushirikiano na wabia katika mambo ya afya duniani.

### Maji safi na majitaka

- Kuanzia mwaka 2005, sharti wafadhili wageuze mkondo wa ufifiaji wa misaada katika sekta ya maji na majitaka ili kuwezesha serikali kufikia ahadi ya Dira ya Maji Afrika (DMA) ya kupunguza kwa asilimia 75 idadi ya watu wasiopata maji salama na huduma ya majitaka ifikapo 2015. Ifikapo 2007, nchi za G8 sharti zitoe taarifa ya utekelezaji wa mpango wake wa maji kama ilivyokubaliwa mwaka 2003.

### VVU na UKIMWI

- Jumuiya ya kimataifa haina budi kufikia makubaliano ya dunia nzima ya mwaka 2005 ya kuunganisha juhudi mbalimbali za kupambana na VVU na UKIMWI. Hii sharti iwe njia ya kuunga mkono mikakati ya Serikali za Afrika inayozingatia mahusiano ya kimamlaka kati ya wanaume, wanawake na vijana.
- Kama ilivyokubaliwa katika Azimio la Kikao Maalumu cha Baraza la Umoja wa Mataifa (UNGASS) kuhusu VVU na UKIMWI, Serikali za Afrika na jumuiya ya kimataifa sharti zifanye kazi haraka kwa pamoja ili kuwawezesha watu kufurahia haki yao ya kinga, tiba na huduma. Wafadhili hawana budi kugharimia mahitaji ya haraka na hivyo kuongeza mchango wao kwa angalao dola za kimarekani bilioni 10 kila mwaka katika kipindi cha miaka mitano.

### Utunzaji wa wanaoishi katika mazingira magumu

- Serikali za Afrika hazina budi kuweka mikakati ya ulinzi wa kijamii wa watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu. Wafadhili hawana budi kutoa ahadi inayotabirika ya kugharimia, tena kwa kipindi kirefu, mikakati hii kwa kuanza kutoa mara moja dola za kimarekani bilioni 2 na kuendelea hadi dola bilioni 6ifikapo mwaka 2015.
  - Wafadhili hawana budi kusaidia mpango wa NEPAD wa kukuza mfumo wa haki na ushirikishwaji na kusaidia nchi kukuza mikakati ya huduma za jamii ifikapo 2007.
  - Wafadhili na nchi za Afrika hawana budi kuridhia na kutekeleza Kiunzi cha UN kwa ajili ya Ulinzi, Huduma na Misaada kwa watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu.
  - Wafadhili na Serikali za Afrika hawana budi kutoa msaada wa kibajeti wa moja kwa moja kwa mashirika ya kikontinenti ili kusaidia katika kazi za kulinda haki za wanawake na watoto.

## D: Mapendekezo kuhusu ukuaji wa uchumi na upunguzaji wa umasikini

Umasikini katika Afrika utaendelea kuongezeka iwapo hapatakuwa na ukuaji mkubwa wa uchumi – na wa aina itakayoshirikisha watu masikini. Na hakuna anayepaswa kuachwa nje. Wale wanaoweka sera sharti wafikirie daima athari za sera hizo kwa watu masikini. Mapendekezo yaliyomo katika sura hii na sura nyingine hayana budi kuwezesha nchi za Afika za kusini mwa jangwa la Sahara kufikia na kuendeleza viwango vya ukuaji wa uchumi vya asilimia 7 ifikapo 2010.Vilevile vitaongeza ushirikishwaji wa watu masikini katika fursa zilizoletwa na ukuaji huo. Kwa njia hiyo watashughulikia upunguzaji wa ukosefu wa ulinganifu katika mapato, ambao unaweza kudhoofisha matokeo ya ukuaji wa uchumi kwa umasikini.

Mapendekezo yetu yamegawanywa katika sehemu mbili: Sehemu ya kwanza inahusu hasa ukuzaji wa uchumi. Ukuaji wa haraka na upunguzaji wa umasikini kwa kiwango kikubwa, vinahitaji uwekezaji mkubwa katika miundombinu, kilimo, maendeleo mijini, ujenzi wa mazingira mazuri ya uwekezaji na sera zinazozingatia mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa. Ukuaji utaongozwa na sekta binafsi, lakini serikali inajenga mazingira ya hili – changamoto ni kujenga ubia kati ya serikali na sekta binafsi.

Sehemu ya pili ya mapendekezo yetu inahusu ushirikishwaji wa watu masikini katika ukuaji huo. Katika hili, msisitizo maalum sharti uwekwe kwenye fursa muhimu na haki za wanawake, ambao mara nyingi wana mchango muhimu sana katika ukuaji wa biashara ndogondogo. Vijana wanahitaji ajira. Jumuiya ya kibiashara inaweza kusaidia katika maeneo haya.

### Kushirikisha watu maskini katika ukuaji wa uchumi

Nchi zilizoendelea hazina budi kuunda Mfuko wa Kukuza Biashara Afrika wa dola za kimarekani milioni 100 kwa ajili ya kusaidia juhudi za sekta binafsi ambazo zinachangia ukuaji wa biashara ndogo kwa kuziwezesha kufikia masoko. Mfuko utahimiza ushirikiano mpya katika sekta za fedha na zisizo za fedha na kuchangia kwenye utekelezaji wa shabaha za UA za kukuza uongezekaji wa ajira kwa vijana na ujasiriamali wa wanawake.

Serikali za Afrika sharti ziwe mstari wa mbele katika kukuza ajira kwa vijana, wanawake kwa wanaume, katika sera zao za ukuaji. Wafadhili hawana budi kusaidia Serikali za Afrika katika kuandaa na kutekeleza mipango ya kitaifa ya ajira kupitika Mtandao wa Ajira kwa Vijana (YEN).

### Kuimarisha nafasi ya biashara

Tume inatoa wito wa mabadiliko makubwa zaidi katika njia ambazo jumuiya ya biashara, katika nchi zinazoendelea na duniani kote, inavyojihusisha katika hatua za maendeleo katika Afrika. Makampuni ya biashara sharti yakubali kufuata kanuni kuu za maadili mema kijamii na kimazingira, ikiwa ni pamoja na yale yanayohusu rushwa na uwazi, na kuelekeza juhudi zao katika hatua ya pamoja ya kuukabili umasikini. Hii inapaswa kufanywa kwa ushirikiano wa wote – wafadhili, serikali za kitaifa, jumuiya za kijamii, ikiwa ni pamoja na vyama vya wafanyakazi. Katika kuunga mkono hili, nchi zilizoendelea hazina budi kusaidia juhudi za Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) za kukuza biashara endelevu katika eneo la Afrika. Kwa upande wao, wafadhili na Serikali za Afrika sharti wakuze ushirikiano na sekta ya binafsi.

### Mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa

Kwa kuunga mkono mpango wa NEPAD wa Juhudi za Mazingira, wafadhili hawana budi kuzingatia suala la mazingira katika mipango yao. Serikali za wafadhili na mashirika ya kimataifa, ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia na Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa (UNEP) na Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO) sharti wahimize uingizwaji wa mazingira endelevu katika mbinu za Serikali za Afrika za kupunguza umasikini. Hizi sharti zihusishe viashiria vya ufuatiliaji wa utendaji katika masuala ya mazingira.

Nchi zilizoendelea sharti ziweke malengo ya matumizi makubwa ya teknolojia safi za nishati ili kukuza biashara yake duniani na kuchochea matumizi yake katika nchi zinazoendelea. Wafadhili sharti wajitahidi kukuza mitandao ya uchunguzaji wa hali ya hewa kupitia Mfumo wa Uchunguzi wa Hali ya Hewa Duniani (GCOS), misaada kati ya nchi na nchi na mipango ya kujenga uwezo wa uratibu kati ya wafadhili na taasisi za uchunguzi za Afrika. Kuanzia mwaka 2008 wafadhili hawana budi kufanya tofauti za hali ya hewa na mabadiliko ya hali ya hewa kuwa sehemu muhimu ya mipango na uhakiki wa miradi yao. Sharti watimize ahadi zao za kutoa fedha kusaidia nchi za Afrika kujiweka tayari kwa hasara na athyariza mabadiliko ya hali ya hewa.

## E: Mapendekezo kuhusu Biashara

Ongezeko katika biashara ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi. Mgawo wa Afrika katika biashara ya kimataifa umeshuka hadi asilimia mbili, kutoka asilimia sita miaka ishirini iliyopita, na imekuwa nyuma ya washindani wake. Afrika inakabiliwa na changamoto kubwa iwapo inataka kubadili mwenendo huu na kusonga mbele. Sharti Serikali za Afrika zisimamie mchakato huu wa kuruhusiwa kuweka sera zao za biashara. Kuna hatua tatu muhimu ambazo zinaweza kuchukuliwa, kwa ushirikiano, na nchi za Afrika na jumuia ya kimataifa, ili kuwezesha hili kufanikiwa. Hizi ni kuunga mkono mikakati iliyoundwa na Afrika kwa ajili ya kujenga uwezo wa biashara; kubomoa vikwazo vya kiuchumi duniani kwa kupitia mazungumzo ya Doha kuhusu biashara duniani; na kutoa msaada wa mpito kwa Afrika ili iweze kujiandaa kwa mifumo mipya ya biashara duniani.

### Kukuza uwezo wa Afrika katika biashara

- Afrika sharti iongeze uwezo wake wa kufanya biashara. Haina budi kuondoa vikwazo vyake vya kiuchumi kati ya nchi moja na nyingine. Hatua za kusaidia biashara zitakuwa muhimu, ikiwa ni pamoja na marekebisho katika forodha na sheria nyingine. Na sharti Afrika iongeze juhudi ili kupata ufanisi mkubwa katika uchumi kwa njia ya ushirikiano baina ya kanda za Afrika. Baadhi ya hatua hizi zitakuwa rahisi na za gharama ndogo.
- Sharti Afrika ifanye juhudi zaidi za kurekebisha mazingira ya kiuchumi ya wakulima na makampuni, ikiungwa mkono na vitegauchumi vikubwa vinavyotokana na misaada ya wafadhili wa kimataifa ili kuhakikisha kwamba Afrika inaweza kuzalisha na kufanya biashara kiushindani. Aidha, sharti sehemu ya gharama za miundombinu itumike kukuza uchukuzi na mawasiliano ili kupunguza gharama.

### Kuboresha mauzo ya Afrika katika masoko ya nchi tajiri

- Nchi zilizoendelea hazina budi kuhakikisha kwamba mazungumzo ya Doha kuhusu biashara duniani yanafanya maendeleo kuwa kipaumbele pekee kwenye mikutano ya Desemba 2005 ya Shirika la Biashara la Dunia (WTO) huko Hong Kong. Mazungumzo ya Doha hayana budi kumalizika kabla ya mwisho wa mwaka 2006 ili yaweze kuwa ya maana kwa Afrika na nchi nyingine zinazoendelea.
- Nchi tajiri sharti zikubaliane kuondoa mara moja ruzuku kwa wakulima wa pamba na sukari; na kuahidi ifikapo mwaka 2010, zitakapokutana Hong Kong, kufute ruzuku zote kwenye biashara ya nje na kwenye kilimo. Wakati wa kuhitimisha mazungumzo ya Doha, nchi tajiri zikubaliane kupunguza ushuru, hatua kwa hatua, hadi utakapokuwa umefutwa ifikapo 2015 na kupunguza vikwazo visivyokuwa vya ushuru. Kwa kufanya hivyo watakuwa wamepunguza kwa kiwango kikubwa matumizi yasiyokuwa ya lazima na kuleta faida kwa watu wao na kwa Afrika na nchi nyingine zinazoendelea.
- Nchi zinazoendelea ambazo zina mapato ya juu nazo hazina budi kupunguza ushuru na vikwazo vingine vya biashara kati yake na Afrika.
- Kwa kufanya maendeleo kuwa aula katika mazungumzo ya biashara, ikiwa ni pamoja na mikataba ya biashara ambayo Ulaya inajadili hivi sasa na Afrika, ulegezaji wa masharti ya biashara usifanywe kuwa jambo la lazima kwa Afrika kupitia biashara au masharti ya misaada; na sharti hili lifanywe katika njia inayopunguza uwezekano wa mmoja kudai kutendewa sawa kama alivyotendewa mwingine. Nchi mojamoja za Afrika sharti ziruhusiwe kupanga utaratibu wake wa mageuzi ya kiuchumi, kwa kasi yao wenyewe, kufuatana na mipango yao ya upunguzaji umasikini na maendeleo. Msaada mwingine wa kifedha hauna budi kutolewa kuwezesha nchi zinazoendelea kujenga uwezo wanaouhitaji kufanya biashara na kujiweka tayari kwa masoko yaliyo wazi zaidi.

- Sharti kuwepo upendeleo maalum kwa Afrika na nchi nyingine zinazoendelea, kwa kulazimika kuingilia migogoro ya kisheria inayofungamana na tathmini ya masuala ya maendeleo. Tafakuri ya ibara ya XXIV ya Makubaliano ya Jumla ya Ushauri na Biashara (GATT) kuhusu kupunguza mahitaji ya kudai kutendewa kama ulivyomtendea mwenzako kibiashara, na kuongeza mwelekeo kwenye vipaumbele vya maendeleo, inaweza kuwa muhimu hapa.
- Ingawa Afrika inataka kufikia viwango vya bidhaa vya nchi zilizoendelea, inapambana kupata fedha za kuiwezesha kufanya hivyo. Nchi tajiri hazina budi kutumia vipimo vya maendeleo, ikiwa ni pamoja na kutathmini ufanisi, wakati wa kuandaa viwango hivi ili kupunguza vikwazo vinayoweza kupunguza ufanisi , na ziwe tayari kusaidia katika kufikisha viwango hivyo.

### Kuisaidia Afrika katika kuingia kwenye mifumo mipya ya biashara

Itachukua muda kujenga uwezo wa Afrika wa kufanya biashara na kuwa na mageuzi katika mazungumzo ya Doha. Katika kipindi hiki, Afrika itahitaji msaada wa mpito ili iweze kwenda mbele.

- Nchi zilizoendelea lazima ziondoe vikwazo kwa bidhaa zote zinazouzwa nje ambazo zinatoka katika nchi za Afrika zenye mapato ya chini za kusini mwa jangwa la Sahara, kwa kuingiza bidhaa zake zote kwenye mgawo maalum na kuziondolea ushuru. Hatua hii itazigharimu kidogo sana nchi zinazoendelea. Sharti ziache kutumia kanuni ya "bidhaa zitokako" kwa njia iliyonuia kuzuia badala ya kusaidia wauza bidhaa nje wa Afrika, kwa kuruhusu Afrika ipate malighafi kutoka kokote duniani na kutaka Afrika iongeze tu asilimia 10 ya thamani ya usindikaji. Mikataba mipya kati ya Ulaya na Afrika sharti ishughulikie hili haraka sana. Kama nchi zilizoendelea zingetoa mgawo wa bidhaa za kuuza nchini mwao na kuziondolea ushuru bidhaa hizo, mapato ya nchi za Afrika za kusini mwa jangwa la Sahara yangepanda kwa dola za kimarekani bilioni 5.
- Nchi tajiri pia hazina budi kusaidia uchumi wa Afrika kujiweka tayari kwa mfumo wa biashara wa dunia ulio wazi zaidi, kuendeleza mazuri yake na kuzuia athari mbaya kwa watu masikini.

## F: Mapendekezo kuhusu rasilimali

Kuongeza viwango vya ukuaji katika Afrika na kufanya maendeleo thabiti kufikia Lengo la Maendeleo la Milenia (MDG), ukubwa na ubora wa misaada kutoka nje kwenda nchi za Afrika kusini mwa jangwa la Sahara, hauna budi kubadilika kwa kiwango kikubwa. Misaada kwa nchi hizo sharti iongezeke kwa dola za kimarekani bilioni 25 kwa mwaka kwa kipindi cha miaka mitatu hadi mitano ijayo. Hili sharti liandamane na mabadiliko makubwa katika tabia ya wafadhili katika kutoa misaada, na uendelezaji wa marekebisho katika utawala katika nchi za Afrika. Tunaonyesha kwamba katika mazingira haya, ongezeko hili la misaada linaweza kutumika vizuri. Fedha nyingine hazina budi kutafutwa kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa mfuko wa Fursa za Fedha Kimataifa (IFF).

### Ubora wa misaada

- Ili kukuza ubora wa misaada, hapana budi kuwa na mazungumzo kila mwaka yatakayohusisha Mawaziri wa Maendeleo wa nchi za Shirika la Ushirikiano wa Uchumi na Maendeleo na Mawaziri wa Fedha wa Afrika, pamoja na wawakilishi wa vyama vya kiraia na mashirika ya kimataifa. Mazungumzo haya yawe kuhusu vigezo vya kutoa misaada na kutoa mapendekezo kuhusu utaratibu bora wa utoaji misaada, hasa kati ya nchi zenye mapato ya kati na zile zenye mapato ya chini. Katika nchi ambako utawala na asasi zake ni dhaifu, wafadhili hawana budi kutafuta jinsi ya kutoa kiasi cha fedha kinachotosha na kuweka mtiririko bora wa misaada kupitia njia muwafaka, huku wakizingatia haja ya kuepuka kudhoofisha mifumo ya kitaifa na ya muda mrefu.
- Misaada isiwe na masharti, ipatikane kwa muda uliopangwa, iratibiwe kiasi kwamba iende kwa pamoja na iwe imeshonwa kwenye maamuzi na hatua za bajeti za nchi inayoipokea. Muda wa ahadi ulingane na shabaha ya msaada unaohitajiwa: kwa mfano, misaada kwa ajili ya miundombinu na matumizi ya serikali sharti iwe ya muda mrefu kuliko misaada ya kiufundi.
- Misaada kwa Afrika, kwa kiwango kikubwa, iwe kwa njia ya ruzuku.
- Matumizi ya masharti yanayohusu ubadilishaji wa sera ambayo yanahusishwa na misaada kutoka nje, sharti yapunguzwe kwa kiwango kikubwa. Sharti ziwekwe njia za kukuza uwajibikaji wa pande zote mbili zinazohusika na ufuatiliaji wa utekelezaji. Kazi za mashirika ya fedha ya kimataifa na wafadhili sharti ziunge mkono na siyo kudhoofisha taasisi zinazohusiana na uwajibikaji katika nchi za Afrika. Kwa mfano, mashirika na wafadhili wasaidie nchi kuimarisha kanuni na viwango vya kimataifa na kuepuka adha za utoaji wa taarifa nyingi na zisizo za lazima.
- Kupitia mfumo mpya wafadhili hawana budi kusaidia nchi za Afrika kukabili matatizo yanayotokana na misukosuko ya bei za bidhaa na majanga ya asili.

### Ukubwa wa misaada

- Misaada kwa nchi za Afrika kusini mwa jangwa la Sahara, sharti iongezwe mara mbili. Hii ina maana kwamba iongezwe kwa dola za kimarekani bilioni 25 kwa mwaka kwa miaka mitatu hadi mitano ijayo ili kushamirisha viwango vya kodi vinavyoongezeka kutokana na ukuaji na utawala bora. Kwa kuzingatia maendeleo ifikapo mwishoni mwa kipindi hiki, kiasi kingine cha dola za kimarekani bilioni 25 kwa mwaka hakina budi kutolewa, kwa kutegemea mabadiliko katika ubora wa misaada na maendeleo katika utawala.

### Unafuu wa madeni

- Kwa nchi za Afrika kusini mwa jangwa la Sahara ambazo zinahitaji unafuu katika ulipaji wa madeni, shabaha sharti iwe ufutaji madeni kwa asilimia 100 mapema iwezekanavyo. Hili sharti liwe sehemu ya mpango wa utoaji fedha za misaada ili nchi hizi ziweze kufikia MDG kama ilivyoahidiwa huko Monterrey na Kananaskis. Kigezo kikuu sharti kiwe, fedha zinazosamehewa zitumike kuleta maendeleo, kukua kwa uchumi na kupunguza umasikini katika nchi ambazo zinakuza utawala bora kwa dhati.
- Vilevile, kazi haina budi kuanza mara moja kuweka mkataba wa wazi kuhusu madeni utakaohusisha nchi zote za Afrika kusini mwa jangwa la Sahara zenye mapato ya chini, pamoja na zile ambazo hazimo kwenye mpango wa sasa wa kusamehewa madeni. Mpango huu ufute madeni yenyewe na riba kwa kiwango cha asilimia 100 na uhusishe madeni baina ya nchi na mashirika ya fedha ya kimataifa na yale ya nchi na nchi.
- Kama hatua ya haraka, utoaji fedha sharti uanze mara moja ili kuweza kufuta asilimia 100 ya madeni baina ya nchi na mashirika ya fedha pamoja na riba yake, pale ambako hili ni lazima ili kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs).

### Taratibu za utoaji fedha

- Nchi wafadhili sharti zijifunge mara moja kwenye ahadi ya kutoa mgawo wao wa nyongeza ya dola za kimarekani bilioni 25 kwa mwaka, kiasi ambacho Afrika inahitaji sana.
- Njia za kuongeza maradufu misaada kwa Afrika sharti ziwe pamoja na uanzishwaji haraka wa Fursa za Fedha Kimataifa (IFF).
- Nchi tajiri sharti zilenge kutumia asilimia 0.7 ya mapato yao ya mwaka kwenye misaada, na kuwepo mipango maalum inayoonyesha jinsi ya kutekeleza lengo hili.
- Juhudi nyingine hazina budi kufanywa kuweka mapendekezo yanayotekelezeka kwa

## G: Mapendekezo kuhusu namna ya kufanikisha haya yote

Ili Afrika iweze kubeba jukumu lake kwa ajili ya maendeleo, sharti ipewe sauti zaidi katika kufanya maamuzi yanayoihusu moja kwa moja. Sharti iwe na sauti thabiti katika vikao vya kimataifa, na sharti iwe na uwezo wa kuweka shinikizo kwa nchi tajiri duniani la kuzitaka ziheshimu ahadi zake kwa watu masikini wa Afrika. Aidha, sharti uanzishwe mfumo huru wa kufuatilia na kuhakikisha kwamba yote haya yanatekelezwa.

### Uimarishaji wa asasi za kimataifa za Afrika

- Wabia wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) sharti walenge kuifanya benki hiyo ya maendeleo kuwa taasisi kubwa ya kifedha katika Afrika katika miaka 10 ijayo. Mapendekezo ya kufanya hayo hayana budi kuwasilishwa na rais mpya katika kipindi cha miezi sita tangu kushika madaraka hayo. Wabia nao hawana budi kuunga mkono kwa dhati utekelezaji wa mapendekezo hayo.
- Uboreshaji zaidi wa wajibu wa Tume ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa kwa Afrika (ECA) hauna budi pia kuungwa mkono kwa dhati.

### Kufanya mabadiliko katika mashirika ya kimataifa

#### Mkakati

- Menejimenti za Benki ya Dunia, IMF na WTO hazina budi kutoa kipaumbele cha juu zaidi katika uharakishaji maendeleo ya Afrika. Mapendekezo ya kufanya hivyo hayana budi kuwasilishwa kwenye Bodi za Magavana za Benki ya Dunia na IMF (ingawa ingekuwa vizuri zaidi kwenye mikutano ya mwaka ya asasi hizo ya mwaka 2005, lakini hakika isiwe zaidi ya mikutano ya Machi hadi Mei ya 2006) na kwenye Mkutano wa 2005wa Mawaziri wa WTO.
- Katibu Mkuu wa UN na Kundi la Maendeleo la Umoja wa Mataifa sharti waimarishe uratibu wa mashirika ya UN, fedha na programu kwa ngazi ya nchi mojamoja ili kuboresha ufanisi wake.

#### Fursa

- Nchi za Afrika sharti zipewe fursa kubwa katika asasi za kimataifa, hasa kupitia uwakilishi mkubwa kwenye bodi za Benki ya Dunia na IMF.
- Nafasi za juu za uongozi na utoaji maamuzi katika IMF na Benki ya Dunia sharti viwe mikononi mwa uongozi wa kisiasa wa nchi wanachama. Kwa njia hii, Baraza la kufanya maamuzi, linaloundwa na wawakilishi wa kisiasa wa nchi wanachama, sharti lianzishwe kwa kila asasi.
- Uteuzi wa wakuu wa asasi za kimataifa sharti ufanywe kwa ushindani wa wazi unaotafuta mgombea bora kuliko mazoea ya uteuzi kwa misingi ya utaifa.
- Kila nchi inayopokea misaada, serikali na wafadhili sharti waunde vikundi vya ufuatiliaji vitakavyotathmini ubora wa misaada na uratibu wa wafadhili.
- Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lipanuliwe ili liweze kuwa na uwakilishi mkubwa wa Afrika.

### Kuanzisha taratibu za ufuatiliaji zilizo madhubuti na huru

Kuongeza kasi ya mafanikio ya mapendekezo ya Tume, utaratibu huru, wenye mwelekeo wa makabala wa Tume wa kushauriana, sharti uanzishwe kwa ajili ya kufuatilia na kutoa ripoti ya maendeleo. Huu unaweza kuongozwa na watu wawili mashuhuri, wenye ushawishi na ambao wana uzito katika jumuiya ya kimataifa, mmoja kutoka Afrika na mwingine kutoka jumuiya ya wafadhili, ambao wanaweza kutoa taarifa fupi ya mwaka. Hawa sharti wasaidiwe na kitengo kidogo katika moja ya asasi za Afrika au za kimataifa.



Tony Blair (Mwenyekiti)

Fola Adeola
K. Y. Amoako
Nancy Kassebaum Baker
Hilary Benn
Gordon Brown
Michel Camdessus
Bob Geldof
Ralph Goodale
Ji Peiding
William Kalema
Trevor Manuel
Benjamin Mkapa
Linah Mohohlo
Tidjane Thiam
Anna Tibaijuka
Meles Zenawi

Madhumuni ya Tume ni:

- Kuibua mawazo mapya na vitendo vya kujenga Afrika yenye nguvu na ustawi, kwa kutumia urais wa Uingereza kwenye kundi la nchi tajiri zenye viwanda (G8) na Umoja wa Ulaya katika mwaka 2005;
- Kusaidia miradi mizuri iliyopo sasa katika Afrika, hasa Mpango Mpya wa Ushirikiano kwa Maendeleo ya Afrika (NEPAD) na Umoja wa Afrika, na kuhakikisha kwamba juhudi hizo zinafikia malengo yake;
- Kusaidia kuweka msukumo katika utekelezaji wa ahadi za sasa za kimataifa kwa Afrika;
- Kutoa mwelekeo mpya na wenye matumaini kwa Afrika na tamaduni zake anuwai katika karne ya 21, wenye kuhoji mitazamo isiyo ya haki, na unaosadia kuleta mabadiliko; na
- Kuelewa na kusaidia kupatikana kwa matamanio ya Afrika katika siku za usoni kwa kusikiliza maoni ya Waafrika wenyewe.

Taarifa zaidi juu ya kazi za Tume zinaweza kupatikana kwenye tovuti:
www.commissionforafrica.org

**Tume ya Afrika**

Sehemu yoyote ya chapisho hili yaweza kunakilikwa alimradi itajwe asili yake.